**14 APRILI, 2025**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA TISA**

**Kikao cha Tano – Tarehe 14 Aprili, 2025**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa tuketi.

Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tutaanza na Ofisi ya Rais TAMISEMI, Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake. Kwa niaba yake Mheshimiwa Rashid Shangazi.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally, ninaomba swali lake lipate majibu ya Serikali.

**SPIKA:** Swali lake ni namba 55.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Spika, naam!

**SPIKA:** Taja namba ya swali, namba 55.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally, ninaomba swali lake Na. 55 lipate majibu ya Serikali.

Na. 55

**Ujenzi wa Maboma ya Zahanati na Shule - Nzega**

**MHE. RASHID A. SHANGAZI K.n.y. MHE. AZIZA S. ALLY** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kukamilisha ujenzi wa maboma ya zahanati na shule yaliyojengwa kwa nguvu za wananchi Nzega?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua mchango wa nguvu za wananchi hususan katika uanzishaji wa miradi ya kijamii kama shule na vituo vya kutolea huduma za afya katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2020/2021 hadi 2023/2024, Serikali ilipeleka shilingi bilioni 64 kwa ajili ya maboma ya zahanati na shule. Katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Serikali imetenga shilingi milioni 835 kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma sita ya zahanati na madarasa 17 yaliyoanzishwa kwa nguvu za wananchi katika Halmashauri ya Nzega.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya kukamilisha maboma ya zahanati na madarasa yaliyoanzishwa kwa nguvu za wananchi ili kusogeza huduma za afya ya msingi na elimu karibu na wananchi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Rashid Shangazi, swali la nyongeza.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri kabisa ya Serikali, nina swali moja tu la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa maboma haya mengi yana muda mrefu sana, Serikali haioni umuhimu sasa wa kufanya tathmini ya kina na kuweza kubaini maboma yote nchi nzima ili iweze kutenga bajeti kwa wakati mmoja na kumaliza changamoto ya umaliziaji wa haya maboma? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba wananchi wameitikia wito wa Serikali na kuchangia nguvu zao kwa ajili ya ujenzi wa maboma ya zahanati na madarasa na tayari Serikali ilishafanya tathmini na kuyatambua na kuyaorodhesha maboma yote ya zahanati na madarasa yaliyojengwa kwa nguvu za wananchi na kila mwaka wa fedha Serikali imekuwa ikitenga fedha kwa ajili ya kwenda kuyakamilisha maboma hayo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali itaendelea kutenga fedha kwa awamu ili kukamilisha maboma ambayo yamejengwa kwa nguvu za wananchi. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Yahaya Massare, swali la nyongeza.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Spika, katika Halmashauri ya Itigi yapo maboma mengi ya shule katika kata karibu zote, lakini na maboma ya zahanati. Je, Serikali ipo tayari sasa kupeleka fedha katika Halmashauri ya Itigi kumalizia maboma haya ambayo wananchi walijitolea? Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, Serikali ipo tayari kupeleka fedha kwa ajili ya kumalizia maboma

ya zahanati na madarasa katika Halmashauri ya Itigi na imekuwa ikifanya hivyo kila mwaka wa fedha na zahanati kadhaa zimekamilishwa, lakini madarasa yamekamilishwa. Nimhakikishie Mheshimiwa Massare kwamba tutaendelea kuweka kwenye bajeti ya kila mwaka ili kukamilisha maboma hayo ya zahanati na shule katika Halmashauri ya Itigi. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda, Mbunge wa Viti Maalum; kwa niaba yake Mheshimiwa Festo Richard Sanga.

Na. 56

**Kulitengeneza na Kulitangaza Daraja la Mungu – Rungwe**

**MHE. FESTO R. SANGA K.n.y. MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA** aliuliza:-

Je, lini Serikali italitengeneza na kulitangaza Daraja la Mungu la kihistoria lililopo Wilaya ya Rungwe ambalo lipo katika hali ya kutotunzwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Daraja la Mungu lililopo Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe limetokana na mabadiliko asili ya miamba na kulifanya kuwa ni daraja ambalo halikuwahi kutengenezwa na mwanadamu hivyo kuwa kivutio cha utalii wa ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na sababu hiyo, daraja hili haliwezi kutengenezwa kwa njia za kibinadamu hivyo litaendelea kuwa la asili kama lilivyo kwani halitumiki kwa shughuli nyingine za kibinadamu isipokuwa kwa utalii pekee.

**SPIKA:** Mheshimiwa Festo Sanga, swali la nyongeza.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Spika, ninaishuruku Serikali kwa majibu mazuri ambayo imeyatoa, lakini hukohuko Rungwe kuna daraja lingine ambalo linaunganisha Makete na Rungwe, kwa maana ya Kata ya Kigulu na Kata nyingine ya Mbigili. Je, ni lini Serikali itajenga daraja hilo ambalo kwa kweli linatumika na wananchi wengi na hadi sasa niseme wazi hicho Kijiji cha Kigulu hakijawahi kuona hata gari, lakini wanategemea daraja hilo lijengwe, ni yapi maelekezo ya Serikali hasahasa kwenye ule mradi ambao umekuwa ukisaidia maeneo kama haya?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Ni kweli kwamba kuna daraja ambalo linaunganisha Halmashauri ya Wilaya ya Makete Mkoani Njombe na Halmashauri ya Rungwe Mkoani Mbeya na ni daraja la muhimu sana kwa wananchi wa Wilaya ya Makete na Wilaya ya Rungwe. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali ilikwishalitambua hitaji la daraja katika eneo hilo na tunaendelea kutenga fedha kwa ajili ya kwenda kujenga daraja lile ili wananchi wa Rungwe na wa Makete na Mikoa ya Njombe na Mbeya ipate mawasiliano ya uhakika zaidi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri kwanza sijaelewa kwa nini hili swali lililetwa TAMISEMI badala ya kuelekea Utalii, kwa sababu kwa namna lilivyoulizwa siyo daraja la kawaida kama ambavyo majibu yanasema. Sasa sijajua kwa nini lilikuja kwenu TAMISEMI. Ninadhani hili swali linapaswa kujibiwa na watu wa Maliasili kuliko kujibiwa na TAMISEMI; kwa sababu linasema, je, lini Serikali itatengeneza na kulitangaza Daraja la Mungu la kihistoria. Ninadhani ni ule utengenezaji wa kuliweka katika hali ambayo liendelee kuwepo badala ya kupotea, sasa sijui kwa nini lilikuja TAMISEMI. Ninadhani ni swali lenu Maliasili, kwa hiyo litaletwa kwenu ili muweze ninyi kulijibu watu wa Maliasili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, Mbunge wa Nanyamba, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Agnes Hokororo.

Na. 57

**Uhaba wa Walimu Nanyamba**

**MHE. AGNES E. HOKORORO K.n.y. MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itatatua changamoto ya uhaba wa Walimu katika Halmashauri ya Mji Nanyamba?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa spika, Serikali inatambua changamoto ya uhaba ya walimu katika shule za Msingi na Sekondari nchini. Katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Serikali imeajiri walimu 15,925 ambapo walimu 27 na mafundi sanifu maabara wawili wamepangwa Halmashauri ya Mji Nanyamba. Serikali itaendelea kuajiri walimu na kuwapanga katika shule zenye upungufu katika Halmashauri ya Nanyamba. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Agnes Hokororo, swali la nyongeza.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, ninaomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; baadhi ya Halmashauri za miji kama Nanyamba, Newala na Masasi zina mwonekano wa vijijini kibajeti, kwa maana ya kuwa na bajeti ndogo; je, Serikali haioni ipo haja ya kuweka mgao sawa wa walimu katika halmashauri hizo changa au mpya?

Mheshimiwa Spika, …

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri keti kwanza, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya. Mheshimiwa Agnes Hokororo swali la pili.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Spika, Shule ya Sekondari Dinyecha ina wanafunzi zaidi ya 818; kwa kidato cha tano na cha sita, ni wasichana lakini ina upungufu mkubwa sana wa walimu wa sayansi. Je, Serikali ina mkakati gani wa dharura wa kuwaokoa hawa wasichana kwa sababu pia kuna mkakati wa kuwafanya wasichana wasome sayansi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, Halmashauri za Miji Nanyamba, Masasi na halmashauri nyingine zote kote nchini zinapewa watumishi wa Sekta ya Elimu kwa maana ya walimu kwa kuzingatia upungufu ya idadi ya walimu waliopo katika halmashauri hizo na si kwa kuzingatia hadhi kwamba ni halmashauri za mji. Kwa hivyo, katika utaratibu wetu wa ajira tumeweka makundi matatu: kundi la kwanza ni mikoa na halmashauri zenye upungufu mkubwa zaidi wa walimu; lakini kundi la pili ni upungufu wa wastani; na kundi la tatu ni zile halmashauri na mikoa yenye upungufu mdogo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, kuwa halmashauri ya Mji haiathiri ikama ya watumishi wanaopelekwa kwa sababu kigezo ni kujua watumishi wangapi wanahitajika, wangapi wapo na hivyo tunapeleka kwa kipaumbele kwenye halmashauri zile zenye upungufu mkubwa ikiwemo Nanyamba, Masasi na halmashauri nyingine kote nchini.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na Shule ya Sekondari Dinyecha ambayo ina upungufu mkubwa wa walimu wa sekondari kwa maana ya walimu wa sayansi, ninaomba nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba katika ajira za Sekta ya Elimu, Serikali imeweka kipaumbele kikubwa zaidi kwa

walimu wa sayansi na walimu hao wamekuwa wakiajiriwa na kupelekwa kwenye shule zote zenye upungufu mkubwa zaidi wa walimu hao wa sayansi. Kwa hivyo, tutahakikisha pia shule ya Sekondari Dinyecha tunaitazama kwa jicho la karibu ili iweze kupata waalimu hao na kuboresha huduma za elimu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Shamsia, swali la nyongeza.

**MHE. SHAMSIA A. MTAMBA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kunipatia nafasi ili niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Tatizo lililopo Nanyamba linafanana kabisa na tatizo lililopo katika Jimbo la Mtwara Vijijini. Je, ni lini Serikali itatatua changamoto ya uhaba wa walimu katika Jimbo la Mtwara Vijijini? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Mtwara na Halmashauri zake zote ni moja ya mikoa 10 ambayo tumeitambua kwamba ni mikoa yenye upungufu mkubwa zaidi wa watumishi wa sekta zote ikiwemo Sekta ya Elimu; ikiwemo Halmashauri ya Mtwara Vijijini. Ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Shamsia kwamba Halmashauri yake ni moja ya halmashauri ambazo zimewekewa kipaumbele na kwenye kila ajira za kila mwaka tumekuwa tukipeleka watumishi wengi zaidi na tunaendelea kufanya hivyo ili kuweza kupunguza pengo la walimu katika halmashauri hiyo. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Minza Simon Mjika, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake. Kwa niaba yake, Mheshimiwa Esther Midimu.

Na. 58

**Ujenzi wa Miundombinu ya Maji Shuleni**

**MHE. ESTHER L. MIDIMU K.n.y. MHE. MINZA S. MJIKA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani kujenga miundombinu ya maji shuleni ili kuepuka milipuko ya magonjwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, shule 5,311 za Sekondari zina vyanzo vya maji vya uhakika ambapo shule zenye maji ya bomba ni 2,960, visima shule 1,217 na wanaovuna maji ya mvua ni shule 1,134. Aidha, shule 20,509 za msingi zina vyanzo vya maji vya uhakika ambapo shule zenye maji ya bomba ni 10,965, visima shule 4,966 na shule zinazovuna maji ya mvua ni 4,578.

Mheshimiwa Spika, Mikakati ya Serikali ya kujenga miundombinu ya maji shuleni ili kuepuka milipuko ya magonjwa ni pamoja na kuhakikisha kuwa: -

(a) Ujenzi wa shule mpya unajumuisha miundombinu ya maji inayohusisha kuvuna maji ya mvua, kuunganisha na mifumo ya Mamlaka za Maji na kuchimba visima;

(b) Ujenzi wa miundombinu ya vyoo unajumuisha wa miundombinu ya maji tiririka; na

(c) Kutumia sehemu ya fedha ya ruzuku ya uendeshaji wa shule kukarabati miundombinu ya maji.

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Midimu, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza. Je, ni lini sasa Serikali itapeleka hiyo miundombinu ya maji katika shule zilizobaki? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na zoezi hili ni endelevu la kuboresha miundombinu ya maji katika shule zetu katika Mkoa wa Simiyu na katika mikoa yote kote nchini. Kwa hivyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wote kwamba tutaendelea katika kila bajeti ya mwaka kutenga fedha kutoka vyanzo mbalimbali kwa ajili ya kuboresha huduma za maji katika shule zetu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Grace Tendega, swali la nyongeza.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza. Ni nini mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba shule zinazojengwa sasa zinawekewa miundombinu ya uvunaji wa maji ya mvua ili kuzisaidia ziweze kupata maji safi na salama? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, Mkakati wa Serikali ni kwamba tumetoa maelekezo na mwongozo rasmi kwamba shule zote zinazojengwa, lakini pia vituo vya huduma za afya lazima kwanza viwe na miundombinu ya kuvuna maji ya mvua ikiwemo kufunga gata kwenye majengo yote, lakini kuchimba visima kwa ajili ya kuhifadhi maji ya mvua. Kwa hiyo, zoezi hilo linafanyika na shule zote, kwa mfano za mikoa 26 za wasichana zote zina miundombinu hiyo mahususi kwa ajili ya kuvuna maji, lakini shule ambazo zimejegwa hivi sasa za *SEQUIP* zimeendelea pia kuwekewa miundombinu ya maji. Zoezi hili ni endelevu, tutaendelea kulisimamia kuhakikisha watoto wetu wanapata maji ya uhakika katika shule zao. Ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Khamis Yussuf Mussa, Mbunge wa Kwahani, sasa aulize swali lake.

Na. 59

**Nishati ya Gesi Kutumika kwenye Magari – Zanzibar**

**MHE. KHAMIS YUSSUF MUSSA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itainufaisha Zanzibar katika matumizi ya nishati ya gesi kutumika katika magari?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Judith Kapinga, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, mwezi Februari, 2022, Serikali kupitia Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania *(TPDC)* iliingia makubaliano ya ushirikiano na Shirika la Maendeleo ya Petroli Zanzibar *(ZPDC)* ambapo kupitia ushirikiano huo masuala mbalimbali yamekuwa yakifanyika ikiwemo kubadilishana ujuzi na utaalam. Katika ushirikiano huu, suala la kupeleka gesi asilia Zanzibar ni mojawapo ya *agenda* kuu. Pande zote mbili bado zinaangalia namna bora ya kufikisha gesi asilia Zanzibar ili iweze kupatikana kwa bei rafiki kwa watumiaji.

**SPIKA:** Mheshimiwa Khamis Yussuf Mussa, swali la nyongeza.

**MHE. KHAMIS YUSSUF MUSSA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa majibu mazuri ya Serikali. Pamoja na majibu hayo mazuri nina swali moja la nyongeza pamoja na ushauri.

Mheshimiwa Spika, swali langu lipo hivi, je, Serikali imejipangaje katika kutoa elimu juu ya matumizi ya gesi katika magari Visiwani Zanzibar?

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu ni kwamba mafunzo yatakapotolewa yawalenge hasa watumishi wa Serikali pamoja na Wizara na Mashirika ili wao ndiyo wawe changamoto kubwa sana katika kuwashajihisha watumiaji wengine binafsi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa swali la Mheshimiwa Mbunge. Kama ambavyo nimetangulia kusema tutaendelea kushirikiana na wenzetu wa *ZPDC* kwa sababu tayari tuna ushirikiano basi na hilo la lenyewe tutalichukua kwa ajili ya kufanya kazi kwa pamoja na wao waweze kulichukua na kulifanyia kazi kwa upande wa Zanzibar. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Maji, Mheshimiwa Francis Isack Mtinga, Mbunge wa Iramba Mashariki, sasa aulize swali lake.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Spika, …

**SPIKA:** Mheshimiwa Yahaya Massare ninaona umesimama ili uulize kwa niaba yake.

Na. 60

**Vijiji Vilivyopo Kando ya Mradi wa Maji wa Ziwa Victoria Kupatiwa Maji – Mkalama**

**MHE. YAHAYA O. MASSARE K.n.y. MHE. FRANCIS I. MTINGA** aliuliza:-

Je, nini mpango wa kuhakikisha Vijiji vya Mkalama vilivyopo umbali wa Kilometa 20 litakapopita Bomba la Mradi wa Maji wa Ziwa Victoria vinapata maji?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Mhandisi Kundo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa Mradi wa Kutoa Maji Ziwa Victoria kwenda

Mikoa ya Singida na Dodoma unaotarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2025. Mradi huo utakapotekelezwa unatarajia kuhudumia Miji ya Singida na Dodoma pamoja na vijiji vilivyo ndani ya umbali wa kilometa 12 kutoka kila upande wa bomba kuu ikiwemo Vijiji vya Wilaya ya Mkalama. Aidha, vijiji vitakavyokuwa nje ya kilometa 12, Serikali itavipelekea huduma ya Mradi wa Ziwa Victoria baada ya awamu ya kwanza ya mradi huo kukamilika na kuanza kutoa huduma.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa jumla ya vijiji 29 kati ya 70 vya Wilaya ya Mkalama vinapata huduma ya majisafi na salama kupitia mtandao wa bomba wakati vijiji 41 vinapata huduma ya maji kupitia *point source* na pampu za mkono. Vilevile, Serikali inaendelea na utekelezaji wa jumla ya Miradi Sita ya Mbigigi, Isene – Matongo, Mdilika, Tumuli, Singa na Mwangeza ambapo kukamilika kwake kutanufaisha wananchi zaidi ya 15,000 waishio kwenye Vijiji Saba vya Wilaya ya Mkalama.

**SPIKA:** Mheshimiwa Yahaya Massare, swali la nyongeza.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri sana ambayo yanatia matumaini kwa wananchi wa Mkoa wa Singida, lakini na Mkoa wa Dodoma, nina swali moja tu la nyongeza. Je, Serikali sasa iko tayari wakati inafanya upembuzi yakinifu kuhusisha Mji wa Itigi katika Mradi huu wa Maji wa Ziwa Victoria wakati unakuja Dodoma kutokea Singida?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua uhitaji wa maji kwa wananchi wake wote na ipo tayari kufanya hivyo Itigi na maeneo mengine ya Mikoa ya Singida na Dodoma.  Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Hussein umesimama lakini una swali lako la msingi. Haya swali la nyongeza.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Spika, ni lini Serikali itaanza kufunga mita za *prepaid* kwa Mkoa wa Geita na Wilaya yake ya Nyang'hwale? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, Serikali kwa utaratibu wake na kwa maelekezo ya Mheshimiwa Rais, tayari tumeshaanza kufunga *prepaid water meter* katika maeneo mengine. Pia ni maelekezo ya Serikali kuendelea kufunga mita ili kuendelea kuondoa malalamiko ya *bill* ambazo wananchi wanadhani kwamba kwa namna moja au nyingine siyo *bill* halisi kwa ajili ya matumizi yao. Kwa hiyo, yako maelekezo mahsusi kwa Mkoa wa Geita pamoja na Wilaya ya Nyang'hwale pia ya kuhakikisha kwamba tunafunga *prepaid water meter*. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Boniphace Butondo, swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Bomba hili litakalokuwa linasafirisha maji kutoka Ziwa Victoria litakuwa linapitia Ihelele huko Mwanza. Pia, litakuwa linapitia katika wilaya ya jirani kabisa ambayo ni Kishapu, Kata ya Busangwa, Kata ya Mondo, Kata ya Sekebugolo na Kata ya Bubiki; ambazo ni kata zilizomo ndani ya kilometa 12…

**SPIKA:** Mheshimiwa Butondo, ni swali la nyongeza. Ni swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Spika, Serikali inasema nini juu ya hatua ya utelekelezaji wa mradi huu kunufaisha wananchi wa Kishapu? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ninafahamu kiu ya Mheshimiwa Butondo kwa wananchi wake wa Kishapu na Serikali tunatambua kiu hiyo kwa sababu ndiyo dhamira ya Serikali ya Chama Cha Mapinduzi kuhakikisha watu wake wanapata huduma ya maji safi na salama. Hivyo, nimtoe wasiwasi, Serikali itahakikisha katika upembuzi yakinifu tunaangalia namna bora ya kuhakikisha kwamba tunawafikishia maji, lakini kwa gharama ambayo haitakuwa na changamoto. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Shabani Shekilindi, swali la nyongeza.

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru na ninaishukuru Serikali imetupa shilingi 1,800,000,000 kwa ajili ya kujenga mradi wa maji, lakini ule mradi wa maji, bomba zake zimechomwa moto na mtu na mtu huyo aliyezichoma moto anajulikana. Je, ni nini kauli ya Serikali kwa watu wanaohujumu miundombinu ya maji kwa makusudi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, ninasikitika kwamba hili ni kosa kama makosa mengine ambapo huyo mtu anatakiwa kuchukuliwa hatua za kisheria na sisi kama Wizara ya Maji na Serikali hatutosita kuchukua hatua kwa mujibu wa sheria ambayo inaongoza maeneo hayo kwa watu wote wanaohujumu miundombinu, huduma zetu na hata michakato ya ujenzi wa huduma za maji kwa wananchi wetu. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kasalali Mageni, swali la nyongeza.

**MHE. KASALALI E. MAGENI:** Mheshimiwa Spika, Mradi wa Kupeleka Maji ya Bomba kutoka Ziwa Victoria katika Jimbo la Sumve kupitia Kata ya Mantale na Malya umekuwa ukisuasua kutokana na malipo kucheleweshwa kwa mkandarasi. Je, Serikali haioni umuhimu wa kumlipa kwa wakati mkandarasi huyu ili mradi huu ukamilike kwa muda kama ilivyopangwa? Ninashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, Serikali tunatambua uhitaji wa wakandarasi wetu kulipwa ili kuendelea kutekeleza miradi hii ili iweze kukamilika kwa wakati na iweze kutoa huduma ya maji ambayo imetarajiwa. Pia, ninatambua kwamba Mheshimiwa Mageni amekuwa akiupigania sana Mradi huu wa Ziwa Victoria kwa upande wa Sumve – Mantale na sisi tulishapokea hati za madai na tayari tumeshapeleka Wizara ya Fedha kwa ajili ya malipo ili mkandarasi aweze kuharakisha utekelezaji wa mradi huo. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, Mbunge wa Vwawa, sasa aulize swali lake.

Na. 61

**Mradi wa Maji Vwawa**

**MHE. JAPHET N. HASUNGA** aliuliza:-

Je, lini Mradi wa Maji wa Ichenjezya, Hasamba, Nwansana, Vwawa hadi Ilolo utakamilika na kuanza kutoa maji ya uhakika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na utekelezaji wa Mradi wa Upanuzi wa Mtandao wa Maji Vwawa – Mlowo pamoja na Mradi wa Ukarabati wa Vyanzo vya maji Mwansyana na Mlowo. Utekelezaji wa Mradi huo wa Vwawa – Mlowo umefikia wastani wa 79% wakati Mradi wa Ukarabati wa Mwansyana – Mlowo umefikia wastani wa 94%. Tayari baadhi ya maeneo ya Mlowo *Forest,* Izyla, Saganoti, Malenje, Segerea, Mbimba, Ilolo Shule na Namleya yameanza kupata huduma ya maji kupitia miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, Miradi hiyo inatarajiwa kukamilika mwezi Mei, 2025 na kunufaisha wananchi wapatao 36,744 waishio kwenye Maeneo ya Hasamba, Ilolo, Vwawa, Ichenjezya, Mlowo

Mabatini, Mlowo Mjini, Tazara, Kiwandani, Ichenjezya, Isangu, Hasanga, *Mlowo Forest,* Izyla, Saganoti, Malenje, Segerea, Mbimba, Ilolo Shule na Namleya.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hasunga, swali la nyongeza.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, ninashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; kwa kuwa, wakandarasi wote wawili wa Mwansyana hadi Vwawa na wa Ichenjezya hadi Vwawa kwa muda mrefu walikuwa wameshaondoka *site* na wameacha kutekeleza ule mradi. Ni nini kauli ya Serikali kuhakikisha kwamba hawa wakandarasi wanarudi kazini ili waweze kutekeleza mradi huo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa kuwa, tulikubaliana na Serikali suluhu ya muda mrefu na Serikali ikatoa fedha zaidi ya shilingi bilioni saba, ni kuleta mradi wa maji kutoka Mafumbo kuja kuungana na huu mradi ili kuweza kutatua tatizo la maji. Ni lini Mradi huu wa Maji wa Mafumbo utakamilika? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa swali zuri la Mheshimiwa Hasunga na kwa kazi nzuri ambayo anaendelea kuifanya katika jimbo lake; kwa hakika amekuwa mwakilishi mwema na ni kweli anafanya kazi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa wakandarasi ambao wameondoka *site,* Mheshimiwa Waziri wa Maji, Mheshimiwa Jumaa Hamidu Aweso alimwelekeza Mheshimiwa Katibu Mkuu *Engineer* Mwajuma Waziri, kuhakikisha anakaa na hao wakandarasi na kuangalia namna bora zaidi ya kwenda kuhakikisha kwamba jambo hili linatatuliwa; hata kama wana madai basi madai hayo yatawafuata wakati wakiwa wanaendelea na utekelezaji wa miradi hiyo kwa sababu

tunatambua umuhimu mkubwa wa miradi hii kukamilika ili iweze kuwasaidia wananchi.

Mheshimiwa Spika, vilevile, kwa upande wa swali la pili, Mradi wa Mafumbo ni mradi wa kimkakati na ni mradi ambao unakuja kuleta suluhisho la kudumu katika Jimbo la Mheshimiwa Hasunga. Sisi Serikali tunaendelea kuhakikisha kwamba jicho letu haliondoki pale kuhakikisha kwamba mradi huu unakamilika.

Mheshimiwa Spika, mradi huu ulikuwa na changamoto mbili, tatu, lakini tunaelekea kuzikamilisha na zitakapokamilika, mtiririko wa fedha na kasi ya ufanyaji wa kazi itakuwa ni kubwa na hatimaye kazi hii itakamilika na wananchi wa eneo hilo watapata huduma ya maji safi na salama na yenye utoshelevu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, moja kwa moja kwenye swali. Mheshimiwa George Malima, swali la nyongeza.

**MHE. GEORGE N. MALIMA:** Mheshimiwa Spika, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Mradi wa Maji wa Kisokwe – Idilo – Mazae ulioko katika Mji wa Mpwapwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua uhitaji wa ukamilishaji wa miradi mingi inayoendelea na kuna miradi zaidi ya 1,000 chini ya Wizara ya Maji nchi nzima, miradi ya kimkakati, miradi ya kitaifa, mabwawa na kadhalika. Lengo letu ni kuhakikisha kwamba ndani ya mwaka huu wa fedha ifikapo Oktoba, basi miradi hii iwe imekamilika ikiwemo na miradi ambayo Mheshimiwa Mbunge ameitaja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki, swali la nyongeza.

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI:** Mheshimiwa Spika, ni lini Serikali itawalipa wakandarasi wa Miradi ya Maji Kata ya Zanzuwi, Kata ya Mwamashimba na Kata ya Malampaka ambao wameomba

kulipwa hela zao toka mwaka 2024 ili waendelee kukamilisha miradi ambayo iko kwenye maeneo hayo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Mashimba Ndaki kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Mashimba Ndaki kwanza kwa ushirikiano anaotupatia Wizara ya Maji, lakini pili kwa kutoa ushirikiano tunapokuwa na miradi ndani ya jimbo lake na tatu ni kwa namna ambavyo anatekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kumekuwepo na madai ya wakandarasi katika Wilaya ya Maswa, lakini tumekuwa tukilipa hatua kwa hatua. Mpaka sasa madai ambayo wameshayaleta wakandarasi kutoka Maswa, tayari Katibu Mkuu ameshayapeleka Wizara ya Fedha, kwa ajili ya kupata idhini ya malipo ili waweze kuendelea na mradi huo na ukamilike kwa wakati. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Condester Sichalwe, swali la nyongeza.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kunipatia nafasi. Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru sana ulifanya ziara kwenye Jimbo la Momba tarehe 14 Januari, 2025. Ukaahidi miezi mitatu Mradi wa Msangano mpaka kufikia sasa tupate maji na Mradi wa Lwatwe, mwezi mmoja mpaka tupate maji, lakini mpaka sasa hivi hakuna ambacho kinaendelea. Ni nini kauli yako ya faraja kwa wananchi wa Jimbo la Momba?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ninatambua na ninafahamu kwamba nilikuwepo na Mheshimiwa Condester

katika jimbo lake na tulifanya mkutano wa hadhara na Serikali ilitoa ahadi.

Mheshimiwa Spika, ni kwamba, wakati tunatoa ahadi kulikuwa na miradi mingine iliyokuwa inaendelea ambayo pia ilikuwa inahitaji fedha kwa wakati huo huo. Pia, katika jimbo ambalo Serikali imepeleka miradi mingi ya maji katika kipindi cha miaka mitano ni pamoja na Jimbo la Mheshimiwa Condester.

Mheshimiwa Spika, tunapokea changamoto hii na tutaendelea kuifanyia kazi ili kuhakikisha kwamba lazima ahadi ya Serikali kwa wananchi ni inatekelezwa. Sisi Wizara ya Maji tuko tayari kuhakikisha kwamba tunachukua hatua kali kwa viongozi wetu ambao tumewapa majukumu ya kutekeleza ili waweze kutekeleza kwa wakati na wananchi wapate huduma ya maji safi na salama. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Suma Fyandomo, swali la nyongeza.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Mradi wa Maji wa Kiwila ambao unategemewa sana na wananchi wa Mbeya Jiji pamoja na Mbalizi, mkataba wake ilikuwa uishe mwezi huu wa Aprili na Machiu. Sasa je, ni lini wananchi wa Mbeya Jiji watakamilishiwa mradi huo? Ukizingatia kauli kubwa ya Mama Samia Suluhu Hassan ni "kumtua ndoo mama kichwani." Ninaomba majibu Wanambeya Jiji pamoja na Mbalizi wasikie. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ninatambua na Serikali inatambua umuhimu wa Mradi huu wa Kiwila. Ni mradi mkubwa, nimeshaenda kuutembelea na nimeuona. Pia, tunafahamu kabisa kwamba, wakati tunaanza kufanya kazi kulikuwa na baadhi ya changamoto kwenye *source,* kule kwenye *intake,*

ambayo ndiyo iliyochelewesha. Pia, tunafahamu kabisa kwamba mradi huu ndiyo mwarobaini wa wana Mbeya na Jiji la Mbeya na Serikali tumejizatiti kuhakikisha kwamba mradi huu unakamilika kwa wakati ili Wananchi wa Jiji la Mbeya waweze kupata huduma ya maji safi na salama. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, hapo kwenye wakati hapo, mmeshaongeza muda gani? Miezi sita, mwaka au miaka miwili? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ili Serikali itoe jibu la uhakika, ninaomba tulifanyie kazi halafu tutamrejea muuliza swali. Ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Fredy Atupele Mwakibete, swali la nyongeza.

**MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Ni lini Serikali itakamilisha miradi inayojenga katika Bonde la Mwakaleli, hususan Kata za Luteba, Isange, Kandete na Mpombo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, miradi hiyo iko ndani ya muda wa mkataba na tunaamini kwamba mpaka kufikia kwa mujibu wa mkataba jinsi ambavyo umesainiwa, miradi hiyo itakuwa imekamilika. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, swali la nyongeza.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niulize swali la nyongeza. Kutokana na shida kubwa ya maji tuliyonayo Urambo, je, ni lini maji kutoka *Lake* Victoria yatafika? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ninatambua namna ambavyo Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta anawapambania wana Urambo na tunatambua kwamba mradi huu ni *extension* ya Mradi wa Ziwa Victoria uliogharimu shilingi bilioni 680. Pia, tunatambua huu ni mradi wa *extension* ya kwenda Urambo, Sikonge pamoja na Kaliua. Ambapo una jumla ya *package* ya bilioni 143, lakini pia mradi huu umefikia ziadi ya 50% na sasa tunatarajia kwamba kabla mradi haujakamilika, tumetoa *option* ya kuhakikisha kwamba maeneo mengine yanaweza kuanza kupata huduma ya maji wakati mradi ukiwa unaendelea.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, namtoa hofu, tayari ma-*engineer* wetu wanafanyia kazi maelekezo haya na wananchi wataanza kupata maji safi na salama kutoka Ziwa Victoria. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Afya, Mheshimiwa Kabula Enock Shitobelo, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Neema Lugangira.

Na. 62

**Majibu ya Tafiti za Kansa Kanda ya Ziwa**

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA K.n.y. MHE. KABULA E. SHITOBELA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itatoa majibu ya tafiti zilizofanywa Kanda ya Ziwa kubaini visababishi vya kansa iliyokithiri?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imefanya utafiti wa kina nchi nzima wa kusaidia kutambua kuwa ni saratani zipi zinaongoza katika Kanda ya Ziwa na kubaini kuwa saratani ya kibofu cha mkojo, saratani ya mji wa uzazi wa akinamama, saratani ya damu, macho na figo ndiyo zinazoongoza.

Mheshimiwa Spika, aidha, wataalam wamekusanya sampuli za damu 9600 za watu ambao hawana saratani ili kulinganisha na sampuli za damu za wenye saratani. Utafiti huu utasaidia kubaini chanzo cha hizo saratani. Hivyo kwa sasa bado utafiti unaendelea na visababishi vinavyosemwa bado ni nadharia tu kutokana na shughuli za kijamii katika maeneo husika.

Mheshimiwa Spika, hadi sasa mpango wa kudhibiti ongezeko umejikita katika kutoa elimu ya afya kwa viashiria vinavyodhaniwa pamoja na kuzingatia mkakati wa kitaifa wenye maeneo saba yaliyoainishwa ili kudhibiti viashiria vya saratani.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Neema Lugangira, swali la nyongeza.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Spika, Pamoja na maelezo ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuzingatia kuwa katika Mikao ya Kanda ya Ziwa kuna shughuli nyingi za Sekta ya Madini na uchepushaji wa kemikali kwenda kwenye Ziwa Victoria unasemekana kuweza kuathiri samaki na dagaa ambazo jamii inayozunguka Ziwa Victoria wanakula. Hivyo, kuna uwezekano wa kuchangia katika ongezeko la kansa. Sasa je, Wizara ya Afya hamwoni ipo haja ya Serikali kuwa na chombo maalum cha kudhibiti masuala yote ya chakula, lishe na usalama wa chakula kwa maana ya *food safety*? Hilo ni swali la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa, Wizara ya Afya hapa kwenye majibu imeeleza kwamba inajikita katika kutoa elimu, ninaamini elimu hii ni pamoja na masuala ya usalama wa chakula kwa maana ya *food safety*. Je, Wizara haioni iko haja kwa Serikali kufuata miongozo ya dunia ikiwemo Shirika la Afya

Duniani, kwamba masuala ya udhibiti wa usalama wa chakula kwa maana ya *food safety* yawe chini ya Wizara ya Afya na siyo chini ya *TBS? (Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kuuliza masuala muhimu ya afya na muhimu sana kwa usalama wa afya zetu, lakini pia kwa usalama wa nchi yetu. Ninakushukuru sana Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maswali yake mawili: swali la kwanza kama Serikali haioni sababu ya kuwa na chombo maalum cha kusimamia usalama wa chakula. Serikali ina chombo maalum ambacho kwa sasa masuala ya chakula yanasimamiwa na *TBS*. Pia, Serikali imekuwa inafanya kazi ya kina kuhakikisha uchafuzi unaofanyika na mambo hayo mengine ambayo yanaweza yakaleta madhara kwa binadamu yanasimamiwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kuna usimamizi wa kina sana. Hata hivyo, ninakubaliana na wewe kwamba, bado kuna watu ambao sio wazuri na hawafuati zile sheria ambazo wenzetu wa afya, wenzetu wa mazingira na wenzetu wa maji wamezitoa katika kuchepusha vitu mbalimbali ambavyo vinaweza vikawa na madhara kwa binadamu. Kwa hiyo tutaendelea kuongeza nguvu katika kufuatilia eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, suala lake la pili, kwamba ni suala la kurudisha chakula kutoka *TBS* kuja *TMDA* kwa maana ya kuwa *FDA* kama ambavyo tulikuwa zamani. Kwanza, Mheshimiwa Mbunge isisahaulike kwamba suala hilo lilipitia hapa Bungeni na likaamuliwa na Bunge kwamba iende *TBS*. Sasa tunamwomba Mheshimiwa Mbunge aendelee kuipa Serikali muda ndani ya Wizara husika kuna mchakato unaoendelea wa kujadiliana kuona sababu ambazo zilisababisha ziende kule *TBS* kama inawezekana, basi tukatafuta sababu ya kuweza kurudisha kama ambavyo Bunge kwa wakati wote limekuwa likishauri. Tunaomba aendelee

kutuvumilia mara nyingi tumesikia akilisimamia hilo, lakini kwa kweli mjadala unaendelea kwa ajili ya kutekeleza hilo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Mkundi, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa takwimu zinaonyesha idadi kubwa ya wagonjwa walioko Hospitali ya *Ocean Road* wakipata huduma kutokana na matatizo ya saratani wanatoka Kanda ya Ziwa na Hospitali ya Rufaa ya Bugando ina Kitengo cha Saratani. Ni kwa nini Serikali isiimarishe Kitengo hiki kwenye Hospitali ya Rufaa ya Bugando ili kupunguza gharama kwa wagonjwa wa saratani wanaotumia gharama kubwa kwenda Hospitali ya *Ocean Road?* Ninashukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge. Utafiti unaonyesha baada ya hili swali kuwa linaibuka kila wakati na umefanyika utafiti unaonyesha wagonjwa wengi walioko *Ocean Road* wanatokea Kanda ya Kaskazini. Pamoja na hayo haizuii kwamba Serikali, imeshatoa zaidi ya shilingi bilioni nane kwenye Hospitali yetu ya Bugando kwa ajili ya kuboresha hili eneo la *cancer*. Kwa kweli lengo na maelekezo ya Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ni sisi baada ya uboreshaji uliofanyika *Ocean Road* sasa tuanze kuboresha hospitali zote za kanda ikiwezekana kwamba wagonjwa wawe wanabaki kwenye hospitali zao za kanda, wachache sana wawe na sababu ya kuja Dar es Salaam, *Ocean Road*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo swali la Mheshimiwa Mbunge ni zuri na linaenda kutekelezwa kwa nguvu sana na ni maelekezo ya Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge mmerejea tena, mnaanza na maelezo marefu mnajinyima wenyewe fursa ya kuulizwa maswali. Nenda moja kwa moja kwenye swali unapopewa fursa. Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa waathirika wa huu ugonjwa wa *cancer*, kuna wengi ambao hawana uwezo kwa gharama ya Bima ya Afya ...

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati, uliza swali, nenda moja kwa moja.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, Serikali inawasaidiaje wananchi ambao wanaugua *cancer*, hawana uwezo wa matibabu wala bima ya afya? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, ndiyo maana wakati uliopita niliwahi kusema hapa kwa takwimu za miaka miwili iliyopita kwamba Serikali ilitumia shilingi bilioni 667 kwenye eneo la kusaidia watu wasioweza kulipia tiba. Pia, ni kweli kwamba, ni ukweli pamoja na kutumia shilingi bilioni 667 bado haijaweza kuwasaidia wote waliohitaji kupata hiyo huduma. Kwa hiyo, ndiyo maana tumekuja na Bima ya Afya kwa Wote, lakini tutaendelea kuongeza nguvu kwenye hilo na ndiyo maana tunasisitiza sana mapato ya ndani na Utalii Tiba. Tunaposisitiza Utalii Tiba ina maana watu wanaotoka nje kuja kutibiwa wanapoacha fedha ndani basi fedha hizo zinaenda kusaidia watu ambao hawajiwezi kama hao ambao Mheshimiwa Dkt. Kabati amesema.

**SPIKA:** Mheshimiwa Abbas Tarimba, swali la nyongeza.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Spika, ninaomba nimuulize Mheshimiwa Naibu ...

**SPIKA:** Uliza tu swali, huna haja ya kuomba tena nimeshakupa nafasi.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Spika, ninataka kujua kuna taarifa kwamba mashine za *PET Scans* ziko pale *Ocean Road*. Swali, je, zimeshaanza kufanya kazi na ni wataalam wa aina gani ambao tuko nao kwa minajili ya mashine hizo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli Mashine ya *PET CT-Scan* imeshafungwa na imeshaanza kazi. Kulikuwa tuna shida kidogo ya *software* fulani ambayo ilitakiwa ndani ya wiki mbili iwe imemalizwa ili huduma nyingine ziendelee, lakini imeshafungwa na imeanza kazi, lakini kuna *software* ambayo tunahitaji ifungwe pale ili uweze kufanya kwa *capacity* yake nzima. Imeanza kazi na ndiyo maana tumekuwa tukiwaambia mashine alizofunga Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, tuna uwezo hata wa ku-*detect cancer* inayokuja miaka mitano, miaka 10 ijayo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Felista Njau, swali la nyongeza.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Spika, wagonjwa wengi wa saratani wanajulikana na ugonjwa huo wakiwa wameshafika *stage* za mbali kabisa na hivyo kuleta athari ya uhai wao. Nini mkakati wa Serikali kuhakikisha wanatoa elimu ili watu wengi waweze kupima mapema kabla ya kuathirika? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, miaka mitatu iliyopita kwa kweli swali la msingi alilosema dada yangu hapa lilikuwa hivyo, lakini baada ya Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kusambaza teknolojia na miundombinu mpaka kule chini, sasa kutoka 90% ya wagonjwa waliokuwa wanakuja ikiwa *cancer* imefika mbali sasa wameshapunguzwa kwa 78%. Maana yake mpaka mwaka unaofuata baadaye utaona wamepungua kabisa, kwa sababu sasa teknolojia iko chini na wataalam wameshushwa chini na uwezeshaji umeenda. Kwa hiyo hilo limeweza kushughulikiwa kwa kina kama ambavyo ungetamani. Kwa hiyo ripoti ndiyo hiyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Angeline Mabula, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Spika, wagonjwa wa *cancer* wamekuwa wakiongezeka siku hadi siku.

Je, Serikali haioni ni muda muafaka sasa kuona namna bora ya kuweza kutoa ruzuku kwa wagonjwa hawa waweze kuwa wanapata matibabu, kwa sababu wengi hawana uwezo wa kuweza kujitibia wenyewe? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, moja ya Sera yetu ni kuwatibu hawa wagonjwa bure, lakini suala sio kutoa ruzuku. Kama ambavyo nimeshasema kwenye swali la Mheshimiwa Dkt. Kabati, kuna utaratibu huo wa kuwasaidia, lakini inawezekana zamani watu walikuwa wanakufa kwa *cancer,* lakini hawajulikani. Hata hivyo, kwa sababu ya uboreshaji wa huduma za afya, sasa watu wanajulikana mapema na watu wamekuwa *screened* mapema na kujulikana tatizo ni nini. Pia, tutaendelea kukabiliana kuendelea kutoa elimu ili kupunguza sababu ya watu kupata *cancer* badala ya kuongeza ruzuku.

**SPIKA:** Mheshimiwa Stella Manyanya, swali la nyongeza.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, kwa nini Madaktari Bingwa ambao wangeweza kusaidia masuala ya *cancer* na wale wanaoenda kwa ajili ya zile huduma za kupeleka vijijini hawalipwi posho zao kupitia Bima ya Afya, kwamba hawatambuliki katika Bima ya Afya? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, nimelisikia hapa, sitegemei Bima ya Afya isiweze kuwalipa Madaktari ambao wanasaidia wagonjwa wa *cancer*. Mheshimiwa Ritta Kabati tutasaidiana anionyeshe *specific* ni nini kimetokea na ninataka kumhakikishia tutalitatua leo na kwisha na halitojirudia.

**SPIKA:** Ni Mheshimiwa Stella Manyanya, siyo Mheshimiwa Ritta Kabati. Mheshimiwa Khadija Shaaban Taya, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake, kwa niaba yake ...

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Spika, mimi hapa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Husna, si una swali lingine tayari utauliza kwa niaba? Wewe umechelewa kufika, kwa hiyo ngoja nimpe Mheshimiwa Shally, wewe nitakupa swali la nyongeza. Mheshimiwa Shally Raymond.

Na. 63

**Utaratibu wa Kuwasaidia Matibabu Wagonjwa wa Saratani ya Ngozi**

**MHE. SHALLY J. RAYMOND K.n.y. MHE. KHADIJA S. TAYA** aliuliza:-

Je, Serikali imeweka utaratibu gani wa kuwasaidia matibabu ya ngozi watu wenye Ualbino kutokana na Ugonjwa wa Saratani ya Ngozi kuongezeka?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua changamoto wanazokabiliana nazo watu wenye ualbino. Serikali imechukua hatua kadhaa kusaidia matibabu na kinga ya saratani ya ngozi kwa watu wenye ualbino kwa kutekeleza yafuatayo:-

(i) Kuanzisha vituo maalum vya uchunguzi na matibabu ya saratani ya ngozi katika hospitali mbalimbali nchini ili kuhakikisha watu wenye ualbino wanapata huduma hizi kwa urahisi;

(ii) Kuimarisha upatikanaji na usambazaji wa vifaa kinga ikiwemo mafuta maalum ya kujikinga na jua ambayo yamejumuishwa kwenye bidhaa za afya zinazoagizwa na Bohari Kuu ya Dawa *(MSD)*;

(iii) Serikali imeandaa Mpango Kazi wa Taifa wa Haki na Ustawi kwa Watu Wenye Ualbino, unaolenga kuboresha hali ya maisha ya watu wenye ualbino kwa

kuimarisha huduma za afya, elimu na ulinzi dhidi ya saratani ya ngozi.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Shally Raymond, swali la nyongeza.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; ualbino unatokea kutokana na wazazi wa aina mbili kuwa zile *chromosomes* za aina fulani. Je, elimu inatolewa vipi ili hao watu wasiende tena kukutana au kuoana ili waongezeke kwa kasi?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa kuwa vifaa hivyo umevitaja eneo linalofahamika zaidi ni Hospitali ya *KCMC*. Je, inawezekana kutoa vifaa hivyo kwenye Hospitali za Rufaa na kushusha kwenye vituo vya afya hadi kwenye *dispensaries? (Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa namna ambavyo amekuwa akifanya kazi nzuri sana kwenye Wilaya zetu sisi Wabunge ambao tunatokea Mkoa wa Kilimanjaro, tunamshukuru sana dada yangu kwa jinsi ambavyo anawahudumia akinamama kwenye hili eneo lake.

Mheshimiwa Spika, swali lake la kwanza, kwamba kuhamasisha watu ambao wana uwezekano wa kupata mtoto *albino* wasioane hilo ni gumu kidogo, kwa sababu wanaanza kupendana hata kabla ya kuanza kupima mambo mengine. Kwa hiyo sasa wakati mwingine na hili nalo ukilichukua kama Serikali, inabidi tuwe makini sana kwenye suala zima la unyanyapaa na mambo mengine yanayofanana na hayo. Tunalichukua kulitafakari, lakini ni ngumu sana, namna ya kulitekeleza japo sababu hizo zinajulikana.  Tunafikiri sio suala la kuzungumza sana ili kuondoa unyanyapaa na kupunguza mambo mengine ya aina hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili, anasema *KCMC*. Kwanza nitumie fursa hii kuipongeza *KCMC* kwa sababu wao wamefika mbali wana kiwanda chao cha kuzalisha wenyewe hayo mafuta. Kwa hiyo, niwapongeze sana. Pia, niseme ndiyo maana tumeweka kwenye bidhaa zinazosambazwa na *MSD*, maana yake *MSD* inasambaza mpaka vituo vyetu vya afya, *dispensary* kuhakikisha tunapatikana.

Mheshimiwa Spika, kikubwa ni kuwaomba ma-*DMO* pamoja na Wafamasia wa Wilaya katika hizi bidhaa inawezekana wakati mwingine hazifiki huko chini sio kwamba hazisambazwi. Mara nyingi wanachoangalia *MSD* ni maombi kutoka Wilaya husika. Niwahamasishe ma-*DMO* wawatambue watu wenye Ualbino kwenye maeneo yao halafu sasa waweze kuweka hizo bidhaa kwenye bidhaa wanazoagiza, ili waweze kupata huduma hukohuko kwenye wilaya zao.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ester Bulaya, swali la nyongeza, huna, *okay*. Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, swali la nyongeza.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Spika, je, Serikali iko tayari kufanya mabadiliko ya mwongozo wa utoaji wa huduma za afya ili kuruhusu huduma za watu wenye ualbino na watu wenye ulemavu vifaa vyao viweze kupatikana kwenye ngazi ya wilaya na vituo vya afya? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza hilo ni swali zuri sana na halihitaji kubadilisha Sheria, liko *obvious* kulingana na uwezo wa kituo husika. Kwa hiyo, ninachosema kwa Waganga wetu wa Mikoa na Waganga wetu wa Wilaya, ni kwamba watazame matatizo hayo ya watu wenye ualbino pamoja na wenye ulemavu kulingana na uwezo wa kituo ihakikishe kwamba vifaa husika vinapatikana kwenye eneo husika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Halima Mdee, swali la nyongeza.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, mashine ya *PET Scan* ni muhimu sana katika kutambua namna ambavyo *cancer* imesambaa mwilini na kuweza kujua ni namna gani inaweza kutibiwa. Sasa ninataka nijue, ninafahamu mashine ipo lakini changamoto iliyopo ni kuanza kufanya kazi, ninaomba tupate taarifa sahihi kuhusiana na hilo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Halima Mdee kwa namna ambavyo sio suala hili tu na masuala mengi ya afya na kijamii amekuwa akiyafuatilia kwa karibu. Hata hivyo, nimwambie *PET Scan* kweli ipo, lakini unazungumzia *human resource* ambao wataziendesha, kweli sasa hivi tunao, lakini hawatoshi. Sasa hivi tunavyozungumza kupitia Dkt. Samia *Scholarship,* kuna watu zaidi ya nane wako nje wanasoma kwa ajili ya kurudi kutoa huduma zinazofanana na hizo. Pia, *software* ambayo nayo ilikuwa ni tatizo imeshafanyiwa kazi tunategemea baada ya muda itakuwa imefungwa vizuri na huduma hiyo itatolewa kwa 100% ambayo ilikuwa inatolewa kwa 80% ya *capacity* ya mashine yenyewe.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Cecil David Mwambe, Mbunge wa Ndanda, sasa aulize swali lake.

Na. 64

**Kutafsiri Upya Sheria ya *Intoxicating Liquors Act, 1968***

**MHE. CECIL D. MWAMBE** aliuliza:-

Je, lini Serikali itatafsiri upya *Liquor and Intoxication Act, 1968* ili kutoa fursa kwa Wakulima wa Korosho kupata kipato kwenye Gongo ya Mabibo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Jumanne Sagini majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Sheria ya *Intoxicating Liquors Act*, inaweka utaratibu wa kuwasimamia watengenezaji na wauzaji wa pombe za asili. Kwa mujibu wa Sheria hiyo, mtu yeyote anayekusudia kutengeneza au kuuza pombe ya asili anapaswa kuomba leseni kwa Mamlaka husika ya Serikali za Mitaa. Aidha, kwa mujibu wa Sheria hii Gongo sio miongoni mwa pombe za asili *(local liquor)* kama ilivyotafsiriwa katika kifungu cha 3 cha Sheria husika.

Mheshimiwa Spika, Pombe aina ya Gongo, Machozi ya Simba, Moshi au Umeme kama ilivyotafsiriwa na kifungu cha 2 cha Sheria ya Kudhibiti Utengenezaji wa Pombe za Asili, Sura 384 *(Traditional Liquor (Control of Distillation) Act)* inaweza kutengenezwa ikiwa mtengenezaji ana leseni iliyotolewa kwa mujibu wa kifungu cha 19 cha Sheria ya Kudhibiti Pombe za Asili Sura ya 384. Leseni hiyo hutolewa na Waziri mwenye dhamana ya viwanda. Aidha, ni kosa la jinai kuzalisha pombe ya asili ikiwemo Gongo bila leseni. Hivyo wakulima wa korosho wanayo nafasi ya kujiongezea kipato kupitia gongo ya mabibo ikiwa wataomba leseni ya kuzalisha pombe hiyo kutoka Wizara husika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Cecil Mwambe, swali la nyongeza.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, kwanza nishukuru kwa majibu mazuri kabisa ya Serikali kuhusiana na suala hili, kwa sababu limekaa hapa mbele yetu na utakuwa shahidi kwa muda mrefu sana tukilijadili na malengo ni kwamba kuongeza ile *value chain* ili wakulima wa korosho waweze kujipatia mapato. Sasa Serikali ipo tayari kutoa elimu kwa wakulima wa korosho kutokana na hii sheria? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali ipo tayari. Kupitia Wizara ya Viwanda na Biashara, mara kadhaa tumemsikia Waziri akitoa hapa ufafanuzi, *SIDO* wana Idara ya Elimu kwa ajili ya kutumia teknolojia inayoweza kuongeza thamani katika mazao mbalimbali yanayozalishwa na

wananchi wetu. Kwa hiyo, wakulima wa jimbo lako wanaweza wakatumia fursa hiyo ili kujiimarisha wakafanya kitu ambacho kinakubalika kwa mujibu wa Sheria. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Zaytun Seif Swai, Mbunge wa Viti Maalum swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Husna Sekiboko.

Na. 65

***TANAPA* Kutumia Fursa za Misitu kwenye Biashara ya *Carbon***

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO K.n.y. MHE. ZAYTUN S. SWAI** aliuliza:-

Je, lini *TANAPA* watatumia vizuri fursa za Misitu waliyonayo kunufaika na Biashara ya *Carbon* kama nchi nyingine zinavyonufaika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Dunstan Kitandula, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania *(TANAPA)* ikiwa ni miongoni mwa Taasisi za Serikali zenye maeneo ya misitu inatambua uwepo wa biashara hii na tayari imeanza kuchukua hatua ili kuhakikisha upatikanaji wa manufaa yanayotokana na biashara ya hewa ukaa. Katika kutekeleza azma hiyo, Menejimenti ya Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania iliwasiliana na Kituo cha Uratibu wa Biashara ya Hewa Ukaa cha Taifa kilichopo katika Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine ili kupatiwa Mwongozo wa Biashara ya Hewa Ukaa ulioandaliwa na Ofisi ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kufuatia mwongozo huo, Shirika limebainisha hifadhi zenye fursa ya biashara hii katika maeneo ya kaboni ya kwenye udongo, Kaboni ya kwenye miti na Kaboni ya

kwenye maji. Kwa sasa taratibu za kuandaa mikataba ya makubaliano baina ya *TANAPA* na makampuni yanayohusika na biashara ya hewa ukaa zinaendelea na baada ya mikataba hiyo kukamilika, *TANAPA* itaweza kunufaika na biashara ya hewa ukaa kama nchi nyingine zinavyonufaika na biashara hiyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Husna Sekiboko, swali la nyongeza.

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; je, ni lini Serikali itaanza utekelezaji wa mkakati madhubuti wa kutumia misitu iliyopo katika Mlima Meru Mkoani Arusha kwa ajili ya uwekezaji wa biashara hii?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; ni kwa namna gani mkakati huu wa Serikali utakwenda kunufaisha wananchi wa Mkoa wa Tanga katika Milima ya Usambara na Amani. Ninashukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, anaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, biashara hii ni biashara mpya ambayo inafanyika katika *level* ya Kimataifa, tunachofanya kama nchi kwa sasa ni kuhakikisha tunakuwa na umakini mkubwa katika kuweka sawa mambo yetu ndani ili mikataba hii tutakapoingia na makampuni haya ya Kimataifa isije ikawa ni tatizo kwetu kama nchi isipokuwa iweze kutunufaisha.

Mheshimiwa Spika, maeneo ya Mlima Meru ni eneo ambalo ni urithi wa Taifa, tusipokuwa makini katika mikataba yetu tunaweza kujikuta tumekabidhi haki ya kumiliki maeneo hayo kwa watu wachache na sisi mwisho wa siku tukashindwa kuyatumia kunufaika kwa njia nyingine. Kwa hiyo naomba Waheshimiwa Wabunge tuwe na subira wakati Serikali inachukulia jambo hili kwa umuhimu mkubwa ili mikataba hii isije kuwa janga iwe ni mikataba ya kuleta manufaa kwa Taifa letu.*(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Kimei swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Spika, ninafikiri hii subira tunayoambiwa tuvute tunapoteza fursa ya kupata mapato kutokana na chanzo hiki. Kuna nchi nyingi tayari zinafanya biashara hii, kwa nini watu wetu wasiende kujifunza tukapata fedha Vijiji vyetu kule Moshi - Vunjo vimekosa *cooperate social responsibility* kutokana na biashara hii. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, tuna utajiri wa maarifa katika nchi yetu na ndiyo maana tunasema subira yavuta kheri. Wataalam wetu wamekwisha kwenda kujifunza kwenye nchi nyingine tumeona makosa ambayo wenzetu wameyafanya na katika kujifunza huko ndiyo maana Tanzania imekuwa nchi ya kwanza katika Afrika kuwa na mwongozo thabiti wa kufanya biashara hii. Nimesema sasa hivi taasisi zetu zinaandaa mikataba itakayotuwezesha tusiingie kwenye matatizo.

Mheshimiwa Spika, naomba tuwe na subira ili tutoke vizuri kwenye jambo hili.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Masauni.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuongezea majibu kwa maswali ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni sahihi kwamba kwenye biashara ya *carbon* kuna fursa pana sana ambayo inaweza ikasaidia nchi yetu kuweza kupata fedha, lakini kusaidia pamoja na jitihada za kidunia kupambana na mabadiliko ya tabianchi, lakini kuna hatua kadhaa ambayo Serikali zimechukua katika kufanikisha hilo hasa tukitilia maanani...

Mheshimiwa Spika, nasema ni sahihi kwamba kwenye biashara ya *carbon* kuna fursa kubwa sana inayoweza kusaidia nchi yetu kupata fedha, lakini kupambana na changamoto ya mabadiliko ya tabianchi. Ni sahihi kwamba bado kama Taifa hatujatumia vya kutosha fursa hiyo, kwa hiyo katika kuchukua hatua Serikali imefanya yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, Bunge lililopita kama utakumbuka wakati tumepitisha mabadiliko ya Sheria ya Mazingira, kwa mara ya kwanza tuliweza kukitambua Kituo cha Kuratibu Biashara ya *Carbon* kilichopo Morogoro kisheria, lakini sasa tupo katika hatua za kukiimarisha kituo hicho kwa maana ya kuweza kuunda *board* na *management* ili kiweze kufanya majukumu yake vizuri.

Mheshimiwa Spika, hali kadhalika, hizi siku chache zilizopita tuliunda Kamati ya wataalam ya kushauri namna bora ya kuweza kufaidika na biashara hii lengo ni kuhakikisha kwamba uwekezaji katika maeneo yote muhimu ikiwemo miradi mikubwa ya kimkakati na maeneo ambayo bado yana fursa ya kuweza kufanyika biashara hii tunaweza kuitumia vizuri.

Mheshimiwa Spika, ninaungana na Mheshimiwa Naibu Waziri kuwaomba Waheshimiwa Wabunge wawe na subira wakati Serikali inajipanga vizuri kuhakikisha kwamba katika muda mchache unaokuja tuweze kunufaika na biashara hii katika maeneo yote yenye fursa katika eneo hili. Ninakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Tarimo, swali la nyongeza.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Swali la kwanza; kwa sababu Serikali ipo kwenye utaratibu wa kukamilisha hiyo sheria na miongozo; je, wapo tayari sasa kuhakikisha kwamba hayo manufaa yatakayopatikana yatashirikisha Halmashauri ambazo zimezunguka misitu hiyo kwa mfano Msitu wa Rau pale Moshi upo ndani ya Moshi ndiyo wanaoulinda, wapo tayari sasa kwamba hayo manufaa yatumike na Halmashauri pia. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, Serikali ipo tayari. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya. Mheshimiwa Rehema Migilla swali la nyongeza. Mheshimiwa Naibu Waziri, kuna Mheshimiwa Mbunge mwingine kasimama pale. Mheshimiwa Rehema Migilla swali la nyongeza.

**MHE. REHEMA J. MIGILLA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Serikali kusema kwamba wanasubiri mikataba tayari Wilaya ya Tanganyika wameshaanza kufanya biashara hii ya hewaukaa na sisi kama Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua tumekwenda hivi juzi kujifunza kuhusu uvunaji wa hewaukaa. Je, hawa Wilaya ya Tanganyika wanatumia mikataba gani ambayo haiwezekani kutumika kwenye Wilaya zingine? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali...

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, napenda....

**SPIKA:** Huyu ni Mheshimiwa Naibu Waziri, yule ni Mheshimiwa Waziri ama nimesema Naibu Waziri? Changamoto ni kwamba akiwa amesimama Mheshimiwa Waziri inabidi nimtambue Mheshimiwa Waziri, kwa hivyo ndiyo maana nimeita Mheshimiwa Waziri maana huyu ni Mheshimiwa Naibu Waziri huyu aliyesimama Mheshimiwa Waziri, ulikuwa na wewe unaongea?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ndiyo.

**SPIKA:** Aaah! Basi uniwie radhi, lakini nilimtambua Mheshimiwa Waziri kwa sababu nilimwona amesimama, haya Mheshimiwa Waziri majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali ya nyongeza ya Waheshimiwa Wabunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nilizungumza kwamba sheria ipo tayari, Bunge lililopita sheria imepitishwa, lakini hali kadhalika kanuni ilikuwepo kabla hata sheria haijatungwa ambayo imeeleza namna ambavyo Halmashauri zetu zinapata faida kiasi gani na Serikali inapata kiasi gani, ndiyo maana kama alivyozungumza Mheshimiwa Mbunge kule Wilaya ya Tanganyika wanapata mgao kulingana na kanuni hiyo iliyopo sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, changamoto kubwa iliyopo ni kwamba kama Serikali haturidhiki juu ya utaratibu mzima juu ya uendeshaji wa biashara hii, tunadhani kwamba katika biashara hii inaweza ikaendeshwa vizuri zaidi na Serikali ikapata tija zaidi. Vilevile tunaamini kwamba kuna fursa nyingine pana zaidi katika hii nchi haijatumika ipasavyo. Kwa hiyo mikakati ambayo tumechukua au hatua tulizochukua zinalenga katika kutatua changamoto ya masuala mengine ili kwa ujumla wake Serikali iweze kunufaika vizuri ziadi katika biashara hii. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi Mheshimiwa Hussein Nassor Amar Mheshimiwa Mbunge wa Nyang'hwale sasa aulize swali lake.

Na. 66

**Uhitaji wa Gari la Zimamoto – Nyang'hwale**

**MHE. HUSSEIN N. AMAR** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka gari la Zimamoto Wilaya ya Nyang'hwale?

**SPIKA:** Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Daniel Sillo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Jeshi la Zimamoto na Uokoaji inatekeleza Mradi wa Ununuzi wa Magari na Vifaa vya Kuzimia Moto na Uokoaji wenye thamani ya Dola za Marekani milioni 100 kutoka kampuni ya *NAFFCO FZCO* iliyopo Dubai. Mradi huo utawezesha kupatikana kwa vitendea kazi mbalimbali ikiwemo magari 150 ya kuzima moto na uokoaji yatakayosambazwa nchi nzima ikiwemo Wilaya ya Nyang'hwale.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali itaendelea kuliimarisha Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kwa kulipatia vitendea kazi ili liweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hussein Nassor Amar swali la nyongeza.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kuipongeza Serikali kwa kutupatia gari la Zimamoto Wilaya ya Nyang'hwale, lakini pia niwapongeze Jeshi la Zimamoto Wilaya ya Nyang'hwale wanafanya kazi kwa kujituma pamoja na kwamba wapo wachache naomba niwatambue tu wa kwanza kiongozi wa Sajini Abdalah Mwinyimvua, Konstabo Fadhili Kipilipili, Konstabo Bichi Philemoni wanafanya kazi kubwa sana kipindi hasa cha masika yanapotokea mafuriko.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; je, Serikali ipo tayari kutupatia gari kwa ajili ya Maafisa hawa waweze kufanya kazi ya kuzunguka na kutoa elimu kwenye taasisi mbalimbali?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; je, Serikali ipo tayari kusambaza au kutengeneza miundombinu kwa ajili ya maji ya dharura ya zimamoto katika Makao Makuu ya Wilaya ya Nyang'hwale?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Mbunge kwa pongezi alizotoa kwa Askari ambao wanafanya kazi nzuri sana katika Wilaya ya Nyang'hwale.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maswali mawili ya nyongeza, swali la kwanza, kwa sasa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limesambaza magari katika mikoa yote nchini, hatua inayofuata ni kusambaza magari kwenye wilaya zote ikiwepo Wilaya ya Nyang'hwale.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, tayari Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limeshafanya vikao vitatu na mamlaka za maji ili kuhakikisha kwamba wilaya zote za Mkoa wa Geita zinapata *fire hydrants* ikiwepo Wilaya ya Nyang'hwale.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali. Subiri Mheshimiwa Naibu Waziri naona kuna Mheshimiwa Mbunge alisimama huku, Mheshimiwa Oliver Semuguruka swali la nyongeza.

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Ngara hatuna gari la zimamoto ningependa kujua ni lini Serikali itatupatia gari la zimamoto na hili swali nimeuliza mara ya tatu katika Bunge lako Tukufu? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Oliver, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu kwenye jibu na msingi tayari Serikali imeshaagiza magari 150 kwa ajili ya kupatia Zimamoto Wilaya zote nchini, ikiwemo Wilaya ya Ngara. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Umesema ikiwemo Wilaya aah! ya Ngara, haya ahsante sana. Mheshimiwa Robert Maboto swali la nyongeza.

**MHE. ROBERT C. MABOTO:** Mheshimiwa Spika, je, ni lini Serikali italeta gari ya zimamoto katika Halmashauri ya Mji wa Bunda? Ninakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Robert Maboto, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali tayari imeshaagiza haya magari 150 kwa ajili ya Wilaya zote ikiwepo Wilaya ya Bunda pia. Ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaenda Wizara ya Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, Mheshimiwa Mbunge wa Muleba Kusini, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Omari Kigua.

Na. 67

**Matumizi ya Bidhaa na Huduma Zinazozalishwa Nchini**

**MHE. OMARI M. KIGUA K.n.y MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhamasisha watumiaji wa Tanzania kununua bidhaa na huduma zinazozalishwa hapa nchini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Exaud Kigahe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na jitihada za kutangaza bidhaa zinazozalishwa nchini kwa lengo la kuhamasisha matumizi ya bidhaa hizo kupitia mikakati mbalimbali

ya ukuzaji biashara ndani na nje ya nchi. Mikakati hiyo ni pamoja na:-

(i) Kuanzishwa kwa rajamu/chapa maalum ya bidhaa ya *Made in Tanzania* ambayo itatumika kwa lengo la kutambulisha na kutangaza bidhaa zinazozalishwa nchini katika masoko yetu ya ndani na pia yale ya Kimataifa;

(ii) Kuratibu maonesho ya bidhaa za Tanzania *(TIMEXPO)* na Maonesho ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (Sabasaba) yanayofanyika kila mwaka, ikiambatana na utekelezaji wa kampeni ya "*Nunua bidhaa za Tanzania, Jenga uchumi wa Tanzania*" ambapo wazalishaji, wasambazaji, wanunuzi pamoja na watoa huduma za usaidizi kutoka sekta za umma na binafsi hushiriki.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuhamasisha matumizi ya bidhaa zinazozalishwa nchini kupitia majukwaa mbalimbali ikiwa ni pamoja na niliyoyataja hapo juu. Aidha, niwaombe Waheshimiwa Wabunge kuwa mabalozi kwa kununua na kutumia bidhaa zinazozalishwa na wazalishaji wa ndani na kuhamasisha jamii ya Watanzania kuendelea kutumia bidhaa hizo. Ninakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Omari Kigua, swali la nyongeza.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na ninashukuru kwa majibu mazuri tu ambayo Serikali imetoa juu ya eneo hili. Ni ukweli usiyopingika kwamba kuhamasisha utumiaji bidhaa za ndani kwa kiasi kikubwa utaenda kupunguza matumizi ya *foreign currency* kwa maana fedha za kigeni, lakini hakuna jitihada kubwa zimefanyika kwa upande wa Serikali kuhakikisha kwamba bidhaa hizi za ndani wanapewa elimu ya kutosha ili ziwe na *quality* au thamani ya hali ya juu.

Mheshimiwa Spika, nini mpango mkakati sasa wa Serikali kuhakikisha kwamba bidhaa za ndani utayarishaji wake na

*packing* inakuwa ni nzuri ili wananchi waweze kununua kwa kiasi kikubwa sana? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Kigua kwa kazi kubwa anayoifanya kwa Sekta hii ya Biashara na umekuwa ukifuatilia mara nyingi sana kuona tunaendelea kuboresha biadhaa zetu ziwe na ubora, lakini pia ziwe shindani.

Mheshimiwa Spika, nikuhakikishie wewe pamoja na Bunge lako Tukufu kwamba Serikali tayari ina mipango mahsusi, moja ni kupitia maonesho yetu ambayo hasa ndiyo yanahamasisha ubora wa bidhaa zetu kwa sababu zinapoenda kwenye maonyesho yale kupitia kama ile niavyosema Sabasaba na *TIMEXPO* maana yake bidhaa zetu zinashindana na bidhaa za nje, tumeshaona tayari wananchi wananunua wapenda bidhaa zetu.

Mheshimiwa Spika, Serikali tayari imetenga fedha mahsusi kupitia Shirika letu la Kuendeleza Viwanda Vidogo Vidogo Nchini - *SIDO* pia kwa kushirikiana na *TBS* kwa maana ya Shirika la Viwango Tanzania ili kuwasaidia wazalishaji wa ndani wapate teknolojia nzuri lakini kuwawezesha ili wawe shindani kwa kuwawekea nembo ya ubora ili bidhaa zao ziweze kuwa shindani katika masoko ya ndani, lakini pia na masoko ya nje.

Mheshimiwa Spika, zaidi tayari tuna Biashara *App* ambayo yenyewe inasaidia kutangaza bidhaa zinazozalishwa ndani kwa Watanzania ili waweze kuona na kujua bidhaa moja inapatikana wapi kwa bei gani, lakini na ubora kama ulivyosema kwenye bidhaa hizo. Ninakushukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Janeth Mahawanga swali la nyongeza.

**MHE. JANETH E. MAHAWANGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Je, Serikali ina mpango gani wa kudhibiti uingizwaji wa

bidhaa kutoka nje ambao unaathiri ushindani wa wazalishaji wa bidhaa za ndani? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Nimpongeze sana dada yangu Mheshimiwa Janeth Mahawanga kwa swali zuri. Moja ya maeneo ambayo Serikali imeweka msisitizo na mkazo mkubwa ni kudhibiti bidhaa ambazo hazina ubora kutoka nje. Tayari tuna taasisi zetu ikiwemo hii taasisi ya kuhamasisha ushindani *(FCC - Fair Competition Comission)* Tume ya Ushindani ambayo yenyewe inaratibu na kuhakikisha bidhaa zinazotoka nje zinaingia zikiwa katika ubora unaotakiwa.

Mheshimiwa Spika, pili, kupitia Shirika letu la Viwango Tanzania - *TBS* nao pia tunathibiti kuhakiki ubora wa bidhaa zinazotoka nje ili kulinda bidhaa zetu za ndani. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inahakikisha tunafuatilia hasa mipakani na hasa hii mipaka ambayo ni vipenyo ambavyo si rasmi vinavyotumika kuingiza bidhaa hizi ambazo hazina ubora.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Kilimo Ndaisaba George Ruhoro, Mheshimiwa Mbunge wa Ngara swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate.

Na. 68

**Serikali Kununua Mahindi Jimbo la Ngara Kupitia NFRA**

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE K.n.y. MHE. NDAISABA G. RUHORO** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanza kununua mahindi ya wananchi wa Jimbo la Ngara kupitia *NFRA*?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa David Silinde majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, zoezi la ununuzi wa mahindi ikiwemo Jimbo la Ngara linatarajia kuanza mwezi Mei, 2025. Wakulima wanasisitizwa kuzingatia usafi wa mahindi na kukausha mahindi yao hadi kufikia kiwango cha unyevu wa 13.5% ili kuepuka usumbufu unaoweza kujitokeza endapo mahindi yao hayatakidhi ubora unaohitajika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Bilakwate, swali la nyongeza.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Ni lini Serikali itawatafutia soko la uhakika wakulima wa vanila, Wilayani Kyerwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, natambua jitihada kubwa inayofanywa na Mbunge kuhusu zao la vanila siku zote na moja ya jukumu kubwa ambalo sisi, kama Wizara, tunalo sasahivi ni kuhakikisdha kwamba, tunapata soko la uhakika kwa kutumia wadau mbalimbali. Kwa hiyo, tumeshaagiza na tumepeleka maelekezo katika balozi zote nje ya nchi kutafuta wadau kuja kuwekeza hapa nchini, kwa ajili ya zao la vanila. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwantumu Zodo, swali la nyongeza.

**MHE. MWANTUMU M. ZODO:** Mheshimiwa Spika, je, ni lini *NFRA* watakwenda kununua mahindi Handeni, ambao wamekuwa wakitoa ahadi kila mwaka kwa wananchi na hawaendi? Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ni kwamba, *NFRA* tayari wameshafanya tathmini katika maeneo yote ambayo tunapaswa kununua mahindi likiwemo eneo la Handeni. Kwa hiyo, katika mwaka huu wa fedha unaokuja tutatimiza kwa sababu, sasa hivi lengo letu kubwa ni kununua tani milioni moja za mahindi peke yake. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Abubakari Asenga, swali la nyongeza.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Spika, je, ni lini Serikali ama *NFRA* itaanza kununua sukari, ili kuwaepusha wakulima na bei ndogo ya kiwanda cha sukari inayolipa kwa wakulima wa muwa sasa hivi kwa kisingizio cha kwamba, sukari inabaki na hakuna soko? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, moja; mwaka jana Serikali kupitia Bunge lako Tukufu tulifanya mabadiliko ya Sheria ya Bodi ya Sukari kuruhusu *NFRA* kununua sukari na kuhifadhi, kwa ajili ya wakati wa dharura. Kwa hiyo, tumeshatimiza na tumeshaandaa kanuni, maana yake ni kuanzia sasa tutaanza kununua zinazotokana na viwanda vinavyozalisha sukari hapa nchini, hususan, katika Jimbo lako la Kilombero. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Erick Shigongo, swali la nyongeza.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniona. Wakati wa ziara ya Mheshimiwa Rais katika Jimbo la Sengerema nilizungumza na Mheshimiwa Naibu Waziri kuhusu kununua mahindi Buchosa na akampigia Mkurugenzi wa *NFRA,* Mr. Komba, wakasema wataanza kununua, lakini mpaka sasa hawajaanza kununua. Ningetaka kufahamu sasa, ni lini wataanza kununua mahindi Buchosa? Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ni kwamba, kama nilivyoeleza hapo awali, mwaka huu *NFRA* wamefanya

tathmini katika mikoa yote 26 na maeneo yote nchini ambayo tunapaswa kuweka vituo, kwa ajili ya kununua mahindi likiwemo Eneo la Buchosa analotokea Mheshimiwa Mbunge. Kwa hiyo, mwaka huu kutakuwa na utekelezaji halisia. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ester Bulaya, swali la nyongeza.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Watanzania na hasa Mikoa ya Njombe, Mbeya na maeneo mengine, wamehamasika sana na zao la parachichi na Mheshimiwa Naibu Waziri unajua uwekezaji wa zao la parachichi ni ghali sana. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha wanatafuta masoko ya uhakika, kwa ajili ya zao la parachichi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, anachokisema Mheshimiwa Mbunge ni kweli kabisa; moja ya zao ambalo lina gharama kubwa katika uwekezaji wake, lakini lina faida kubwa sana kwa nchi ni zao la parachichi na sisi kama, Wizara, tarehe 4 Aprili tulikuwa na kikao cha wadau wa parachichi, ili kuhakikisha kwamba, tunakuwa na bei ya uhakika kwa wakulima. Miongoni mwa maelekezo tuliyotoa ni kwamba, sasa hivi parachichi itauzwa kwa kuzingatia *grade*. Kwa hiyo, tutakuwa na *grade* ya kwanza na *grade* ya pili, hatutakuwa na zile *reject* kama ambavyo imekuwa ikisikika awali kuharibu bei. Vilevile, tumeingia mikataba na baadhi ya nchi, kwa ajili ya parachichi kutoka nchini. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi cha maswali kutoka upande wenu, lakini pia kupata majibu kutoka upande wa Serikali. Ninalo tangazo moja hapa la wageni na tutaanza na wageni kutoka Jukwaa la Spika.

Kwanza ni wageni wangu 25 ambao ni Wachungaji na Wajumbe wa Kanisa la Moravian, Jimbo la Kusini Magharibi, Dinali

ya Iyunga, Mkoa wa Mbeya, wakiongozwa na Mchungaji Godwell Simpito ambaye ni Mwenyekiti, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo Mchungaji Nuru Mwamahonje, huyu ni Katibu wa Wilaya ya Mbeya Mjini; Mchungaji Jeremiah Mdenyela, Mlezi wa Idara; Dkt. Nikubuka Malakasuka ambaye ni kiongozi wa Mipango na Maendeleo; na Ndugu Asulumenye Mwangaya ambaye ni kiongozi wa Uwakili. Sasa mnaweza kusimama pamoja na viongozi wetu hawa, karibuni sana Bungeni.*( Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ninao wageni wengine ambao ni viongozi kutoka Toyota Tanzania na hawa ni sehemu ya watu waliodhamini *Bunge Marathon*. Hawa ni Ndugu Kadiva Noah William ambaye ni Meneja Mkuu na Ndugu Jamali Chembela ambaye ni Meneja Mauzo, karibuni sana Bungeni, tunawashukuru sana kwa kuungana na sisi katika *Bunge Marathon* na hasa katika kuhakikisha hakuna mkimbiaji yeyote anayepanda bodaboda. *(Makofi)*

Wapo wageni wanne ambao ni wanariadha walioshiriki *Bunge Marathon* ambao ni Dkt. Satellite Entam, Ndugu Celine Gatuga, Ndugu Erine Kigomba na Ndugu Kombo Jumbe, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 43 wa Mheshimiwa Naibu Spika, ambao ni Maafisa Utumishi, Watendaji wa Kata, Waandishi Waendesha Ofisi na Maafisa Tarafa kutoka Ukonga, Segerea na Ilala, Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni mbalimbali wa Waheshimiwa Wabunge, wageni wenu hao ni wageni 70 wa Mheshimiwa Antony Peter Mavunde ambaye ni Waziri wa Madini. Hawa ni Chama cha Mabroka wa Madini Tanzania, CHAMMATA, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 70 wa Mheshimiwa Dkt. John Danielson Pallangyo ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Sylvia Francis Sigula ambaye anatoka Jijini Mwanza, anaitwa Bujiku, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni waliotembelea Bunge, kwa ajili ya mafunzo; wapo wanafunzi 75 na walimu watano kutoka Shule ya Msingi *Rainbow King'azi* iliyopo Kata ya Kwembe, Wilaya ya Ubungo, Jijini Dar es Salaam, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hao ndiyo wageni tuliokuwa nao, lakini tangazo la mwisho; nitumie fursa kuwashukuru sana ninyi nyote kwa ushiriki wenu kwenye *Bunge Marathon*. Mmefanya vizuri, mmeleta wawakilishi wengi sana kutoka kwenye majimbo yenu.

Kwa hiyo, ninawashukuru sana kwa ushiriki wenu na bila shaka muda si mrefu mtapata taarifa kuhusu maendeleo ya shule yetu na ujenzi tumefikia wapi. Ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote wa Tanzania walioshirikiana pamoja na sisi na wadau wote, ahsanteni sana.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, Mwenyekiti atakuja kunipokea. *(Makofi)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga )Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Katibu, tuendelee.

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:-**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano yetu. Leo tutaanza na Mheshimiwa Profesa Sospeter

Mwijarubi Muhongo, Mheshimiwa Deodatus Phillip Mwanyika na Mheshimiwa Profesa Shukran Elisha Manya wajiandae.

**MHE. PROF. SOSPETER M. MUHONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi ya kutoa mchango wangu kuhusu Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Nadhani tuipitishe hii bajeti kusudi Waziri Mkuu na timu yake waendelee na kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu utakuwa sehemu mbili, nitaongelea kwenye sera na kwenye ajira. Hii bajeti ni muhimu kwa sababu, inamalizia Dira yetu ya 2025 na inaanza utekelezaji wa Dira yetu ya Maendeleo ya mwaka 2050.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa sera nitaongelea Sera ya Maafa ambayo inahitaji marekebisho makubwa, lakini kabla sijaenda mbali naomba niendelee kutoa pole nyingi sana kwa ndugu zangu wa Musoma Vijijini ambao tumepatwa maafa ya nyumba 84 ambazo zimebomoka na wale jirani zetu wa Musoma Mjini vilevile walipata maafa makubwa. Poleni sana na tunashukuru Serikali imeanza kusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya Maafa inapaswa kuboreshwa kwa sababu zifuatazo. Sababu ya kwanza ni sera yetu tuliyonayo haiendani na hali halisi kwa sababu, maafa yamekuwa mengi na ni ya aina tofautitofauti. Kwa mfano, kwa sasa tuna maafa yanayotokana na madhara ya tabianchi, haya ndiyo kama ukame, moto, mafuriko, dhoruba huko ziwani na baharini na tuna maafa mengine yanayotokana na, tuseme hayakupangwa hayo ni *natural,* kama tetemeko la ardhi au milipuko ya volkano. Kuna maafa ambayo yanasababishwa na vyombo vya usafiri na usafirishaji kwa hiyo, ni lazima sera yetu tuipitie upya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu ya pili ni kwamba, Watanzania wameongezeka wamekuwa wengi kwa hiyo, maafa yakitokea hayaendani na hali halisi ya kukabiliana nayo. Mwaka 1961 wakati tunapata uhuru tulikuwa Watanzania karibu milioni 10, sasa hivi tukifika mwishoni mwaka huu tutakuwa tumevuka watu milioni 70 na dira ya maendeleo yetu ya Mwaka 2050

tukifika Mwaka 2050 tutakuwa Watanzania milioni 137. Kwa hiyo, inabidi tuboreshe sera hii ya maafa na uboreshaji wake cha muhimu ni lazima iendane na upatikanaji wa vyanzo vya fedha za kukabiliana na maafa haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa uzoefu wa dunia nyingine, maafa madogomadogo huwa yanashughulikiwa na *local government,* Serikali ya Mitaa. Kwa kule Marekani yanashughulikiwa na majimbo na hata kule China vilevile yanashughulikiwa na Serikali za Majimbo, kwa hapa kwetu ni kama vile halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maafa makubwa sana yanashughulikiwa na Serikali Kuu *(Central Government),* ndiyo maana kule Marekani unasikia *Federal Government* imeingilia kati na yanashughulikiwa na taasisi na *NGOs* za kimataifa, kama *Red Cross,* halafu ushirikiano wa nchi kwa nchi. Chanzo cha tatu cha fedha za maafa ni zinatokana na bima; sasa sisi hatuna bima nyingi ndiyo maana maafa yanashindwa kuhudumiwa. Kwa hiyo, tukishaipitisha hii bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, napendekeza sana tupitie sera yetu ya maafa iendane na vyanzo vya maafa halafu iendane na upatikanaji wa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha pili ninachokiongelea ni ajira. Ajira vilevile naiangalia, tunamaliza Bajeti ya Dira ya Mwaka 2025 tunataka ajira inayotupeleka kwenye Dira ya mwaka 2050. Sifa kuu za ajira ni mbili, elimu na cha pili ni mafunzo na nguzo ya ajira zote ni uchumi. Kwa hiyo, ajira zitategemea uchumi wa sekta binafsi, ajira zitategemea uchumi wa Serikali nzima na taasisi zake. Kwa mataifa yote duniani kote mwajiri mkubwa huwa ni sekta binafsi na siyo Serikali kwa hiyo, ajira ninazoziongelea mimi ni za miaka 25 inayokuja kufika mwaka 2050. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Tanzania, ajira tuzitoe kwanza sekta binafsi ndani ya Tanzania na sekta binafsi nje ya Tanzania. Pili, ajira tuzitoe kwenye Serikali ya Tanzania na zitoke kwenye Serikali za Mabara mengine, yaani huko Ulaya, Marekani, Asia na nchi za kiafrika. Watu wanaweza kuajiriwa na Serikali za huko na siyo lazima kutegemea Serikali ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuangalie mahitaji makubwa ya hizi ajira, wanataka sana mambo ya sayansi, teknolojia na *innovation*. Nina mifano hapa, mitatu minne, nitakayoitoa ambayo ajira zina soko kubwa huko kwenye dunia nyingine, upande wa afya, upande wa teknolojia, *artificial intelligence,* hiki siyo kitu kipya; mara ya kwanza, semina ya kwanza ya *artificial intelligence* ilifanyika Marekani mwaka 1956 siyo kitu kipya, halafu na mambo ya *manufacturing,* uzalishaji viwandani. Hayo maeneo manne yatawapatia vijana wetu kazi nje ya Tanzania kama tutakuwa tumejipanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, hii *artificial intelligence* ni kubwa mno, ni kufanya kazi kama mashine na wanataka *data scientists* na ndugu zangu *data centres* ndiyo zinachukua umeme kuzidi hata viwanda vikubwa. Sasa hivi duniani kwa siku tunatumia umeme karibu trilioni 70 za *watts* na asilimia mbili ya huo umeme inaenda kwenye *data centres.* Kwa hiyo, ndiyo maana watu wengi wanatakiwa huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, umuhimu wa kazi za nje ni vijana wetu kupata kazi huko nje halafu na pato la kitaifa kuongezeka, sasa hizi kazi za nje imekuwa ni biashara, ni bidhaa mpya duniani. Kwa mfano, mwaka 2023 bidhaa hii ya kazi za nje na watu kupeleka fedha nchini kwao ilikuwa na thamani ya dola bilioni 867 na mwaka jana hii bidhaa ilikuwa na thamani ya dola bilioni 905. Ndani ya mwaka mmoja tu zimeongezeka asilimia 4.6 za bidhaa hii. Hakuna biashara yoyote utakayoweza kuipata ndani ya mwaka mmoja inaongezeka kiasi hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana, ili kuona umuhimu wa sisi kutafuta hizo kazi za nje, waliopata pesa nyingi, kipato kingi, *remittances* na kurudisha kwao fedha, ya kwanza ilikuwa India. India ilirudisha fedha shilingi bilioni 129, inashinda kuuza pamba yetu nje. Mexico ilikuwa ya pili, shilingi bilioni 66, China ilikuwa ya tatu shilingi bilioni 50. Kwa hiyo, kwa upande wa Bara la Afrika tukichukua tano bora, ya kwanza ilikuwa Egypt kazi za nje hizo, ilitengeneza shilingi bilioni 30, ya pili ilikuwa Nigeria shilingi bilioni 21, ya tatu ilikuwa Morocco shilingi bilioni 12, nusu dakika, namalizia; kwanza sikuwepo, niongezee muda kidogo. Halafu

Morocco shilingi bilioni 12, Ghana shilingi bilioni 7.0 na Kenya shilingi bilioni 5.0. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimalizie kwa kusema kwamba, kama tunataka ajira zipo nje. Jambo la muhimu ni elimu na mafunzo na nimalizie hapa kwenye mafunzo, lazima tuwekeze kwenye sayansi, teknolojia na *innovation,* yaani kwa lugha nyingine hayo masomo yanaitwa *STEM (Science, Technology, Engineering and Mathematics)* kuanzia shule zetu za awali na shahada za vyuo vyetu vikuu ziwe shahada zinazotakiwa huko dunia nyingine. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Profesa Sospeter Mwijarubi Muhongo. Tunaendelea na Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika, Mheshimiwa Profesa Shukrani Elisha Manya ajiandae.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipatia nafasi ili nami niweze kuchangia kwenye Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu na timu yake kwa maandalizi mazuri na hotuba ndefu ya saa mbili ambayo tuliisikia hapa wiki iliyopita. Nipende kusema kwamba, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ameeleza kwa kirefu sana mafanikio makubwa ambayo nchi yetu imeyapata katika kipindi hiki ambacho Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Sita, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, amekuwa madarakani; ni mafanikio makubwa na sisi watu wa Njombe kama Mkoa hususan Jimbo la Njombe Mjini ni mashuhuda wa mafanikio makubwa hayo ya kuwasogezea wananchi wa Tanzania huduma mbalimbali za kuboresha miundombinu kama vile madarasa, usafiri wa reli, usafiri wa anga na mambo mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna kila sababu ya kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa haya yote ambayo yamefanyika. Sisi Njombe tunasema tumefanyiwa mengi katika kipindi hiki kifupi. Siwezi kuyataja yote, lakini nitataja yale ambayo ni machache

ambayo yalikuwa ni makubwa na kero kubwa ambazo zimefanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shida kubwa ya Mji wa Njombe ilikuwa ni maji; hatukuwahi kuwa na uwekezaji mkubwa kwenye sekta ya maji; lakini kwa mara ya kwanza ndani ya kipindi cha miaka minne tumekuwa na miradi mikubwa minne ya maji. Miradi mwili kati ya hiyo minne imekwishakamilika na imekwishaanza kuleta maji katika Mji wa Njombe. Vilevile, tunavyoongea kwa mara ya kwanza kwa wananchi wa Njombe ambao wana maji mengi ambayo Mungu amewajalia, bado walikuwa katika mgao wa maji safi na salama. Kwa mara ya kwanza kwenye kiangazi hiki wameanza kuonja matunda ya uwekezaji huo mkubwa wa miradi mikubwa ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna Mradi wa Ijunilo bilioni 3.9; tuna Mradi wa Livingstone bilioni 9.8; tuna Mradi wa Miji 28 ambao unakwenda kwa kasi, bilioni 41. Kwa hiyo, jumla tuna bilioni kama 67 katika maji peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu umeme, vijiji vyote sasa hivi vina umeme na sasa tunakwenda kwenye vitongoji. Hata hivyo, ni angalizo kidogo; Mji wa Njombe ni Mji na vijiji. Bado kuna maeneo ya mjini baadhi ya mitaa hakuna umeme na wananchi wa Njombe wananisikia. Maeneo kama ya Mpumbwe pamoja na Ihanga yote hayo bado yana tatizo la umeme. Nina hakika katika mpango unaokuja ingawaje si vitongoji na ni mitaa nayo yataangaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye afya yamefanyika mambo makubwa sana.  Ndani ya Mji wa Njombe tuna Hospitali kubwa ya Rufaa ya Mkoa ambayo Serikali imeingiza pale bilioni 27.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni hospitali ambayo imebadilisha maisha ya Wananjombe. Uwekezaji huu ni mkubwa, *capacity* ya vitanda ni 400, lakini vitanda vilivyopo mpaka sasa ni 238. Mama na Mtoto peke yake ni vitanda 100 na akinamama 12 wanaweza wakajifungua kwa wakati mmoja. Ni mambo makubwa ambayo yamefanyika katika kipindi hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako mengi, ipo pia kampasi ya Chuo Kikuu cha Dodoma ambayo inakuja Njombe yenye thamani ya bilioni 18. Tuna kiwanja cha ndege, tumesikia nacho kinakuja kwa kasi Njombe; kwa maana ya kwamba Serikali imeridhia na tunaanza kutafuta eneo. Tunawashukuru wenzetu wa Serikali ya mkoa ambao wanalishughulikia suala hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo letu ambalo ninapenda nitoe ushauri ni kwenye uwekezaji, ambalo ndilo eneo kubwa, na ninamshukuru Profesa Muhongo ameniwekea msingi wa hoja yangu. Shida yetu sisi ni kutengeneza ajira katika Mkoa au Mji wa Njombe. Njombe kwa kiasi kikubwa inategemea kilimo, kwa 99%. Kilimo chetu sisi ni kilimo cha mazao ya chakula na mazao ya biashara. Vilevile, tunategemea mazao ya misitu. Hapa ndipo ambapo kwa kweli tunamshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, amekuja Njombe takribani mara mbili na mara zote amejaribu sana kushughulikia changamoto zinazohusiana na uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kiasi kikubwa nipende kusema, sekta ya uwekezaji wa chai ndio uwekezaji mkubwa sana kwa Njombe kwa miaka mingi sana. Hata hivyo, kuanzia mwaka 2018 sekta hii imedorora. Tunafahamu jitihada za Serikali kutaka kufufua au kuhakikisha kwamba sekta ya chai inafanya kazi vizuri. Hata hivyo, ni ukweli usiopingika kwamba kuna kukosekana kwa umakini katika kutafuta wawekezaji. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais pamoja na Serikali yake, katika kipindi hiki imetengeneza mazingira mazuri sana ya wawekezaji wa ndani na wawekezaji wa nje; na tumeona mabadiliko mengi ya Sheria ya kutaka kuvutia uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninadhani inabidi tufanye tahadhari. Tuna wawekezaji wa aina nyingi wanaokuja kwa mwamvuli wa uwekezaji. Kwa kiasi kikubwa tusipokuwa makini, hasa na wawekezaji wanaokwenda vijijini na kujifanya wao wana uwezo mkubwa wa kusaidia kilimo, lakini mwisho wa siku tunachokiona ni kwamba wananchi ambao wanategemea kilimo, kwa maana ya kuwategemea wawekezaji ambao wanajenga au wananunua viwanda, na hasa ninaongelea viwanda vya chai, wamekuwa ndicho kiini cha kusogeza

umasikini na kupunguza au kuondoa ajira kwenye maeneo ya vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili lazima tulipige vita kama nchi. Kwa sababu tunahitaji ajira, tunahitaji kodi na tunahitaji mazao ya kupeleka nje ili tupate fedha za kigeni. Tunapompa mwekezaji kama wa chai; na nitakuwa *more specific,* kwa mfano tuna uwekezaji wa chai wa kampuni inaitwa *DL* ambayo imekuwa mwiba mkubwa sana kwa wananchi wa Njombe; pamoja na jitihada, ninachopenda kusema ni kwamba, Serikali iwe tayari kufanya maamuzi magumu kwa wawekezaji wa aina hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wawekezaji kwenye eneo la chai wanapewaa ardhi. Ardhi ni *productive asset.* Kama haitumiki kuzalisha ajira, kuzalisha bidhaa, haitumiki kuleta fedha za kigeni maana yake ni kwamba hatuitumii ardhi tuliyopewa na Mwenyezi Mungu kwa ajili ya kuondoa na kustawisha maisha ya wananchi wetu. Kwa hiyo, mwekezaji ambaye anahodhi ardhi na hafanyii kazi, niombe sana kwamba; Ofisi ya Waziri Mkuu inafanya uratibu, na Mheshimiwa Waziri Mkuu amekuja Njombe zaidi ya mara moja; tuwe na mkakati wa Kufanya maamuzi magumu, ikiwezekana kuichukua hiyo ardhi. Sisi ni wananchi wa Tanzania na Mwenyezi Mungu ametupatia ardhi, ni lazima itumike kwa watu ambao wako tayari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo lingine ambalo liko kwenye misitu, nako ni suala kubwa la ajira. Ninapenda kusema, tuna kampuni kubwa pale ya Kibena *(TANWAT)* huo ndio mfano halisi wa kampuni ya uwekezaji ambazo tunataka uje kwenye maeneo kama ya Njombe na maeneo mengine ya Tanzania. Ni kampuni ambayo inazalisha ajira, inafanya *plantation* za mazao mbalimbali na ikipewa ardhi inaitumia. Vilevile, kwa siku za hivi karibuni, tumeanza kuona kampuni nyingine nyingi ambazo zinatoka pande za Asia zikija kwa jina la kutaka kuwekeza kwenye upande wa sekta za misitu. Uhalisia ni kwamba kampuni hizi zinakuja kufilisi nchi, kwa maana ya wananchi wa maeneo yanayozunguka. Hawa kazi yao ni kupata mazao ya mbao na kuyasafirisha yakiwa ghafi au *semi-processed.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hiyo *process* nchi inapoteza ajira, nchi inarudi kwenye umasikini, kwa maana ya wananchi waliopo kwenye yale maeneo badala ya kupanda miti kwa wingi wanaendelea kufyeka miti  na kuzipelekea kampuni hizo za Kichina, ambazo kwa kweli tunasema ni uwekezaji ambao hauna tija kwa sababu hawana jukumu la kuzalisha miti, kupanda miti, wao ni kupokea mazao ya miti ambayo hawajui yanatokea wapi, wanawalipa wananchi fedha ndogo kwa sababu wananchi wetu wana shida na hizo fedha. Sasa, Serikali ina jukumu la kuhakikisha kwamba inawalinda wananchi wake na kuhakikisha wawekezaji kama hawa hawapewi vibali vya kuja kukata miti hovyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niishukuru Serikali kwamba, jambo hili tumeliongea hapa na wameanza kuchukua hatua. Tunafahamu wana kitu wanakiita Mpango Mkakati wa Mwaka 2021 mpaka 2030 wa kuangalia namna gani tunaongeza thamani kwenye mazao ya misitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mpango huo bado kuna *GN* ya 2023 *(GN. 211)* ambayo bado inaruhusu au inaratibu usafirishaji wa malighafi za misitu kwenda nje. Ndani ya *GN* hiyo tuna mategemeo na tumepiga kelele sana hapa, tunaitaka Serikali kwa kweli ihakikishe kwamba inatumia GN hiyo kuzuia kutoa vibali kwa wawekezaji wa aina hii ambayo nimeitaja, ambao mpaka muda huu wanafanya na wamehalalishwa na Wizara yetu ya Maliasili kuendelea kukata miti na kuwafanya wananchi wasiweze kufaidi matunda ya miti hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni mategemeo yangu; tuliambiwa hapa kuwa vibali hivyo wamepewa kwa mara ya mwisho. Hata hivyo, mwaka juzi tuliambiwa hivyo hivyo kuwa wamepewa kwa mara ya mwisho. Ni matumaini ya watu wa Njombe kwamba kama hakutakuwa na *improvement* au kuwataka waongeze thamani na ajira ndani ya nchi ni bora tuhakikishe vibali hivyo havitolewi tena kwa kwa wawekezaji wanaotoka maeneo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, niongelee kwa kifupi kuhusu Liganga na Mchuchuma. Sisi tunaishukuru sana

Serikali, kwa mara ya kwanza tumepewa taarifa hapa ndani ya Bunge lako kwamba sasa nchi yetu imepiga hatua nyingine katika kuhakikisha kuwa uwekezaji kwenye Liganga na Mchuchuma unakwenda kwenye hatua nyingine. Tunaishukuru sana Serikali na tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa juhudi zake binafsi za kuhakikisha anafufua uwekezaji huo na sasa tunangojea majadiliano ya mwisho ambayo tunasikia yanafanyika wiki ijayo ili tuweze kupata uwekezaji mkubwa wa Liganga na Mchuchuma katika Mkoa wa Njombe. Ninakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika. Nilimtaja Mheshimiwa Profesa Shukrani Elisha Manya, Mheshimiwa Constantine John Kanyasu ajiandae.

**MHE. PROF. SHUKRANI E. MANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu ambayo inaomba kuidhinishiwa bilioni 595.2 kwa shughuli za Ofisi ya Waziri Mkuu, lakini pia bilioni 186.8 kama Mfuko wa Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hotuba ya Waziri Mkuu imerejea utekelezaji wa shughuli za Serikali kwa kuzingatia utekelezaji wa dira ya mwaka 2025 inayoisha na pia ndio mwanzo wa utekelezaji wa dira nyingine ya miaka mingine 25. Ni kweli kwamba kupitia hotuba hii ya Waziri Mkuu Serikali imeonesha kwamba inaweza kusimamia kwa mambo ambayo imeyapanga na tunaona mafanikio makubwa sana kupitia utekelezaji wa dira inayokwisha. Ni katika msingi huo tunampongeza sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu mwenyewe kwa usimamizi mzuri, pamoja na Mawaziri wote ambao chini yao ndio wamekuwa wakisimamia utekelezaji wa shughuli za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya miradi ambayo imeonesha kwamba Serikali inaweza ikasimamia vema malengo yake na moja ya miradi ambayo Watanzania wengi bila kujali jinsia zao, itikadi zao za kisiasa au kidini wamefurahia na wakaona kwamba inakata kiu yao wakati huu kwa wale ambao mradi huu

umewafikia na kwamba ikajenga kiu zaidi kwa wale ambao mradi huu haujawafikia, ni Mradi wa *SGR*. Wale ambao tumefanikiwa kusafiri baina ya Dar es Salaam, Morogoro na Dodoma kupitia SGR, tunaweza tukawa ni mashuhuda kwa jinsi ambavyo treni yetu imeweza kurahisisha usafiri kwa kuchukua abiria wengi kwa wakati mmoja. Kwa msingi huo kuondoa foleni barabarani ambayo wakati mmoja treni ikisafiri unahitaji mabasi 20 kufanya safari hiyo hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tumeanza vizuri sana katika namna ambavyo SGR inaendeshwa. Mambo yafuatayo ninadhani ni ya msingi sana yakaendelea kusimamiwa vema. Jambo la kwanza ni ukataji tiketi kwa njia ya kidigitali. Tusingetamani kurudi nyuma kama ilivyokuwa kwa mwendokasi. Mwendokasi Dar es Salaam walianza kukatisha tiketi kwa kidigitali, lakini baada ya muda wakarejea nyuma na kuanza kukatisha kwa mkono. Tungetamani kwa jinsi ambavyo tumeanza vizuri na *SGR* mfumo huu wa ukataji tiketi kwa kidigitali uweze kuendelea kwa sababu unaona kabisa kwamba fedha inaingia moja kwa moja katika Mfuko Mkuu wa Mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa jinsi hiyo wataalam wa mifumo ya mtandao tunaomba wawe *alert,* wakae chonjo muda wote ili uendelee kufanya kazi kwa ufanisi siku zote. Tusije tukawa na *cyber security attack* ambayo inaweza ikaturudisha nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *SGR* ni treni ya umeme na kwa jinsi ambavyo Serikali imeanzisha mkoa wa *SGR* katika huduma ya nishati, basi wataalam wetu hawa wahakikishe sasa kwamba, katika huduma za *SGR* kusiwe na kile ambacho wakati fulani kilitokea cha kukatikakatika kwa umeme na hatimaye treni yetu ikasimama ghafla maporini mahali fulani. Kwa jinsi hiyo, iwapo wataendelea kudumisha huduma bora za kutoa huduma ya nishati katika *SGR* maana yake ni kwamba tutakuwa na huduma bora na huduma shindani ndani ya nchi yetu na kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu usalama wa *SGR;* m. Mwanzoni tulipokuwa tunaanza tulishuhudia Watanzania wachache ambao walikuwa wanatamani kuhujumu

miundombinu ya *SGR*. Hili jambo ni la msingi, uongozi uendelee kusimamia vizuri usalama ili kusiwe tena na watu ambao wanaweza wakahujumu miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na yote hayo, ninaomba niongelee kuhusu eneo la maegesho ya magari katika vituo vya Dodoma na Dar es Salaam. Pamoja na huduma nzuri inayotolewa, bado tunaona kwamba Dodoma kuna eneo dogo sana la maegesho ya magari; na si kwa sababu hakuna eneo la kutosha. Haya ni mambo ambayo tunadhani kwamba yanaweza yakaboresha ili kuondoa msongamano watu wanapokuwa wanashuka na hatimaye kuendelea kufurahia huduma za *SGR*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu Serikali imeonesha inaweza kusimamia vema, basi vile vipande ambavyo vimebaki vya kuelekea Tabora, Mwanza pamoja na Kigoma, basi Serikali katika hatua inayofuata ya utekelezaji wa bajeti ifanye lile linalowezekana ili vipande hivi navyo viweze kukamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nitaliongelea ni kuhusu ushindani wa kibiashara unaoendelea duniani kati ya mataifa makubwa yenye uchumi mkubwa. Sisi kama Taifa ambalo bado linaendelea kupiga hatua, hatuwezi tukakaa na tukatazama bila kutafuta nafasi yetu katika mtanzuko huu unaoendelea. Tumeshuhudia mataifa makubwa mawili ambayo kila kunapokucha mwingine anaongeza kodi juu ya vile vinavyoingia nchini kwake na mwingine pia anaongeza. Jambo hili linaweza likaathiri mataifa ambayo yanaendelea na sisi hatuwezi tukakaa kimya. Hivyo, ni jukumu la Serikali kila wakati kuangalia mwenendo wa biashara unavyoendelea katika mataifa haya ili sisi tuone kwamba tunajiweka mahali gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo ambalo ni la msingi katika hili ni kwamba, kama Taifa litajitosheleza kwenye chakula kwa maana ya kwamba tukawa na usalama wa chakula ndani ya nchi, basi Taifa ambalo limeshiba linaweza likawa linaendelea na mienendo katika mataifa mengine, lakini tukiwa tuna hakika ya kwamba, sisi tuna akiba ya kutosha ya chakula ndani ya nchi na

pia tuna ziada ambayo pia tunaweza tukauza nje ya mipaka yetu na hasa katika Soko la Afrika Mashariki na *SADC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mwingine tunadhani kwamba lazima tuuze nje mbali, lakini yawezekana kabisa kwamba ndani ya *SADC* pamoja na Afrika Mashariki bado kuna soko linalohitajika kwa ajili ya kuuza chakula. Kwa jinsi hiyo, Wizara ya Kilimo iendelee kukifanya kilimo kiweze kuwa cha kuvutia hasa kwa vijana wa Taifa hili ili kuongeza tija, ajira lakini pia wakati huohuo kuwaondoa katika mambo ambayo yanawapotezea muda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaamini kilimo kikiwa cha kuvutia hakuna sababu ya vijana wetu kwenda kufanya *betting*. Wanapotelea huko kwenye *betting* wakidhani kwamba wanatengeneza faida kumbe kama kilimo kingekuwa cha kuvutia kikatengeneza faida hakuna sababu ya kupoteza fedha katika *betting*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho, Serikali isimamie sana uwiano wa kibiashara ili kwamba tuzalishe sana mashambani, migodini, viwandani, katika misitu, uvuvi pamoja na ufugaji; ili kwamba tukifanya uwiano wetu wa kibiashara ukawa mzuri ndani ya nchi lakini katika jumuiya inayotuzunguka. Kile nilichokiongelea cha kwamba kuna ushindani wa kibiashara unaoanza kutokea baina ya mataifa makubwa ya kiuchumi hakutaweza kutuathiri kwa kiasi kikubwa na hivyo Serikali iweze kukaa chonjo muda wote ikiendelea kufanya tathmini ya jinsi ambavyo hatua zinazochukuliwa nje yetu haziwezi zikatuathiri hapa ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kusema hivyo ninakushukuru na ahsante sana kwa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Profesa Shukrani Elisha Manya. Nilimtaja Mheshimiwa Constantine John Kanyasu, Mheshimiwa Stella Ikupa Alex na Mheshimiwa Riziki Said Lulida ajiandae. Anayefuata Mheshimiwa Stella Ikupa Alex.

**MHE. STELLA I. ALEX:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa fursa ya kuweza kuchangia na ninaomba niunge mkono hoja iliyopo mezani. Awali ya yote nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa ajili ya upendeleo wa uzima na afya njema. Ni upendeleo kwa sababu wenzetu wengi walitamani kuiona siku ya leo lakini hawajaweza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitumie nafasi hii kumshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa uongozi wake imara na shupavu, uongozi ambao umepelekea leo hii tuwe na matokeo makubwa lakini tuendelee kujivunia kama Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu imeeleza mambo mengi ninaomba nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu na wasaidizi wake wote ndani ya Wizara kwa kazi kubwa ambayo wameendelea kuifanya. Serikali hii ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imefanya mambo makubwa sana ambayo kwa kweli kama Taifa tunajivunia: ujenzi wa miradi ya kimkakati; uhimilivu wa Deni la Taifa; mfumuko wa bei kuwa kwenye wigo ambao umewekwa; utoshelevu wa chakula nchini; amani na utulivu ambayo bado ipo; na uwekezaji katika Bandari yetu ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo haya yamewezekana ili hali duniani kukiwa kuna misukosuko mikubwa. Kwa hiyo, ndiyo maana tunaendelea kumpongeza na kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwamba uongozi wake ni imara, lakini pia uongozi wake ni shupavu sana japokuwa duniani kuna mambo yanaendelea wenzetu wanaporomoka, lakini sisi Tanzania tunaendelea kwenda viwango vya juu na kuwa kwenye ramani ya dunia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunavyofahamu uwekezaji wa bandari ulileta kelele nyingi sana na nikiwa kama Mbunge, Wabunge wa Dar es Salaam tuliungana kutoa elimu kwa Watanzania kwamba nini kinaenda kufanyika. Hakika tumeona kupitia taarifa ambazo zimeendelea kutolewa lakini kupitia uhalisia ambao tunaenda kuuona kama Wabunge

tumetembelea mara kadhaa pale bandarini hakika mambo ni makubwa sana. Mheshimiwa Rais ni kiongozi ambaye hayumbi hatikisiki yuko imara na uimara wake tunauona umekuwa ukitoa matokeo makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakika penye ukweli uongo umeendelea kujitenga na mwaka huu ninaamini kabisa Watanzania wameendelea kuona na wataona na watafanya maamuzi sahihi kwamba ni kiongozi gani ambaye anafaa kuendelea kuiongoza Taifa letu, kwa sababu upotoshaji umekuwa ni mwingi na ni kwa sababu wenzetu wamekosa hoja. Hoja zote Mheshimiwa Rais amezikamilisha. Kwa hiyo, hawana cha kufanya, wanachokifanya ni kuendelea kupotosha kila iitwapo leo. Ninaamini kabisa niendelee kurudia kwamba Watanzania wana macho wanaona na watafanya maamuzi yaliyo sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pia niishukuru sana Serikali kwa huduma kwa watu wenye ulemavu. Tunaona kabisa kwamba Serikali imejipanga na ina mipango mingi kwa habari ya kundi hili la watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nizungumzie Mfuko wa Taifa wa Watu Wenye Ulemavu. Mfuko huu ulianzishwa kwa Sheria Na.9 ya Mwaka 2010 ya Watu Wenye Ulemavu, kifungu cha 57(1) – (3), pale inaeleza ni kwa jinsi gani Mfuko unaanzishwa, malengo ya Mfuko huu, lakini pIa vyanzo vya fedha vya Mfuko huu wa Watu Wenye Ulemavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya malengo ya Mfuko huu yalikuwa ni kutoa ruzuku kwa Vyama vya Watu Wenye Ulemavu. Vilevile, kuendelea kufanya tafiti za masuala ya watu wenye ulemavu pamoja na kutoa huduma za utengamao na vifaa saidizi kwa watu wenye ulemavu. Fedha ambayo imeelezwa katika sheria hii chanzo kikubwa ni ile fedha ambayo inapitishwa na Bunge lako Tukufu, lakini pia fedha ambayo inapatikana kutoka kwa wadau mbalimbali na mambo mengine yako kwenye ile sheria ambayo yanajieleza vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu kwa Serikali, Serikali ina nia njema ya kuunganisha mifuko ya uwezeshaji wananchi kiuchumi, lakini kwa kadri ambayo nimeeleza hapa na kwa jinsi ambavyo sheria inaeleza Mfuko huu malengo yake makubwa si uwezeshaji kiuchumi kwa watu wenye ulemavu ila ni kutoa huduma kwa watu wenye ulemavu. Kama inavyofahamika ni kwamba kundi la watu wenye ulemavu bado lina uhitaji mkubwa hivyo niiombe Serikali Mfuko huu usiunganishwe na Mifuko mingine ya uwezeshaji wananchi kiuchumi kwa sababu malengo yake hayakuwa hayo ya uwezeshaji kiuchumi malengo yake ni kama ambavyo yanaelezwa kwenye sheria na kama ambavyo nimeyataja kwa uchache. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge lako Tukufu pia lilifanyia marekebisho Sheria ya Vyama vya Siasa. Niendelee kuiomba Serikali katika marekebisho yale kulikuwa na mkazo wa ujumuishi wa haya makundi maalum wakiwemo wanawake na watu wenye ulemavu, Serikali ifanye ufuatiliaji wa Sheria hii na hasa ikizingatiwa kwamba mwaka huu ni mwaka wa uchaguzi. Ni kwa jinsi gani vyama vitakuwa vimetekeleza Sheria hii kwa kuweka ujumuishi wa makundi maalum na hasa kundi la watu wenye ulemavu. Tunatamani kuona watu wenye ulemavu wakishika nafasi mbalimbali za uongozi kwenye vyama vya siasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba vyama hivi viweze kuona mfano mzuri ambao umewekwa na Chama Cha Mapinduzi wa kutenga nafasi maalum za watu wenye ulemavu kwenye nafasi hizi za Ubunge na kwenye *level* ya Madiwani. Vyama vione ni kwa jinsi gani kuanzia ngazi za Udiwani Viti Maalum pamoja na Kata kuweka nafasi zile za upendeleo kwa kundi la watu wenye ulemavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee pia kuishauri na kuiomba Serikali kipindi hiki ni kipindi cha uchaguzi iweze kuona ni kwa jinsi gani itaweka mbele matumizi ya lugha ya alama. Wenzetu viziwi ni wapigakura wazuri, lakini wanashindwa kuhudhuria hata kwenda kwenye mikutano kusikiliza sera za Wabunge, kusikiliza sera za madiwani kwa sababu kunakuwa hakuna ukalimani. Sasa tuweze kufikiria kwamba mtu anawezaji

kupiga kura ambayo hajasikia sera zake. Hivyo niiombe Serikali iweke mkazo huu na ielekeze kwamba kuwe kuna matumizi ya lugha ya alama kipindi hiki cha uchaguzi, lakini wakati wote ili tuweze kuwa sambamba na wenzetu viziwi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nimekuwa nikiliomba kila mara Serikali iweze kuona ni kwa jinsi gani inaendelea kutenga fedha za ununuzi wa mafuta ya watu wenye ualbino na kuweza kuyasambaza na kuwafikia wahusika. Sambamba na hilo, tukiwa tunasubiri ule Mfumo mzuri wa Bima ya Afya kwa Wote, Serikali iweze kuona ni kwa jinsi gani inaweka uratibu mzuri na unaotekelezeka wa matibabu kwa watu wenye ulemavu wasiokuwa na uwezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya haya, ninaomba kushukuru na niunge mkono hoja tena. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Stella Ikupa Alex. Nilimtaja Mheshimiwa Riziki Said Lulida, Mheshimiwa Robert Chacha Maboto, ajiandae.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kunichagua kuchangia katika hii hoja ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema aliyetujalia sote tuwe hapa tukiwa na afya njema. Nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan; Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Makamu wa Rais; na Mawaziri wote ambao Mwenyezi Mungu amewapa nafasi hii ya kuweza kukaa na kusimamia mambo mbalimbali ya kiutendaji na kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninazidi kumtanguliza Mwenyezi Mungu na kuitanguliza nchi yangu ambayo iko katika amani na utulivu. Mheshimiwa Rais amesimamia amani na utulivu, bila amani na utulivu hakuna biashara, hakuna kilimo, hakuna

uchimbaji wa madini. Unaweza ukawa na rasilimali, lakini nchi yako kama haina amani, utulivu na utu ndani yake hakuna kazi. Katika kipindi alichopewa Mheshimiwa Rais ameweza kusimamia vitu hivyo vyote. Mwenyezi Mungu amlinde na amwezeshe na kumwongezea ili anakokwenda Mwenyezi Mungu azidi kumwongezea afya njema. Hii siyo amri yake ni kadari ya Mwenyezi Mungu aliyemwezesha kumpa utu na kazi inaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatoka katika Kamati ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii na nitazungumzia suala la watu wenye ulemavu. Kutokana na *statistics* ya mwaka 2023 tuna walemavu milioni 10.7 hili ni kundi kubwa sana na hili kundi linakwenda katika mambo mengi iwe maendeleo ya kilimo, uchumi mpaka siasa wao wanatakiwa wawemo katika maeneo hayo. Nitazungumzia fedha ambazo zilitengwa kwa ajili ya watu wenye ulemavu, nilisikia mwenzangu Mheshimiwa Ikupa pale hizi fedha wamepewa hizi walemavu ziwasaidie katika vyama vya walemavu kuwasaidia kununua vifaa tiba na vifaa saidizi. Zile fedha hazikuletwa kwa ajili ya *economic recovery*, hapana! Zile 4:4:2 msichanganye na hizi pesa kwa nini? Hamjajua maumivu na machungu wanayopitia watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nenda *Ocean Road* walemavu wana kansa za ngozi. Mafuta yanayonunuliwa haya ndiyo yanakwenda kusaidia haya makundi maalum. Leo unapoitoa ile hela unaipeleka sehemu nyingine wale watasaidiwa na nani? Je, waendelee kuteseka na ngozi wakati hela zilikuwepo? Tunazungumza leo huu mwezi Aprili, hela imetengwa toka mwezi Julai mpaka leo haijatoka hata senti tano. Ninaamini sana Waziri yupo vizuri, Katibu Mkuu yupo vizuri, asimame na watendaji wake. Tunazihitaji hizi bilioni zirudi zikanunue dawa tuokoe maisha ya watu wenye ulemavu ambao wanayahitaji haya mafuta na baadhi ya vifaa saidizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana mimi mwenyewe unaniona ninahangaika kutafuta kila mahali kugawa *wheelchair* kila mahali, kwa nini? Hawa watu wanahitaji kuokolewa. Chukueni mfano akinamama anabeba mtoto mwenye matatizo, mtoto

huyo anambeba mpaka mtoto ana miaka 20 yupo mgongoni, lakini ukimpa *wheelchair* umemwokoa mwanamke, umeokoa mazingira magumu anayopambana nayo mwanamke anayetafuta chakula anatafuta biashara, lakini hawezi ana mtoto mlemavu mgongoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawaomba kwa uchungu niliokuwa nao tuwe wote humu ndani tuuangalie huu uchungu hizi pesa zirudi na siyo zirudi watuambie hapa baada ya hotuba hii ya Waziri Mkuu, lini watazirudisha hizi hela zikafanye kazi? Tayari hela zilishatengwa hela za vijana. Zilitengwa hela za vijana shilingi bilioni 1.9 kwa ajili ya mafunzo yao na maendeleo yao. Mpaka leo tunazungumza hata senti tano. Ninazungumza kama Makamu Mwenyekiti wa Kamati, hazijaingia. Leo kijana anahitaji kujitegemea, watu wanamaliza vyuoni hawana ajira hela hizi ndiyo wanaweza kusaidiana kwa mafunzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumetembelea Tengeru - Arusha, vijana ni ma-*graduate* wanalima mboga, lakini je, kama hawana pesa yao ya ruzuku tunafanya nini? Tusitumie nguvu na mabavu kuwanyang'anya hawa vijana hela zao, tunaomba hizi pesa ziende kwa vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilishukuru sana Bunge lako Tukufu likiongozwa na Mheshimiwa Spika amelifanya Bunge limekuwa la utulivu sana na Mheshimiwa Waziri Mkuu. Tupo hapa utulivu huu na amani hii inateremka mpaka chini na ni imani yangu kuwa katika uchaguzi tunaokwenda nao na tulivyofikia hapa Mungu atatufikisha katika utulivu na amani hakuna kumwaga damu. Dunia yote inaiangalia Tanzania kwa mifumo na mazingira mazuri tuliyoyaweka kwa ajili ya utulivu na Mwenyezi Mungu atasimama na sisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe shukurani sana kwa Mheshimiwa Rais, Waziri wa Kilimo, kwa mara ya kwanza mazao ya kilimo hasa korosho, ufuta na mbaazi zimeruka kwa bei ambayo wananchi sasa hivi kila unayemuuliza yupo mashambani wanalima. Korosho ya kwanza *grade one* imeuzwa kwa shilingi 4,000 kutoka shilingi 1200; namba mbili, imeuzwa kwa shilingi 3,800;

namba tatu shilingi 3,500, haya ni mabadiliko makubwa. Ufuta umeuzwa mpaka shilingi 4,000, mbaazi ambayo ilikuwa inauzwa shilingi 100 sasa hivi mbaazi inakwenda mpaka shilingi 2,500 hatuna cha kusema zaidi ya kumshukuru Mwenyezi Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoomba niyashukuru mashirika mbalimbali ambayo yameonesha upendo wa kufanya *value addition* kwa vijana. Mamlaka ya Korosho wanagawa au wanasaidia vijana mashine za kubangua korosho. Hii maana yake itawakwamua vijana kujiajiri wenyewe badala ya kuombaomba mtaani. Hii ni *value addition* ambayo tunaitaka. Unaposikia hao Wachina au watu wa India waliendelea waliwasimamia vijana kwa biashara ndogondogo. Leo ukimpa kifaa cha kubangua korosho atabangua atafanya *packaging* mafunzo atakwenda na yeye mwenyewe ataweza kujikwamua kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zimetolewa mashine vilevile kwa ajili ya watu wenye ulemavu. Leo mlemavu asiyeona, lakini ana mke na watoto ukimpa mke wake ataweza kubangua korosho yule mke wake na watoto wake wataweza kujikwamua kiuchumi na kuweza kujiendeleza katika uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi hiki cha Mheshimiwa Rais wameweza kugawa maeneo Mbogwe, Kahama. Leo walemavu na viziwi wanachimba dhahabu Kahama kitu ambacho ni mafanikio makubwa ambayo hatukutegemea mtu ambaye ni mlemavu akaweza kuchimba dhahabu. Mwenyezi Mungu awajalie na tumshukuru vilevile Mkurugenzi Mkuu wa *STAMICO* ametoa mitambo mikubwa ya kwenda kuchimba dhahabu kule Mbogwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kilimo; hapa ninapozungumza kuna vikundi vya vijana wenye ulemavu wa ngozi wamepewa mashamba Hombolo na hapa Bihawana na tayari wanalima alizeti. Ninasema hakuna kuachwa nyuma katika maendeleo. Katika maendeleo ukisema unakwenda na hawa, ukawaacha walemavu ina maana hujawatendea haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, katika siasa tuna asilimia tatu ya watu wenye ulemavu ambao wanatakiwa waingie ndani ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, apitie kokote, lakini anayo haki ya kimsingi, lakini mpaka sasa hivi tuna Wabunge walemavu ambao wameingia ni watatu tunahitaji nafasi tisa *extra* ziingie hapa kwa ajili ya kundi maalum, hii ni Sheria ya Umoja wa Mataifa. Kama nchi hii iliridhia watu wenye ulemavu wana haki ya kuingia katika Bunge hili kwa asilimia yao. Nina imani kuwa Serikali tukufu na sikivi italisimamia hili, itaendana nalo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mifuko ya Jamii; Waheshimiwa Wabunge tumetembelea Mifuko yetu ya *NSSF, PSSSF, OSHA, WCF* na *CMA*. Cha kusema sina, tulikwenda kwanza *NSSF* ilikuwa inakufa na ilishakufa. Leo *NSSF* katika mradi mmoja ule tu kwanza wa Kigamboni umeweza kupunguza matatizo mengi na kufanya ule Mfuko uweze kujiendesha. Niliomba Daraja la Busisi tuipatie *NSSF,* kwanza wana uzoefu katika uzoefu huu utailetea uchumi na itaweza kuifanya *NSSF* ambayo ilikuwa inaanguka kuweza kwenda mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *PSSSF;* tulitembelea *PSSSF* tukaona maendeleo makubwa na uchumi. Zamani tulikuwa tunagemea hii Mifuko ambayo waliiwekeza katika maeneo ambayo yalikuwa hayazalisha tutafanyaje watu watakapokuwa wanastaafu? Kwa kweli Mifuko yote inafanya kazi vizuri. Sasa hivi tuna imani hata kama mtu anastaafu hatazungushwa tena kwanza tuna kwenda kidigiti na wanafanya vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *OSHA;* mwanamke jembe anaitwa Khadija Mwenda amefanya kazi. Kwa kweli mimi mwenyewe nikimwona mwenyewe nina-*relax* hapa mbele sina cha kufanya ni kumwachia mwanamke mwenye uwezo aendelee. *WCF,* kwa kweli Mifuko hii yote inafanya kazi vizuri. Wamechaguliwa watu ambao ni wasikivu wanasimamia na tunazidi kuwaombea angalau wasiachwe ili angalau miaka mitano hii wazidi kuboresha katika maeneo haya ili tuweze kwenda mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitazungumzia bandari, katika njia kuu nne za uchumi mojawapo ni bandari, barabara, anga na mawasiliano. Bandari ambayo tulitegemea itakufa, lakini inakwenda vizuri sana. Ombi langu Serikali yangu isimamie bandari zile ndogondogo 56 ziende ikiwepo Bandari ya Lindi. Bandari ya Lindi na Mtwara sasa hivi itakuwa ni uchumi mkubwa wa kuunganisha Comoro na Tanzania na tayari wameshaingia katika mikataba ya kuhakikisha Comoro watatumia Bandari ya Lindi na Bandari ya Mtwara kuchukua mizigo yao ya kupeleka kule Comoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ilikuwa ni barabara, Mheshimiwa Rais baada ya kuiona barabara ya Lindi imefikia kiwango kile ametoa shilingi bilioni 600 ya kuanza nayo kwenye ile Bandari ya Lindi, Barabara ya kutoka Dar es Salaam mpaka Mtwara, lakini inavuka mpaka *Mozambique* na inavuka mpaka *South Africa*, watu wote wanatumia bandari hii, kwanza ni karibu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, kitendo cha Mheshimiwa Rais cha kutoa hizo pesa tunasema Mwenyezi Mungu azidi kusimama. Ombi langu wakandarasi wasije wakatuangusha. Kutolewa pesa kwa wakati na wao wafanye kazi yenye ubora ili angalau haya tunayoyakusudia maendeleo ya kiuchumi ambayo yataunganisha Tanzania, *Mozambique* mpaka *South Africa* iweze kufanyika kazi na sisi hatuna cha kusema. Tunamshukuru Mwenyezi Mungu aijalie Bandari ya Lindi na tayari tumeshatengenezewa fungu la kuweza kurekebisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Lindi, bidhaa badala ya kutoka mikoa ya mbali zitakuwa zinatoka Lindi kwenda Comoro. Lindi na Comoro ni kama unavyozungumzia Dar es Salaam na Zanzibar. Hivyo, tukisema biashara hii tuiendeleze itakuwa tumefanya jambo zuri sana na kazi nzuri sana ya Balozi wetu Yakubu ambaye yuko Comoro ya kusimamia, kuhakikisha bandari hizi za Lindi na Mtwara zinafanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bandari ya Mtwara ni *one of the best* bandari ambayo itabidi tuifanyie kazi. Bandari ya Mtwara

kutoka Zambia kwenda Dar es Salaam na kutoka Zambia kwenda Mtwara, ni karibu kwenda Mtwara kuliko kwenda Dar es Salaam. Kutoka Malawi kwenda Mtwara ni karibu kuliko kuja Dar es Salaam. Tukizidi kuisimamia ile Bandari ya Mtwara tutazidi kusimamia uchumi ambao utaweza kufanya mikoa hii iweze kupata ajira na kuondokana na umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, habari yangu ya mjusi naingojea Wizara ya Maliasili nitaenda kufanya nao kazi, kwa vile suala la mjusi ni suala mtambuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe upo hapa Mwenyezi Mungu akujaalie, mnafanya kazi vizuri Wenyeviti wa Bunge. Wabunge wangu Mwenyezi Mungu awajaalie awape afya njema ili twende tukafanye kazi ya kumsaidia Mheshimiwa Rais kwa umakini na ufasaha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa waliochukua mpira na kukimbia nawaende pembeni maana yake unaona, ada ya mja hunena, muungwana ni vitendo. Ukiona wanalumbana ina maana wamefilisika hawana cha kufanya. Mheshimiwa Rais ambaye ni mtulivu, mwenye heshima yake na mwenye ujasiri wake, Mwenyezi Mungu amlinde aweze kufanya kazi na sisi tuko pamoja naye. Mwenyezi Mungu awalinde sana na aibariki Tanzania na Watanzania. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Riziki Said Lulida. Nilimtaja Mheshimiwa Robert Chacha Maboto, Mheshimiwa Dkt. Angeline Sylvester Mabula ajiandae.

**MHE. ROBERT C. MABOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kupata nafasi. Pia, ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kupata fursa hii siku hii ya leo ya kuweza kusimama katika Bunge lako Tukufu na kuweza kusema machache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ninapenda kutoa pole kwa wananchi wangu wa Jimbo la Bunda Mjini na Watanzania kwa ujumla ambapo tumempoteza aliyekuwa Mkurugenzi wa

*TANESCO* ndugu yangu Gesima Nyamhanga ambaye ni mzawa jimboni kwangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili la msiba huu wa ndugu yetu Gesima Nyamhanga tumelipokea kwa masikitiko makubwa na wananchi wangu wa Jimbo la Bunda Mjini, lakini hatuna namna, yote haya ni mapenzi ya Mwenyezi Mungu. Ninawaomba tu wawe watulivu na wavumilivu katika kipindi hiki kigumu mpaka pale ambapo tutapata nafasi ya kuweza kumsitiri katika nyumba yake ya milele na tumwombee heri kwa Mwenyezi Mungu ili aweze kumpokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine napenda kumshukuru Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa ambayo ameendelea kuifanya kuhakikisha kwamba Jimbo letu la Bunda Mjini linapata miradi mbalimbali ya maendeleo na kuufanya Mji wetu wa Bunda uweze kupata mabadiliko makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepata miradi mingi katika kipindi hiki cha miaka minne ikiwa ni pamoja na ujenzi wa Hospitali yetu ya Wilaya ya Halmashauri ya Wilaya ya Mji wa Bunda ikiwa ni pamoja na kituo cha Afya katika Kata ya Waliku, kujenga zahanati katika kata zetu, kuimarisha miundombinu ya maji katika kata zilizoko pembezoni mwa Mji wa Bunda, kuhakikisha umeme unapatikana katika maeneo yote ya vitongoji katika Halmashauri ya Mji wa Bunda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais amefanya kazi kubwa miaka minne/mitano iliyopita Halmashauri ya Mji wa Bunda barabara zile za mitaa zilikuwa haziwezi kupitika na ziko ndani ya Halmashauri ya Mji wa Bunda, lakini kwa kipindi chake hiki cha miaka minne tumepata barabara nyingi na barabara zote sasa zinapitika. Tumefungua barabara mpya nyingi ambazo zinaifanya Halmashauri ya Mji wa Bunda ipitike kila mahali unakoweza kwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepata pia vyumba vya madarasa, shule za sekondari vyumba vya kutosha. Vinawafanya

wanafunzi wetu waweze kupata elimu iliyo bora kwa sababu mazingira yametengenezwa vizuri. Tumepata shule ya awali ya ufundi ambayo inajengwa kwenye Kata ya Sazira ambapo sasa iko kwenye hatua za mwisho ili iweze kuchukua wanafunzi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine tunaishukuru Serikali ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, Halmashauri ya Mji wa Bunda tuko kwenye miradi ile ya *TACTIC* ya Miji 28 ambayo inakuja kuboresha miji na kuufanya Mji wa Halmashauri ya Mji wa Bunda kuwa mji wa kisasa na mradi huo ndiyo mradi ambao wananchi wetu wa Jimbo la Bunda Mjini wanausubiri kwa hamu kubwa na matarajio makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaishukuru Serikali kwa sababu mchakato wa kwanza ambao utakwenda kujenga stendi, soko na lami kilometa 25.3 kwenye Halmashauri yetu ya Mji wa Bunda umeanza. Kwa hiyo, itaifanya Halmashauri ya Mji wa Bunda kuwa kivutio na kwa sababu iko pembezoni ya Mbuga ya Serengeti na ndiyo sehemu na lango la kuingilia Mkoa wa Mara inaufanya mji ule uweze kuvutia na kuwafanya wawekezaji waweze kuongezeka katika Halmashauri yetu ya Mji wa Bunda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanja vya wawekezaji vipo vya kutosha ambavyo vimepimwa na halmashauri. Kwa hiyo, watu wote ambao wanajihisi kwamba wanaweza kuwekeza Bunda tunawakaribisha kwa sababu maeneo yapo ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru vilevile Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi kubwa ambayo ameendelea kuifanya na kwa namna ambavyo amesimamia miradi mikubwa ya Serikali kwa miaka hii mitano na kuhakikisha kwamba miradi mingi imetekelezeka vizuri. Kwa kweli tunamshukuru kwa sababu amekuwa ni msimamizi mahiri ambaye pia ameifanya Serikali imeweza kutekeleza miradi yake vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nchi yetu ina tatizo la ajira kwa wananchi wake, lakini mimi ni mfanyabiashara kwa zaidi ya miaka 25. Miaka 25 iliyopita tuliokuwa tukianzisha biashara na

zama hizi za leo za mwaka 2025 ni zama tofauti. Miaka 25 iliyopita ilikuwa kijana wako anaweza akamaliza shule ukampa mtaji wa shilingi milioni moja au milioni mbili akaenda mtaani akafanya biashara na akapata matokeo, lakini leo kitu hicho hakiwezekani. Hakiwezekani kwa sababu ya mambo mbalimbali na gharama mbalimbali za uendeshaji wa kibiashara ambazo zimejitokeza na ambazo zinawakabili wafanyabiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninafikiri kwamba ni vizuri Serikali itengeneze mpango maalum kuhakikisha kwamba inatengeneza uwiano wa kodi kwa wafanyabiashara. Wafanyabiashara wanaweza kulipa kodi, lakini pia wafanyabiashara wanahitaji kuelimishwa zaidi ili waweze kulipa kodi kwa hiari yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, saa nyingine huwa najiuliza kwamba bajeti ya Serikali labda ni shilingi trilioni 30 inayokusanywa kutoka kwa wafanyabiashara, hii shilingi trilioni 30 inayokusanywa kutoka kwa wafanyabiashara inajulikana inakusanywa kutoka kwa mfanyabiashara gani na kwa kiasi gan?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ni hivyo ni kwa nini tufikie mahali ambapo labda viongozi wa Serikali wanaweza kwenda kuvutana na wafanyabiashara kwa sababu ukimwelimisha vizuri mfanyabiashara akaelewa suala la kulipa kodi ni suala la hiari na lazima ataenda kulipa kodi kwa ajili ya maendeleo ya nchi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa basi nikasema Serikali ni vizuri itengeneze miundombinu mizuri kati yake na wafanyabiashara ili wafanyabiashara hawa waendelee kulipa kodi kwa ajili ya maendeleo ya nchi yao. Leo hii vijana wetu wakipewa mitaji hii ambayo Serikali imefanya kila linalowezekana kuhakikisha kwamba inatoa hela kwenye halmashauri halafu fedha zile yanakopeshwa makundi maalum yakiwemo ya vijana, lakini leo kijana akipata mtaji wa shilingi milioni moja akaenda nao sokoni, saa nyingine mtaji huo utaishia kwenye gharama za uendeshaji kabla ya kufungua biashara yake. Atalipa kodi na michango mbalimbali kabla ya kufungua biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati huko masoko yetu ya biashara yameingiliwa na watu wengi ikiwa ni pamoja na wageni wa kutoka nje ambao wao wakija kwenye nchi yetu na mitaji yao inakuwa ni mitaji mikubwa kuliko mitaji yetu sisi Watanzania, kwa sababu fedha zetu zinakuwa kwenye thamani ya chini na fedha zao zinakuwa na thamani ya juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunapowapeleka watu wetu katika ushindani wa kibiashara na hawa watu hawataweza ku-*compete* kwa sababu wale wataonekana wanaweza kufanya biashara kubwa kuliko watu wetu. Zaidi ya hapo tutakuwa na vijana ambao watakuwa wapo na wanapata mitaji hii ambayo wanakopeshwa na Serikali wanaitumia na hawawezi kurejesha kwa sababu ya miundombinu ambayo imetengenezwa. Kwa hiyo, ni vizuri Serikali ifanye kila linalowezekana kuwalinda wafanyabiashara wake wadogo walioko nchini, kwa kutengenezea njia madhubuti ambayo itawafanya waweze kufanya biashara zao kwa uhuru, lakini kulingana pia na mitaji yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo mtu ana mtaji wake huu wa shilingi milioni moja au milioni mbili akapelekewa kodi ya shilingi 800,000 katika mtaji wa shilingi 2,000,000 haitawezekana kulipa hiyo kodi, kwa vyovyote vile atakukwepa tu, lakini ukitengeneza miundombinu ambayo itamfanya katika shilingi milioni mbili aliyonayo akaona kodi ni chini ya shilingi 200,000 anaweza kulipa vizuri, nje ya hapo utalaumiana na wafanyabiashara na mwisho watakwepa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, si kweli kwamba Watanzania hawataki kulipa kodi, wanataka kulipa. Pia, tunataka wale ambao wanasimamia kwenye vitengo vya kodi na wao wasaidie kujua wafanyabiashara namna ya kulipa kodi katika usawa ambao unawaruhusu kuishi katika maisha yao. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. ROBERT C. MABOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa nafasi na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Robert Chacha Maboto. Nilimtaja Mheshimiwa Dkt. Angeline Sylvester Mabula, Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela na Mheshimiwa Dkt. Thea Medard Ntara wajiandae.

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa asubuhi ya leo nami kuchangia bajeti hii ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Kwanza, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia afya njema na hatimaye tunashiriki katika bajeti hii ya Waziri Mkuu ambayo imeibeba Serikali nzima katika suala zima la kimaendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana Waziri Mkuu pamoja na timu yake ya Mawaziri; Waziri Lukuvi, Waziri Ridhiwani pamoja na wasaidizi wao kwa kazi kubwa na nzuri ambayo wameifanya katika kipindi hiki na bajeti ni nzuri na imegusa maeneo yote hasa kwa kuonesha mafanikio ya Awamu ya Sita chini ya Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa sababu aliichukua nchi katika kipindi kigumu sana na kwa sababu ya jinsia yake kwamba ni mwanamke hawakuamini kama angeweza kufanya kazi hizi. Amefanya kazi hizi kwa utulivu mkubwa na hasa kwa kuendeleza ile miradi ya kimkakati ambayo ilikuwa imeanzishwa na awamu zilizopita na yote sasa inakamilika. Kwa kweli tumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kumpa hekima Rais wetu na kuweza kuyafanya maendeleo haya kwa uhakika na usahihi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, falsafa yake ya *4R's* aliyokuja nayo ni falsafa ambayo imeleta umoja, mshikamano, upendo na amani zaidi katika Taifa hili kwa sababu ukiangalia namna ambavyo tulikuwa tukiishi labda katika vyama vya upinzani na nini kidogo kulikuwa na changamoto kubwa. Baada ya kuwaleta wote pamoja watu wote waka-*focus* kwenye maendeleo na

ndiyo maana kazi amezifanya kwa utulivu sana. Ninamshukuru sana katika hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijachangia bajeti ya Waziri Mkuu kwa uhakika kwanza nianze kwa kuishukuru sana Serikali kwa namna ambavyo Jimbo la Ilemela limenufaika na miradi mingi ya maendeleo katika kipindi kifupi sana na hasa katika kipindi hiki cha miaka minne ambacho tunakizungumzia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais alijikita zaidi katika suala la huduma za kijamii. Ukiangalia Ilemela ilivyokuwa awali na sasa ni vitu viwili tofauti. Unaweza usiamini, kama ulifika pale 2015 na leo ukienda huwezi kuamini. Jambo la kwanza ni kwenye suala zima la miundombinu ya elimu. Tumepata shule mpya zaidi ya 10 ambazo zote zinakwenda vizuri na kwa bahati nzuri shule ya Amali ambayo ndiyo kwanza imeanza, Ilemela tumeipata na inajengwa katika Kata ya Bugogwa. Tuna imani sasa watoto wetu wataweza kupata elimu ambayo pia itawajengea mazingira ya kuja kupata ajira kwa baadaye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kwenye afya tulikuwa na hospitali ya wilaya. Sasa hivi tuna vituo vya afya zaidi ya vitano na tulikuwa navyo viwili na tuna zahanati zaidi ya 13 na bado wananchi wanajenga kwa sababu *slogan* yetu ni, Ilemela ni yetu Tushirikiane Kuijenga. Kwa hiyo, kwa namna yoyote ile wananchi wanaibua miradi, Mbunge anawekeza pale na Serikali inakamilisha mambo yanakwenda mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unakuta miradi yote inakwenda kwa muda mfupi na inakwisha. Ukija kwenye miradi ya maji amewekeza katika mradi wa maji maeneo mengi sana. Ukija kwenye miradi ya maji amewekeza katika mradi wa maji maeneo mengi sana na fedha nyingi zimewekezwa, lakini changamoto iliyopo pengine ile miundombinu ya usambazaji bado sio mizuri sana. Ukiambiwa kwamba kuna watu hawana maji au wanapata maji mara mbili kwa wiki na ziwa liko pale huwezi kuamini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishukuru Serikali kwa sababu sasa hivi kuna miradi mingi ambayo inaendelea. Tuna ile miradi ya

matokeo ya haraka. Tumepewa shilingi bilioni 4.7 ambayo inakwenda kusambaza maji karibu kilometa 68 eneo la Kahama, Buswelu, Nyamdoke na Ilalila, wanakwenda kuboresha chanzo cha maji cha Kabangaja ambacho kitakuwa kinazalisha lita za maji milioni 3.6 kwa siku na ambacho kitakwenda ku-*save* eneo la Igombe, Kayenze na Sangabuye na kimefikia 70%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hiyo haitoshi tuna upanuzi wa chanzo cha maji pale Capri *Point* ambapo napo tuna imani lita za ujazo milioni 46 zitaweza kuzalishwa pale na zitaletwa upande wa Ilemela. Kwa hiyo, inawezekana changamoto hiyo ikaisha. Ninaishukuru sana Serikali kwa sababu ilikuwa ni changamoto kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunalo eneo letu la Kisiwa cha Bezi hawajawahi kuona maji ya bomba; siku zote wanakunywa maji ya ziwani; wanahangaika na maji hayo. Sasa hivi tayari ameshapatikana mkandarasi; wako kwenye manunuzi nao wanakwenda kupata maji ya bomba kama wengine wanavyopata. Ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais katika suala hilo ambalo ameweza kuwezesha katika jimbo langu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna stendi mpya kabisa, zaidi ya halmashauri sita zimekuja kujifunza. Sasa ombi langu kwa Serikali katika hilo, kwa sababu Nyamagana kuna stendi nzuri na Ilemela kuna stendi nzuri. Sasa ni namna tu ya ku-*coordinate* na tukaweza kuzitumia zile ili zisionekane kama ni *white elephant* kwa sababu ziko vizuri, lakini mabasi namna ya kwenda. Kwa hiyo, hilo ni suala la usimamizi tu ambalo linaweza likaenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazo barabara zetu za *TARURA* na tumepokea zaidi ya shilingi bilioni 9.0 kwa kipindi hiki tu cha Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, lakini kilometa ambazo zinahudumiwa ni 875. Mzunguko wa barabara ni kilometa 1,920. Tuna barabara za lami kilometa 43 tu sawa na 5.5%. Kwa hiyo, unakuta uharibifu wa barabara zilizo nyingi kila mvua inaponyesha barabara zinapata changamoto kubwa kwa sababu ya mvua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Serikali iwaangalie vizuri *TARURA* na namna bora ya kuweza kuboresha zile barabara zikawa za lami, basi angalau tukaondokana na hali ya kila mwaka kuweza kufanya mabadiliko hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi pia tunanufaika na mradi wa *TACTIC* na tayari kuna mradi wa Soko la Kirumba na kilomita 2.9 za lami zinakwenda kujengwa pale, lakini tunalo Soko la Kabwalo nalo pia linakwenda kujengwa, kwa hiyo, ninachotaka kusema tu ni kwamba miradi inapokuwa ipo tayari tuombe sasa wakandarasi waweze ku-*take off* haraka badala ya kufika *site* halafu anapotea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa kwenye barabara tunao wakandarasi zaidi ya watano wameshafika *site* halafu hawapo. Kwa hiyo, namna hii wakati mwingine inaleta picha ambayo sio nzuri sana. Hali halisi ni kwamba miradi ile ipo na tayari wakandarasi wamepewa na tunakwenda kufanya kazi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiangalia katika miundombinu kitaifa ambayo inakwenda. Kwa mfano Uwanja wa Ndege wa Mwanza unapanuliwa na katika upanuzi ule tutakwenda kunufaika kwa sababu mazao ya samaki tayari tunayo ndege ambayo inabeba mazao kupeleka nje, Watanzania watanufaika wakiwemo Wanailemela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto kubwa iliyopo tu pale ni kwamba, niombe tu Serikali ikamilishe masuala mazima ya fidia ili watu waweze kuishi kwa amani pale. Kwa sababu fidia zimetolewa Kilimanjaro, zimetolewa Dar es Salaam sasa na Ilemela nao ninaomba wakamilishe kwa sababu ule mradi ni mkubwa ambao unahitaji kukamilika. Habari ya kusema watawapa viwanja na nini, ni kuchanganya watu tu mawazo. Kama ni fidia wapewe tujue ni fidia ili na wao waweze kuishi na ule mradi uweze kuendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la umeme, nipongeze sana Serikali. Umeme sasa hivi Bwawa la Mwalimu Nyerere

limekamilika. Megawati 2,115 ziko tayari, ambazo zinakuja kuleta jumla ya megawati zaidi 4,000 kwa nchi nzima. Maana yake ni kwamba, tuna zaidi ya umeme kuliko ule tunaohitaji kutumia, kwa sababu katika matumizi ya umeme tunaotumia hauzidi megawati 2,190. Changamoto inakuja kukatika kwa umeme. Niombe tu kwa sababu mimi ni mdau kwenye Kamati ya Nishati na Madini. Niombe sana, umeme unaozalishwa ni mwingi, tuombe *regular maintenance* kwenye vituo vyetu vya kupoozea umeme na uboreshaji njia za usambazaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme unakuja kwa kilovolti 400 kwenye kituo cha kupoozea, unatoka pale kwa kilovolti 220 au 132. Kwa hiyo, unakuta miundombinu katikati pia haiko sawa. Nguzo ziko nyingi zimelala zimeanguka, lakini hazijawekwa. Zingine zinazobadilishwa ziko zimelala. Niombe sana usimamizi uendelee kuwa wa karibu zaidi, kwa sababu namwamini Naibu Waziri Mkuu ni msimamizi mzuri na kazi inaenda vizuri. Basi hawa walioko chini waweze kufanya hasa kwenye *regular maintenances* ili wananchi waelewe kwamba, umeme tunao wa kutosha na umeme utaimarika kwa sababu changamoto iliyopo sasa ni usambazaji tu ambao unahitaji kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee *SGR*. Nipongeze sana ni mradi mzuri, lakini niwaombe Serikali kuna *over employment* pale ambayo haina sababu. Wako watumishi wengi ambao ukiwaangalia wanachukua fursa kubwa katika kuteka yale maeneo ambayo sasa wangeweza kuweka abiria wengi na wakazalisha zaidi. Kunakuwa na watumishi wengi ambao hata yale mafunzo hawana. Ikitokea hitilafu kidogo tu anawaambia tokeni tokeni. Ilitutokea sisi bahati mbaya Kilosa, mtumishi anakuja anasema, “tokeni, tokeni moto unawaka!” Maana yake hata yale mafunzo hana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa namna hiyo ndio unakuta umeme hauja- *stabilize* katika kuendesha unaweza ukakuta watu wenye ugonjwa wa moyo na wengine wanakanyagana. Niombe sana ajira zile, ziangaliwe watu wawekwe wenye utaalam. Pia na lugha yao kwa abiria iweze kuwa nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipongeze Serikali kwa ajira nyingi ambayo ipo, lakini tuelekeze zaidi katika Sekta Binafsi ambazo zimekuwa hasa zinaajiri watu wengi sana. Kuhusu Bolti wamelizungumzia suala la kodi bado ni changamoto sitaki kulirudia kwa sababu amelizungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usafiri wa anga; tuna ndege nyingi za kutosha, lakini *route* za ndani tuziangalie vizuri na hasa hapa Dodoma. Dodoma – Mwanza, Dodoma – Arusha, Dodoma – Mbeya ni muhimu kuwa na ndege hapa. Wasafiri wengi wanakuja hapa Makao Makuu, lakini anatokea Mwanza lazima afike Dar es Salaam ndio aje hapa. Anatoka zake Mbeya achukue ndege aje huku kama hana gari. Kwa nini tusiwe na usafiri wa hapa kwa sababu ndege tunazo za kutosha? Tuone namna bora ya kuboresha usafiri wa ndani. Tumeongeza usafiri wa nje ni kweli abiria wanaongezeka basi niombe tuone namna ya kuangalia ratiba zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana ahsante kwa fursa uliyonipa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Angeline Sylvester Mabula. Nilimtaja Mheshimiwa…

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, nilimtaja Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela, Mheshimiwa Dkt. Thea Medard Ntara na Mheshimiwa Michael Mwita Kembaki wajiandae.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi. Ninaomba nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kunipa uhai. Pia, niwashukuru familia yangu kwa kuendelea kunivumilia nikiwa katika majukumu. Ninawashukuru pia wananchi wangu kwa kuendelea kunipa mkono na kunipa moyo katika kutimiza majukumu yangu ya kibunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuipongeza Serikali ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, Serikali ya Awamu ya Sita kwa jitihada zake kubwa za kufanya maendeleo kila namna. Pongezi zangu zitajikita moja kwa moja kwenye eneo moja tu la kilimo na ni kwa sababu ninazo sababu za kufanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze pia Mheshimiwa Makamu wa Rais wa nchi, Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango kwa kuifanya nchi ikawa tulivu na tunafanya majukumu yetu pasipokuwa na changamoto, kwa kumsaidia Mheshimiwa Rais katika kumshauri mambo kadha wa kadha jinsi ya kuiendesha nchi na kuifanya nchi ikawa tulivu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze pia Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi yake kubwa ya kulituliza hili Bunge. Kama mnavyoona Bunge linafanya kazi njema kabisa na Bunge hili ni Bunge la mfano katika Mabunge ya Nchi hii, kutokana na utendaji wake wa kazi na mafanikio ambayo Bunge hili limefikia na nchi kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema nitajikita katika suala la kilimo. Bunge hili lilimshauri sana Mheshimiwa Rais na lilishauri kupitia Wizara ya Kilimo na hapa Mheshimiwa Waziri wa Kilimo naye atapata pongezi kwa kuchukua ushauri wetu mwingi sana kutoka kwenye hili Bunge na kuutendea kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miongoni mwa ushauri mkubwa kabisa ambao ameuchukua kutoka kwenye Bunge hili na ambao una tija kubwa sana katika suala la kilimo ni kupandisha Bajeti ya Kilimo kutoka takribani shilingi bilioni 257 na kufikia shilingi bilioni 957 inakwenda kwenye trilioni moja na zaidi sasa hivi. Haya ni mafanikio makubwa sana na mafanikio haya utakuwa umeyaona katika maeneo kadhaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na ushauri ambao ameuchukua kupitia Bunge hili ni ule ushauri wa kuanzisha mikakati kadhaa ya kuhakikisha zao la korosho linakwenda vizuri au linachukuliwa kwa umakini. Kwa mfano tangu mwaka 2021 tulishauri Serikali ya Awamu ya Sita kwenye suala la kilimo cha

korosho kuweka pembejeo na ushauri huu ulipokelewa. Mpaka sasa hivi pembejeo zenye thamani ya Dola za Kimarekani takribani milioni 600 na zaidi zimeingia katika zao la korosho pekee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge hili lilimshauri Mheshimiwa Waziri kuhusiana na jambo la korosho hususan ushauri ulitoka kutoka kwa wadau wa Mikoa ya Mtwara, Lindi, Ruvuma na Pwani ambapo tulimshauri kutumia njia bora ya mnada kutoka katika mnada ule wa zamani wa *box* na kutumia mnada wa kisasa ambao ni *TMX*. Huu ni mnada ambao unatumika katika mtandao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri huu umeboresha sana mapato ya mwananchi kwa maana ya mapato ya mkulima. Kwanza, bei kutoka takribani shilingi 1,560 mwaka 2021, mwaka jana tulibahatika kufika bei ya korosho kwa kilo takribani shilingi 4,195. Haya ni maendeleo makubwa sana na ni matokeo makubwa sana ya kupokea ushauri wa Bunge hili. Hapo tunaweza kusema kabisa kwamba pongezi na hongera ziende moja kwa moja kwa Mheshimiwa Rais kwa kuyapokea mapendekezo yetu kwa mikono miwili pasipokuwa na mawaa yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri mwingine ambao tumeshawahi kuutoa na ukapokelewa ni kurekebisha njia mbalimbali ya uendeshaji wa shughuli zote. Kwa mfano, tulishauri suala la kuweka kiasi cha pesa kwenye Mfuko wa Bodi ya Korosho na hili lilitekelezwa. Bodi ya Korosho pia ilipewa kiasi cha pesa za kutosha za kuendesha shughuli zake kama vile za kiuchunguzi na shughuli zingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na sifa hizi zote ambazo zimekwenda kwenye Serikali ya Awamu ya Sita, kupitia Waziri wa Kilimo na wasaidizi wake. Bado kuna mapungufu ambayo tunastahili kutaka kuyasemea ambayo nayo kwayo kama yatasikilizwa jinsi gani tunavyoshauri, bila shaka sasa hivi siku za usoni hali itakuwa nzuri zaidi ya hapa tulipo sasa hivi. Kwa mfano, kwenye zao hili la korosho bado tunaendelea kutumia kilimo cha mvua ambacho chenyewe hakina uhakika sana. Kuna wakati

mvua zinanyesha kwa wingi na kuharibu zao la korosho, lakini kuna wakati inanyesha kidogo na kufanya korosho zipatikane kwa uchache sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo yote kama tulivyosema kwamba ni mashauri ambayo yanaweza kutusaidia huko mbeleni. Pia, katika kueleza mafanikio kuna jambo moja nilishindwa kulidokeza ambalo ni muhimu sana katika mafanikio makubwa ya kilimo ambayo yamejitokeza. Kwa mfano, mpaka mwaka jana tulipata fedha za kigeni kwa maana ya dola takribani milioni 583.7 ambazo ni sawasawa na shilingi trilioni 1.8 kwenye zao la korosho pekee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi kwa maana ya wakulima wao walipata takribani dola 471,380,000 ambazo ni sawasawa takribani shilingi trilioni 1.4. Unaweza ukaona kwamba, ni pesa nyingi sana ambazo zimekuja kwenda kuleta mapinduzi makubwa ya kiuchumi katika nchi hii, hali kadhalika kwa mwananchi mmoja mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa ujumla pia hata ukiangalia katika suala la mnyororo wa thamani. Kwa mfano, kumekuwa na huduma mbalimbali ambazo zilikuwa zikitolewa ambazo zimefanikisha na zenyewe kuchangia pato la wale walioshughulika na shughuli hii. Kwa mfano, kumekuwa na suala la viunganishi pamoja na huduma nyingine za kwenye mnyororo wa thamani takribani shilingi bilioni 200 zimepitia katika eneo hili. Ni kiasi kikubwa kama nilivyojaribu kusema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na ukubwa huu wote bado tungetamani kwamba Serikali iende zaidi, tuondokane na hii hali ya kutumia mvua kama ni nyenzo pekee ya kufanya zao hili la korosho liboreke. Badala yake tuweze kuwa na kilimo cha umwagiliaji maana yake kwamba, tuchague baadhi ya watu ambao wana mashamba makubwa ya korosho tuwakopeshe visima na tutoboe visima virefu kusudi kuwakopesha hawa wakulima wenye mashamba makubwa waweke miundombinu ambayo itawawezesha kumwagilia korosho badala ya kuendelea kutumia kilimo cha mvua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa nafasi hii, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela. Nilimtaja Mheshimiwa Dkt. Thea Medard Ntara, Mheshimiwa Michael Mwita Kembaki ajiandae.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi. Nianze, kwa kupongeza sana Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na nitaenda kwenye eneo hasa la vyuo vikuu, vyuo vya kati pamoja na viwanja vya michezo kwa sababu niko kwenye Kamati ya Elimu na Utamaduni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumetembelea katika majengo ya vyuo vikuu kama *University of Dar es Salaam,* Ardhi *na DIT*. Niseme ukweli usiofichika kwamba, kazi nzuri imefanyika katika vyuo hivyo hasa kwenye haya majengo mapya ya *DIT*. Tukienda pale, kwanza ni kama sehemu ya utalii. Yale majengo yamejengwa kwa ustadi na kinachofurahisha sana, Ofisi ya Waziri Mkuu kila tulipokwenda walileta mwakilishi wa kuja kuona jinsi Serikali inavyofanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kusema hivyo nina maana kwamba, Ofisi ya Waziri Mkuu kumbe inafuatilia na kusimamia ujenzi katika vyuo vikuu. Lingine ambalo lilionekana ni zuri vijana wetu ambao wamesoma katika vyuo hivyo wengi wameajiriwa pale na ndio wanaosimamia ujenzi wa hayo majengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tulipokwenda pale *DIT* kuna kitu kipya kimeanzishwa pale. Wale wanakwenda kurusha *satellite*. Sasa, *satellite* ni kitu kipya na kwa nchi yetu hii ya Tanzania kuweza kurusha kitu hicho, kuna wale wa nchi nyingine zilizoendelea wataona kama kuna wivu fulani hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Ofisi ya Waziri Mkuu, *right from the beginning* waanze kufuatilia ule mradi ili utakapokamilika na kuweza kurushwa 2026 usiwe na dosari. Hili jambo ni kubwa na ni jambo ambalo hatukutegemea, lakini kile chuo kinafanya ile kazi kikishirikiana na wadau mbalimbali

ikiwemo Wizara ya Mambo ya Ndani, Wizara ya Elimu yenyewe, Wajapani wako pale na *UN Organization* moja iko pale. Kwa hiyo, nilitaka kusema kwamba, ni vizuri Serikali, Ofisi ya Waziri Mkuu ijue kwamba kuna *project* kubwa pale, hivyo waweke jicho katika mradi ule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, bado tulitembelea viwanja. Nasema katika ujenzi wa kiwanja bora ni kile Kiwanja cha Arusha. Wizara ya Michezo wamesimamia vizuri, lakini ninaamini hata kule kulikuwa na timu ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Kwa hiyo, niseme hii miradi mikubwa, Ofisi ya Waziri Mkuu inapoweka jicho pale kwa kweli ufanisi unaonekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye habari ya mikopo, nipongeze sana Ofisi ya Waziri Mkuu. Hata tuliposema kwamba mikopo sasa hivi haitoshi mmeongeza. Ni juzi tu nilipiga simu tena nilipiga saa ambazo huwezi kupiga simu. Nilimpigia simu Waziri Mkuu kwamba kuna tatizo watoto wanahitaji fedha na alifanyia kazi usiku ule ule na asubuhi wakawekewa fedha watoto ili watulie wapate fedha yao ya *accommodation* pamoja na *tuition fee*. Hongera sana, huo ndio ufuatiliaji tunaoutaka. Tatizo limesemwa, wakawajibika *immediately*. Hapo nawapa pongezi nyingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo nisisahau hili jambo. Kuna jambo lile nimelizungumza leo ni mara ya tatu, kuhusu mafao ya wakuu wa vyuo vikuu. Mheshimiwa Lukuvi unanisikia hapo, hili jambo tumeliongea. Hao wakuu wa vyuo wamekaa wanasubiri wanasema liko kwenye meza. Niwaombe wakalichukue hapo kwenye meza walishike mkononi wamalizie hilo suala la mafao ya vyuo vikuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi juzi kuna mafao ya watu wale wa vyeti feki, walilifanyia kazi haraka sana. Hawa wahadhiri wa vyuo vikuu ambao ni *Professors* na wasimamizi wa vyuo bado mpaka leo hivi ninavyoongea haijulikani nini kinaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo niunganishe na mafao ya wale waliofanya kazi na Mheshimiwa Lukuvi, wale

wakuu wa wilaya ambao bado mpaka leo wanadai *handshake*. Wale ndio waliojenga zile shule za kata, walisimamia vizuri mno. Mheshimiwa Lukuvi analifahamu hilo, hebu sasa ufike wakati tumalizane nao kama walivyomalizana na wale watumishi wa vyeti *fake* waliwalipa. Mheshimiwa Rais alikuwa na huruma akasema jamani wapeni na hawa hebu wakumbushe, lakini nafikiri yeye ameshamaliza hilo. Nimwombe sana Mheshimiwa Lukuvi yuko hapo wakawajibike kwenye hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nataka kulizungumzia tena leo kwa mara ya nne ni kuhusu *Teaching Hospitals.* Hawa wadau wanapokuja kutaka kutusaidia jambo lolote katika hospitali zetu, huwa wanauliza, hii hospitali ina mahusiano na *university* ipi? Wakijua hilo, basi kuna uwekezaji wataufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Profesa Pallangyo na wenzake waliandika *proposal* nzuri ya *Teaching Hospital* Mloganzila. Walivyoandika, wakaomba na eneo, wakapata Mloganzila. Walivyolipata lile eneo, hospitali ikaanza kuyatamani yale majengo, wakaanza kuleta, mimi nafikiri hizo ni figisu, kwa sababu wale wameandika *proposal* ya hiyo Mloganzila, wameomba na kiwanja wamepata, majengo yamekaa yametulia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wakaenda kusema, tena wakamshauri Waziri pale, kengele ya ngapi?

*(Hapa kengele ya kwanza ililia)*

**WABUNGE FULANI:** Mheshimiwa wewe endelea tu…

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakasema pale hapafai, wakaanza kuleta figisu. Wakapeleka watumishi pale Mloganzila ambao hawafanyi kazi vizuri, Mkurugenzi wa pale akawa anakosa ile *NHIF*. Kwa kufanya hivyo, uwajibikaji katika ile hospitali ukaonekana wa ovyo. Ninyi Wabunge ni mashahidi, mambo yalikuwa hayaendi vizuri, kwa hiyo ilikuwa kama *sabotage.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadaye iliundwa Kamati na Tume, Mheshimiwa Waziri Ummy wakati huo anafahamu. Wakaenda kuandika, wakakuta kumbe hakuna tatizo, ni watu tu wenye ubinafsi na waliokosa uzalendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa ile ripoti ambayo iko kwenye meza ya Katibu Mkuu Kiongozi, mkaiangalie muone ile Mloganzila irudi iwe ni *Teaching Hospital.* Ikiwa ni *Teaching Hospital,* mimi nawaambieni, huko ndiyo kunapatikana wabunifu na wale *specialists*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii Marekani ina *Teaching Hospital* 50, Nigeria wana *Teaching Hospital,* Zambia wana *Teaching Hospital,* Nairobi wana *Teaching Hospital*, na sisi hapa lazima tuwe na *Teaching Hospital* Mloganzila na Benjamini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ushirikiano mzuri upo kati ya *UDOM* na Benjamini. Niwaambie, sasa hivi wameletewa mradi wa figo pale Benjamini na waliwaletea baada ya kujua Benjamini ina ushirikiano mzuri na *UDOM.* Kwa hiyo, nataka kusema kwamba ni lazima sasa tujipange tuwe na *Teaching Hospitals* zetu. Benjamini ambayo inaonekana sasa hivi inafanya vizuri, ina ushirikiano mzuri, na wanafunzi wanatoka *UDOM* wanakwenda pale Benjamini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hilo tu, wadau wote wa maendeleo wakiona hospitali ina ushirikiano na *University* ndiyo wanawekeza mradi. Hawa Wajapani walikataa mwanzoni, wakasema mlikuwa hamna uhusiano mzuri. Leo kuna uhusiano mzuri, wameenda kuwekeza pale kitu kinachoitwa mradi mkubwa kabisa kwa ajili ya figo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naliomba hili tusilichukulie mzaha sasa hivi, tuliweke kabisa *seriously.* Kitu kingine, hivi nchi inakuwaje na *National Hospital* moja? Nchi inaweza kuwa na National Hospital mbili au tatu. Mkiboresha Benjamini, na kuruhusu miradi iende pale, tutakuwa angalau tuna *National Hospitals* mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, viongozi wote wa Kitaifa leo hapa wakiugua, mimi siyo wa Kitaifa; leo viongozi wote wa Kitaifa wakiugua, ninyi Wabunge mnakimbilia wapi? Ni Benjamini, lakini juzi wamekwenda Ubalozi wa Marekani, wametembea Benjamini, wakaona he, kumbe inafanya vizuri hivi! Kwa hiyo, unaona hata wageni, mabalozi wataiamini Benjamini, kwa sababu hii ndiyo ya Makao Makuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba sana sana, tusisitize au tujitahidi kuifanya ile iboreke zaidi ili iwe na hadhi ya kuwa *National Hospital* na wanafunzi wetu waweze kufanya kazi pale, tupate wabobezi. Tutakwenda India mpaka lini? Tutakwenda *South Africa* mpaka lini? Tunataka tukiugua tutibiwe kwenye nchi yetu. Kwa kufanya hivyo, na ili tuweze kufika huko, lazima tuwekeze kwenye hospitali zetu hizi mbili tena, tuwekeze kwa kuruhusu wanafunzi wale wa Muhimbili *University* waende Mloganzila. Pia iangaliwe kwamba kuna uhusiano mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Thea Medard Ntara ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Michael Mwita Kembaki, Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate na Mheshimiwa Kilumbe Shabani Ng'enda ajiandae, Mheshimiwa Michael.

**MHE. MICHAEL M. KEMBAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia katika siku ya leo. Kwanza kabisa, naomba nichukue nafasi hii kuwashukuru sana wananchi wa Tarime Mjini kwa kuniamini na pia uchapaji kazi wao. Wanafanya kazi vizuri katika kuijenga Tarime yetu na Taifa letu kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba nichukue nafasi hii kumshukuru sana Rais wetu, Mama Samia Suluhu Hassan kwa sababu amefanya mazuri katika jimbo letu la Tarime Mjini. Tulikuwa na tatizo kubwa sana la soko, ameleta fedha na tumepata soko la kisasa kabisa ambalo sasa watu wa Tarime

watapa sehemu ya kufanyia biashara na uchumi wa Mji wetu kukua siku hadi siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nitajikita sana katika tatizo kubwa ambalo lipo katika nchi yetu la ukosefu wa ajira kwa vijana wetu. Tarehe 07/01/2022 Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akiwa kule katika Mkoa wa Magharibi alisema maneno haya, "Serikali yenu tunajua tatizo la ajira na tunalifanyia kazi ili kutengeneza fursa mbalimbali ili vijana wapate ajira."

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la ajira ni kubwa sana katika nchi yetu na inasababisha umasikini kukithiri katika jamii yetu. Tatizo la ajira linafanya kupungua kwa kipato cha familia, lakini pia kuongezeka kwa umaskini katika familia. Ukosefu wa ajira unasababisha Serikali ikose kodi kwa sababu watu wengi hawana kazi ya kufanya na hivyo kusababisha upungufu huu wa kodi katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia uchumi wa nchi unadorora kutokana na ukosefu wa ajira kwa watu wengi ambao hawana ajira. Matatizo mengi ya kifamilia ambayo yanatokea mara nyingi yanasababishwa na ukosefu wa ajira katika jamii yetu. Watu wengi wanakuwa tegemezi, na wanaofanya kazi ni wachache, hivyo kusababisha utegemezi katika jamii yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukosefu wa ajira husababisha pia ucheleweshaji wa malengo ya mtu binafsi, lakini pia kwa Taifa letu kwa ujumla. Hizi ni baadhi ya hasara za ukosefu wa ajira katika Taifa letu la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama unavyojua, moja ya mambo ambayo yanasababisha ukosefu wa ajira ni kwamba watu wanakuwa wengi kuliko nafasi za kazi zilizopo. Katika nchi nyingi za Afrika, 70% ya watu ni vijana ambao ndio wanaofanya kazi zaidi kuliko wazee. Ukiangalia katika Taifa letu kulingana na sensa iliyofanyika mwaka 2022 vijana ni wengi kuliko wazee, hivyo watu wanaohitaji kazi ni wengi kuliko kazi zenyewe zilizopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niseme kidogo kuhusu chanzo cha ukosefu wa ajira. Binafsi nimefanya utafiti nikaona miongoni mwa vitu vinavyosababisha ukosefu wa ajira katika Taifa letu ni mfumo wa elimu unaotolewa katika nchi yetu. Mfumo wa elimu unaotolewa katika nchi yetu haukidhi mahitaji, nayo inasababisha wale ambao wanaopata elimu kukosa mwelekeo baada ya kuwa wamehitimu katika masomo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo wa elimu unaotolewa katika nchi yetu haumfanyi mwanafunzi kujitegemea, kwani mfumo wa elimu unaotolewa katika nchi yetu unamfanya mwanafunzi kuwa mtumwa wa ajira badala ya kujiajiri. Mfumo wa elimu unaotolewa katika nchi yetu humfanya mwanafunzi asiwe mbunifu katika maisha ya siku hadi siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia katika mfumo wa elimu unaotolewa katika nchi yetu umeegemea sana katika mambo ambayo hayaendani na uhalisia wa maisha halisi ya Mtanzania, ili tuweze kutatua tatizo la ajira katika nchi yetu, lazima tuangalie wazee wetu; baba na babu zetu walikuwa wanafanya nini kabla mambo kubadilika? Enzi hizo wakati wa baba zetu kulikuwa hamna tatizo la ukosefu wa ajira, lakini ukosefu wa ajira umekuja baada ya elimu kuanza kutolewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tujifunze ni yapi ambayo yalikuwa yanafanyika enzi hizo na kutatua changamoto ya ukosefu wa ajira katika miaka hiyo. Kwanza, lazima tuangalie uhalisia, baba zetu walikuwa wanafanya nini? Baba zetu walikuwa wanafanya kazi ya ufugaji, kilimo, uvuvi, uhunzi na kazi hizi zote ndizo ambazo zimeajiri watu wengi sana katika Taifa letu la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiangalia katika mfumo huu, baba zetu wakati wote walikuwa wanahamasisha vijana kwenda shambani, walikuwa wanasifia hata wakati kijana anataka kuoa walikuwa wanaangalia ni familia ipi ambayo hakuna njaa? Ni familia ipi ambayo inajua kulima? Hivyo walihakikisha kwamba wanaleta nguvu kazi katika familia ili uzalishaji uendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii ninapozungumza, ukienda katika shule zetu, shule za msingi, elimu ya awali, elimu ya sekondari na vyuo vikuu tumefanya hivi vitu ambavyo ni vya asili ya Mtanzania; ufugaji, uvuvi, kilimo na uhunzi vimekua ni vitu ambavyo siyo vya wasomi. Hivyo, kusababisha watu kuchukia kilimo, kufanya watu wachukie uvuvi na kuonekana wale wanaofanya kazi hiyo ni wale ambao wamepitwa na wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi, tumeenda sasa kila mtu anataka afanye kazi ofisini. Kila mtu anataka aendeshe gari, kila mtu anataka awe *secretary,* awe askari na hizi nafasi ni chache. Ili tuweze kutokomeza tatizo hili, lazima kwanza tufanye mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafunzo haya ya asili ya Mtanzania yafundishwe kutoka elimu ya awali, chekechea, watoto wajue kwamba kilimo ni sehemu ya kazi, na ni kazi ya heshima. Shule ya msingi yafundishwe, sekondari yafundishwe, na Vyuo Vikuu wafundishwe ili yakae kichwani wapende, hata wakitoka hawatapata shida, waendelee kulima ili tuweze kupata uzalishaji katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia ni kwa nini viwanda haviwezi kufanya vizuri katika Taifa letu? Ni kwa nini viwanda vya pamba vinavyozalisha nguo haviwezi kufanya kazi siku zote? Ni kwa nini hata alizeti haiwezi tukazalisha mafuta ya kutosheleza? Ni kwa sababu watu wamekwepa kilimo na kila mtu anataka afanye kazi za ofisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukihamasisha watu waende kwenye kilimo, watu wakaenda kwenye uvuvi, tutapata samaki wa kutosha, ambayo itakuwa ni lishe kwenye Taifa letu, lakini pia tutauza nje na kupata mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukihamasisha watu waende kwenye kilimo, tutapata mazao mengi ambayo viwanda vyetu vitapata malighafi ya kutosha ili Taifa letu liwe ni nchi ya viwanda, tuweze kusonga mbele. Kwa kufanya hivi, tutakuwa

tumetengeneza ajira kwa vijana wetu, tutakuwa tumeondokana kabisa na tatizo la ajira katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukifanya maboresho katika mfumo wa elimu, hakika tutakuwa hatuimbi tatizo la jira katika Taifa letu. Sasa ukienda katika vitu vinavyofundishwa shuleni, zipo kozi zinazofundishwa katika vyuo vyetu ambazo hata mtu hawezi kupata kazi baada ya kuwa amehitimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano, watu wengi wanahitimu ambao wamesoma mambo ya *procurement*, *marketing* na kadhalika na kadhalika, vitu ambavyo hata wakitoka pale mtu huyu hajawahi kushika jembe, mtu huyu hajawahi kushika nyavu, sasa akitoka pale anaenda ku-*market* kitu gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku moja Mheshimiwa Mbunge mwenzetu hapa alisema, watu wengi tulianza kumshangaa, lakini ukweli ni kwamba ukiangalia kwa undani vyuo vyetu vimekuwa chanzo cha kusababisha ukosefu wa ajira katika Taifa letu la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza hata vitu vinavyofundishwa katika vyuo vyetu vingi havina tija na havilengi soko halisi la ajira katika Taifa letu. Ukiangalia mfano, mtu aliyesoma *marketing* na kila mtu sasa hivi uchumi umekuwa mgumu akiwa anafanya kazi yake, anaitangaza mwenyewe kwenye vyombo vya habari. Sasa mtu aliyefanya *marketing,* anaenda kutangaza nini na vyombo vya habari vipo kila sehemu na mtu anaweza kutangaza bidhaa zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza tuangalie pia vyuo vyetu na shule zetu vitu vinavyofundishwa. Ukiangalia watu wanaohitimu katika vyuo vyetu walimu, ma-*engineer* na *professions* nyingine utaona kwamba hawana sifa zile za kufanya kazi, maana yake hawajawiva kikamilifu ambao wanaweza kwenda kuajirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana Serikali imekuja na mfumo kwamba watu wamesoma; mfano, Serikali imefundisha

walimu mpaka wamehitimu, lakini mwisho wake ili iweze kumwajiri mtu ambaye ametengenezwa na vyuo vyetu, tunaenda tena kuwataka wafanye *interview,* na wanafanya *interview* zaidi ya mbili mpaka tatu ili waweze kuajiriwa. Maana yake ni kwamba hata Serikali hatuviamini hivi vyuo vya kutosha mpaka tunaanza kusaili wahitimu wetu ili tuweze kuwapa ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa ushauri kwa Serikali, iangalie upya vyuo hivi ambavyo vinafundisha vijana wetu ambao hatimaye wanakuwa *jobless* katika mitaa yetu na katika nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Michael Kembaki, ahsante sana.

**MHE. MICHAEL M. KEMBAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate, Mheshimiwa Yahya Ally Mhata na Mheshimiwa Saasisha Elinikyo Mafuwe, ajiandae.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia kwenye hotuba ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametujalia kuwepo katika Bunge. Hili ni jambo la kumshukuru Mungu, tumekuwepo Bungeni hapa miaka mitano. Kuna wengine tulianzanao, leo hii hatukonao. Kwa hiyo, tunamshukuru Mungu sana ambaye ametuwezesha, hasa kwa kunipa nguvu kuendelea kuwatumikia wananchi wangu wa Jimbo la Kyerwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza kwa kazi kubwa, tumeona kwenye hotuba ya Waziri Mkuu, ameeleza mafanikio makubwa kwenye sekta mbalimbali. Kwa kweli kwa namna ya pekee tunampongeza sana na kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, kwani ndiye namba moja anayetupambania kutafuta fedha. Maeneo mengi tumeshuhudia miradi mingi ambayo

iliachwa na mtangulizi wake, lakini Mama huyu mpambanaji wetu amehakikisha miradi hii anaikamilisha na kuanzisha mingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda upande wa *SGR,* miradi hii ilikuwa bado haijakamilika kutoka Dar es Salaam mpaka Dodoma, lakini imekamilika na miradi hii kwa kweli imerahisisha maisha. Mtu anatoka Dar es Salaam, anakuja anaingia Bungeni, anaendelea na ratiba za Bunge, jioni akiamua anarudi Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia hata wafanyabiashara wanatoka hapa Dodoma asubuhi wanaenda Dar es Salaam wanafanya *shopping,* usiku wanarudi na kesho wanaendelea na biashara zao. Kwa hiyo, haya ni mafanikio makubwa sana kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri ambao nataka kutoa kwenye upande wa *SGR,* kuna haya mabehewa ya *VIP*, unakuta kwenye lile behewa kuna watu 20 na yale mabehewa yanabeba wakati mwingine mpaka hata watu 10. Nafikiri ni kwa sababu ya gharama kubwa za usafiri, shilingi laki moja na nusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali, kama behewa linalobeba watu 40, linabeba watu 10 au 15 mpaka 20 kwa sababu ya gharama za usafiri, kwa nini Serikali isiamue kupunguza kama ni shilingi laki moja na nusu, ikapunguza ikafanya shilingi 70,000/=? Hii inaweza ikaongeza pato kwa Serikali kuliko kuacha bei kubwa, halafu abiria wanakuwa wachache. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine tumeshuhudia mradi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere. Bwawa hili tulikuwa tunalitegemea sana, lilikuwa bado chini wakati mtangulizi wake analiacha, lakini Mama huyu amepambana na wasaidizi wake kuhakikisha linakamilika na sasa tuna uhakika wa umeme. Nchi inapokuwa na uhakika wa umeme, ninaamini viwanda vyetu vitakuwa salama, tutaongeza uzalishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya umeme tunaihitaji sana. Nitoe mfano kwa upande wa Mkoa wa Kagera, umeme umekuwa ukikatika mara kwa mara. Sasa tunao umeme wa uhakika, naomba sana Serikali iunganishe Mkoa wa Kagera na gridi ya Taifa ili nasi viwanda vyetu viwe salama, kwa sababu umeme wa Mkoa wa Kagera kwa siku moja unaweza ukakatika zaidi hata ya mara 20. Naomba sana Serikali iliangalie hili ili tuunganishwe na gridi ya Taifa pia tuweze kuongeza ajira kwa vijana wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ni mambo ambayo ni ya Kitaifa, ni mengi sana, hatuwezi kuyamaliza, lakini wasije wakasema yamefanyika ya Kitaifa tu, kwenye majimbo yetu hayajafanyika. Tumeshuhudia miradi mikubwa sana ambayo imefanyika kwenye maeneo yetu. Nitoe mfano, hakuna jambo ambalo lilikuwa linasumbua na Waheshimiwa Wabunge tumelisemea hapa Bungeni kama michango kwa wananchi wetu. Walikuwa wanapata wakati mgumu na maeneo mengine hata ndoa za wananchi wetu hazikuwa salama kwa sababu, kinapofika kipindi cha kuchangia vyumba vya madarasa, wananchi wanaume unakuta hawakai nyumbani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipindi cha Dkt. Mama Samia, mimi nieleze kwa upande wa Kyerwa, tumepata vyumba vya madarasa 185 upande wa sekondari na matundu ya vyoo 80. Ukija upande wa *primary,* tumepata vyumba vya madarasa 175 na matundu ya vyoo 829. Haya ni mafanikio makubwa, Mheshimiwa Rais ameondoa adha ambayo ilikuwa inawapata wananchi. Kwa kweli, tunamshukuru sana, ndoa za Watanzania zipo salama kwa sababu, michango haipo tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeweza kujenga Shule za Sekondari mpya 10 kwa upande wa Kyerwa. Kyerwa hatukuwa na Kidato cha Tano na Sita, lakini kipindi cha Dkt. Mama Samia tuna shule 12 za Kidato cha Tano na Sita. Kyerwa hatukuwa na *VETA,* leo hii tunajenga Chuo cha *VETA,* vijana wetu wanaenda kupata ujuzi ili waweze kujiajiri kwenye sekta mbalimbali. Kwa hiyo, haya ni mafanikio makubwa ya Mheshimiwa Rais, Mama yetu Dkt.

Samia Suluhu, tunaendelea kumshukuru sana na kumwombea kwa Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, Mheshimiwa Rais amegusa sekta nyingi, mimi nilipoingia hapa Bungeni tangu mwaka 2015 nimekuwa nikiongea habari ya soko la uhakika la zao la kahawa. Nimeongea, lakini hatukupata majibu. Awamu hii chini ya Mama yetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu, ameleta majibu ya kahawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi walikuwa wanapangiwa bei, anayeamua kununua kwa shilingi 400/= au shilingi 1,000; lakini kipindi mwaka 2022 ilibidi ifike wakati tuongee kwa ukali sana na kukataa kuunga mkono bajeti. Mheshimiwa Dkt. Mama Samia, huyu msikivu, akamwelekeza Waziri Mkuu na Waziri wa Kilimo, Kahawa ya Mkoa wa Kagera iuzwe kwenye mnada. Kahawa imetoka shilingi 1,100/=, leo hii tunaongelea shilingi 6,500/=. Haya ni mafanikio makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua kuna wengine waliokuwa wananufaika, hawapendi, na kule Kyerwa wapo. Leo hii wanapambana, wanasema, huyo ambaye ametunyang'anya kahawa tuhakikishe harudi, lakini mimi nina imani Mungu aliyeniwezesha nikapambania kahawa leo hii ikapanda, Mungu huyo huyo bado yupo kazini, na atampitisha Bilakwate. Sina mashaka na Mungu wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais amesikia kilio cha Wabunge; tumezungumza hapa juu ya miradi ya maji, wananchi hawana maji safi na salama. Mheshimiwa Rais amemwaga fedha nyingi kwenye miradi ya maji, hata Kyerwa tunayo miradi mingi inaendelea, zaidi ya shilingi bilioni 16.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoiomba sana Serikali, miradi hii imeanzishwa, lakini wakandarasi wanadai fedha nyingi. Walipeni wakandarasi ili nia ya Mheshimiwa Rais ya kuwapatia maji safi na salama Watanzania iweze kutimia. Naomba sana hili mlizingatie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninao mradi wangu wa Lunyinya – Lwabwele mpaka Chanya, unahitaji zaidi ya shilingi bilioni tatu mkandarasi akamilishe. Ninao Mradi wa Kikukuru wa shilingi bilioni tano, mkandarasi ameshaujenga zaidi ya 75%, mlipeni akamilishe mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukija upande wa barabara, mimi wakati naingia Kyerwa, barabara nyingi zilikuwa hazipitiki. Watu walikuwa wanapita kwenye mitumbwi, lakini chini ya Mheshimiwa Rais tumejenga madaraja makubwa, tumefanya kazi kubwa, Wanakerywa wanaolima wanatoka mashambani, wanapeleka mazao yao kwenye masoko, mambo yapo vizuri. Mama Samia oyee! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine kubwa ambalo amelifanya Mheshimiwa Dkt. Mama Samia, tulikuwa na masoko ya Kimataifa, masoko haya yalishasahaulika zaidi ya miaka 15. Nikamwendea Waziri wa Kilimo nikamweleza, nikamwambia haya masoko yalikuwa ni viwanda, naomba wewe ukayabebe kwa sababu yanawagusa wakulima. Akampelekea taarifa Mama Samia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mama Samia ametoa kila soko shilingi bilioni moja, leo hii tupo tunaezeka masoko Wanakyerwa na Wanakagera tunaenda kupata soko la uhakika. Hayo ni mafanikio makubwa yanayofanywa na Mama Samia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wanakyerwa wakati mama anaingia, vijiji 29 havikuwa na umeme, lakini tumempelekea maombi hapa Bungeni kupitia wasaidizi wake, Mama Samia ametoa fedha vijiji vyote 29 vina umeme. Hayo ni mafanikio makubwa ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana, Kyerwa bado tunavyo vitongoji zaidi ya 300, sasa tunaomba nguvu hiyo hiyo iliyotumika kupeleka fedha kwenye vijiji, ipelekwe kwenye vitongoji ili Watanzania na wanakyerwa waweze kupata umeme wa uhakika na vijana waweze kujiajiri kwenye maeneo

mbalimbali kwa kutumia umeme. Kwa hiyo, naomba sana hilo lizingatiwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate.

Waheshimiwa, kabla sijamtaja mchangiaji anayefuata, naomba niwatangaze wageni ambao wapo Bungeni muda huu tena.

Tuna wageni wanne wa Mheshimiwa Spika ambao ni Wanariadha walioshiriki *Bunge Marathon.* Ndugu Ian Thomas, Ndugu Ivon Alfred, Ndugu Bethasia Ledislaus na Ndugu Erick Msamila. Karibuni sana washiriki wetu wa *Marathon. (Makofi)*

Pia, tuna wageni wa Waheshimiwa Wabunge; wapo wageni 80 wa Mheshimiwa Antony Mavunde, ambaye ni Mbunge na Waziri wa Madini. Hawa ni Wawakilishi wa Wanafunzi wa Vyuo Vikuu na Vyuo vya Kati vya Jijini Dar es Salaam. Karibuni sana wanafunzi wetu. *(Makofi)*

Vilevile wapo wageni wa Mheshimiwa Balozi Liberata Lutageruka Mulamula, ambaye ni kaka yake na rafiki yake kutoka Jijini Dar es Salaam. Karibuni sana wageni wa Mheshimiwa Mulamula. *(Makofi)*

Waheshimiwa, tunaendelea na Mheshimiwa Yahya Ally Mhata. Mheshimiwa Saashisha Elinikyo Mafuwe ajiandae.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naomba nichukue nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipatia nafasi ili kutoa mchango wangu kwenye hii Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, ambaye ameniwezesha siku ya leo

nami kusimama katika hili Bunge lako Tukufu kutoa mchango wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, naomba nimshukuru sana mama yetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri anayoifanya katika nchi yetu. Mama ameonesha ushupavu, jinsi gani alivyoweza kuichukua hii nchi katika kipindi cha majonzi na kutuweka Watanzania pamoja ili kutuvusha katika hali ngumu tuliyokuwanayo. Kwa kweli, tunamshukuru sana Mama yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi ni mashahidi, miradi mingi ya kimkakati ambayo mama aliirithi kutoka kwa mtangulizi wake mingine ilikuwa ipo chini ya 50%. Leo hii Watanzania tunatembea vifua mbele, miradi yote ya kimkakati ipo katika hatua nzuri. Mradi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere leo unafanya kazi, Treni yetu ya *SGR* ilikuwa haijaanza kazi, imeanza kazi na lile Daraja la Busisi linakamilika. Kwa hiyo, miradi mingi ambayo mama aliikuta, amefanya kazi kubwa sana kuitekeleza. Kwa kweli, tunamshukuru sana Mama yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, naomba nichukue nafasi hii kumshukuru sana Waziri Mkuu, yeye ndio Msimamizi wa Shughuli zote za Serikali. Miradi yote hii ambayo mama ametoa fedha, kama tusingekuwa na Waziri Mkuu shupavu na mahiri, haya yasingefanyika. Kwa hiyo, namshukuru sana Waziri Mkuu kwa ujasiri na uhodari wake wa kuweza kusimamia shughuli mbalimbali za Serikali katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi ni mashahidi, tumemwona Waziri Mkuu mara yupo Kigoma, Bukoba, Moshi na Mtwara. Yote ni katika kusimamia shughuli mbalimbali za maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, bila kumsahau msaidizi wake, ndugu yangu Mheshimiwa Biteko, kwa kweli, tuseme kweli mnyonge mnyongeni haki yake mpeni. Ndugu yetu huyu ameonesha uzoefu mkubwa katika shughuli za utawala, na ni msimamizi mzuri. Mimi hupenda sana kusikiliza hotuba zake,

zinanifundisha mambo mengi sana. Kwa kweli ni mtu makini na anachokieleza anakitambua. Tunamshukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile, naomba niwashukuru viongozi wote wa Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa maana ya Watumishi wa Serikali ambao wameshiriki katika uandaaji wa bajeti hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kuwashukuru sana Wapigakura wa Jimbo la Nanyumbu. Jimbo langu kwa kweli wameonesha upendo mkubwa sana kwangu. Walikuwa na wasiwasi nami, lakini wasiwasi umewaondoka. Hili nataka nitoe angalizo kwa majimbo mengine, sisi wenye *style* hii, mkitupatia nafasi tunaweza. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba ndugu zangu wale ambao tulishiriki katika uchaguzi, ambao hawakubahatika, nafasi zinakuja, wachukue fomu, nina imani wananchi watawafikiria. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba sasa nichangie yafuatayo: Kama nilivyosema, namshukuru sana Rais wetu kwa kazi kubwa aliyoifanya. Ndani ya Jimbo langu la Nanyumbu, mtu aliyeondoka miaka minne nyuma akija leo atashangaa. Hataamini kama yupo ndani ya Jimbo lile ambalo lilikuwa duni sana kimaendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii ukija kwenye maji, ilikuwa ni changamoto kubwa sana ndani ya Jimbo letu. Kwa kweli, namshukuru sana Waziri mwenye dhamana na sekta hii. Ndugu yangu Mheshimiwa Aweso ni mchapakazi mzuri sana, ana msaada mkubwa sana kwa Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Aweso nilipokuwa na changamoto ya maji, anakumbuka kwenye Kata ya Maratani kuna *engineer* mmoja alikuwa anazingua pale, tulikwenda kwenye ile kata na pale pale akamshughulikia. Leo kata ile ina mradi mkubwa wa maji na unaendelea vizuri. Namshukuru sana Mheshimiwa *Eng.* Aweso. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile mama ameleta fedha ndani ya Jimbo letu, shilingi bilioni 38 ya kuvuta maji kutoka Mto Ruvuma, karibu kilometa 100 kutoka Mji wa Mangaka. Mradi huu sasa hivi una 83%. Wananchi waliopo ndani ya Jimbo langu katika Mji wa Mangaka wanategemea kupata maji muda wowote kuanzia sasa hivi kwa kweli, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu katika bajeti hii, naomba Mheshimiwa Aweso, hebu aongeze nguvu tuhakikishe maji ambayo tuliwaahidi wananchi wetu kwamba ifikapo mwezi wa Sita wataanza kupata, wayapate, kwa sababu, wananchi wana hamu ya maji na wanataka waone. Wamehangaika sana na *issue* ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, naomba nimshukuru tena Mheshimiwa Rais kwa kutuletea fedha za miradi mikubwa ya maji. Tuna mradi mkubwa wa kuchota maji kutoka Bwawa la Sengenya kupeleka katika vijiji vyote vya Kata ya Sengenya, kaleta karibu shilingi 3,600,000,000/=. Mradi unaendelea. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri wa Maji kwenye bajeti yetu hii ahakikishe ule mradi unakamilika. Mkandarasi yupo, pale kuna changamoto ya upatikanaji wa fedha. Fedha zipelekwe ili mradi ukamilike. *(Makofi)*

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

## TAARIFA

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpatie Taarifa mzungumzaji kuhusu Waziri wa Maji. Hata mimi kwangu alikuja akasimamia, akamtia pingu mkandarasi, na maji yakatoka. Usimamizi wake ni mzuri. Nilikuwa nataka kuongezea tu Mheshimiwa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ally Mhata, unaipokea Taarifa ya Mheshimiwa Amar?

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono, kwa sababu lengo ni kuleta maendeleo kwa wananchi wetu. Kwa hiyo, kwa wale watumishi ambao hawawajibiki, nami naunga mkono hoja hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna miradi mingine ya maji ambayo ipo ndani ya jimbo letu. Kila kata ya jimbo langu tuna miradi ya maji na kwa kweli, inaendelea vizuri sana. Rai yangu ni kwenye bajeti ya mwaka huu, Wizara itie jitihada ihakikishe fedha zinakwenda ili miradi hii ya maji ikamilike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiacha mradi wa maji, tunakwenda kwenye kilimo. Hapa napenda nichukue nafasi hii nimshurkuru sana Waziri Bashe, Naibu wake na wafanyakazi wote wa Wizara ya Kilimo. Mheshimiwa Bashe ameonesha uzalendo mkubwa kwenye sekta ya kilimo. Unavyomtazama Mheshimiwa Bashe, sivyo anavyofanya kazi, *the way* ambavyo Mheshimiwa Bashe anaonekana, ni tofauti na anavyofanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule kwetu sekta ya kilimo, hasa Kilimo cha Korosho, ilikuwa katika wakati mgumu sana. Watu tulikuwa tunaita shamba la bibi, watu wanajichukulia fedha, hawafanyi kazi, lakini leo hii wakulima wa Jimbo langu la Nanyumbu ukiwatajia Mheshimiwa Bashe, wanakuombea, wanasema, tunamwomba Mwenyezi Mungu aendelee kumweka huyu bwana katika sekta hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo wakulima wa jimbo langu mwaka huu wamevuna karibu tani 22,000. Ninavyozungumza, hakuna hata mkulima mmoja ambaye hajalipwa fedha zake. Jambo hili lilikuwa historia, kule zamani ingekuwa ni changamoto. Watu walikuwa wanapeleka mazao yao kwenye vyama, lakini hawalipwi. Kwa mwaka huu tunamshukuru sana Mheshimiwa Bashe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa rai yangu, naomba sana Wizara ya Kilimo, hasa kwa Mheshimiwa Bashe, pale Nanyumbu sisi ni wakulima wazuri sana wa ufuta katika Mkoa wa Mtwara, ndio tunaongoza kwenye uzalishaji wa ufuta. Tunaomba pale

pawe ndiyo *center* ya manunuzi ya zao hilo. Hatuna ofisi maalumu ya kushughulika na masuala ya manunuzi, kwa hiyo, wenzetu wa *AMCOS* na *MAMCU* wahakikishe wanatujengea jengo ili kurahisisha manunuzi, hasa ya stakabadhi ghalani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, namshukuru Mheshimiwa Bashe kwenye masuala ya kuhakikisha stakabadhi ghalani inafanya kazi 100%. Leo korosho tuwe na stakabadhi ghalani, ufuta stakabadhi ghalani na mbaazi. Mbaazi kwetu siyo mboga, ni zao la biashara. Hili Mheshimiwa Bashe amelikazania sana, leo wananchi wa Mtwara na wa jimbo langu wanapata fedha nyingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kuna zao la choroko, ninasikia wanaingiza stakabadhi ghalani. Mimi kwa mikono miwili na baraka jambo hili kwa kweli, litakuwa mkombozi kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia, nichukue nafasi hii kuwashukuru sana viongozi wa *AMCOS,* katika jimbo langu mwaka huu wamefanya kazi kubwa. Wamepokea mfumo mpya wa malipo, lakini umekuwa tayari kusimamia na kuleta tija kwa wakulima wetu. Nakipongeza Chama cha *AMCOS* cha Kata ya Nanyumbu *(Nanyumbu AMCOS)* kwa kufanya vizuri na kuweza kununua gari jipya kwa ajili ya wakulima. Ninawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua muda siyo rafiki, lakini naomba nichukue nafasi hii kuwashukuru sana Waziri wa Afya, na Waziri wa Elimu, kwa miradi mbalimbali ambayo wametuletea katika Jimbo letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ni kuhusu nishati. Leo wilaya yangu, vijiji vyote 93 vina umeme. Katika vitongoji 526, vitongoji 411 vina umeme. Namwomba Waziri ahakikishe vitongoji vilivyobaki vinapata umeme katika mwaka huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Yahya Ally Mhata, lakini kwa mujibu wa kanuni, ukipewa taarifa unatakiwa uikatae ama uipokee na siyo kuunga mkono.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa furaha niliyonayo, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Yahya, nilikuwa nakuelekeza kwenye Taarifa ya Mheshimiwa Amar.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa ya ndugu yangu, nimeipokea.

**MWENYEKITI:** Sawa ahsante, nashukuru. Tunaendelea na Mheshimiwa Saashisha Elinikyo Mafuwe na Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke ajiandae.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi nami niweze kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Namshukuru sana Mungu kwa kunipatia afya na uzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi kubwa anayoifanya kwenye nchi yetu. Kwa kweli, Mungu ametujaalia jamani, hii nchi ina viongozi mahiri. Tuna Waziri Mkuu ambaye akisimama, anachokiongea kinafanana naye. Anatusaidia, ameisimamia nchi, anamsaidia Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na safu ya mawaziri wote, wakitanguliwa na Waziri Mzee wetu Mheshimiwa Lukuvi, ambaye ni *mentor* wangu, na Naibu Mawaziri. Kipekee nampongeza sana Naibu Waziri Mkuu, Mheshimiwa Dkt. Doto Biteko. Kwa kweli wanamsaidia sana Mheshimiwa Rais. Nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nimetumwa na nitasema maneno yao walionituma. Katika Jimbo la Hai nimefanya Mkutano Mkuu wa CCM ili kusoma taarifa ya utekelezaji wa Ilani. Haya nitakayoyasema, wao ndio wamenituma. Nimefanya mkutano wa mabalozi wote wa Chama Cha Mapinduzi, wamenituma, nitasema hapa waliyoniambia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni nimekwenda kwenye kata zote 16, bado moja ambayo nitakwenda kuhitimisha Jumamosi, Kata ya Uroki. Nimefanya mikutano kusoma taarifa ya utekelezaji wa Ilani ya CCM kwenye kata hizi zote. Wanachoniambia watu wa Hai, wanasema, peleka salamu nyingi za shukrani kwa Mheshimiwa Rais. Heshima aliyotupa Mheshimiwa Rais, kazi nyingi alizofanya Jimbo la Hai, kwa kweli tunamshukuru sana sana sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wameniambia nimwambie Mheshimiwa Rais kuwa wanajua wana deni, Mheshimiwa Rais anatudai. Sisi Oktoba ninawahakikishia Waheshimiwa Wabunge wenzangu kuwa Wilaya ya Hai ndiyo itakayoongoza, mapema kabisa, kwa sababu mambo mengi Mheshimiwa Rais ametufanyia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote humu ndani ni mashahidi, nimekuwa nikiimba na Soko la Kwasadala. Leo ninavyozungumza, tayari tuna barua, TAMISEMI imeshaidhinisha, na wako kwenye mchakato wa kutangaza kwenda kujenga Soko la Kwasadala. Soko ambalo mvua ikinyesha ilikuwa ni kero, leo tumepata shilingi bilioni 11.6. Si hivyo tu, na soko ambalo ndilo linakwenda kulisha Soko la Kwasadala, ndugu yangu Mheshimiwa Bashe kaupiga mwingi sana. Tayari limeshatangazwa Soko la Mula, na kero hiyo inaondoka. Hivi kwa nini tusiseme mitano tena kwa Mama Samia? Hatuna sababu, kwa sababu kazi imefanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule kwangu shule mpya 10 na vituo vya afya nane vimejengwa. Kazi iliyofanyika ni kubwa sana. Kwa kweli sisi tunawahakikishia viongozi wetu mlioko hapa, Mawaziri, Naibu Mawaziri kwamba kazi mnayoifanya ni kubwa sana na sisi tunaendelea kuwaunga mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina jambo moja la kuchangia sasa baada ya kusema niliyotumwa. Nilikuwa nawaza hapa, wakati nasoma ukurasa wa 14 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kipengele kinachohusu uzalishaji wa ajira, nikasema, kwa kuwa na sisi tuna ndege zetu, tuna ndege za mizigo, tuna ndege za abiria, hivi kwa nini siku moja tusiitishe vijana wetu kutoka kule Hai, kutoka kule Kisima, na kwingineko, maeneo yote ya nchi yetu, tuwapakie kwenye ndege, nao tukawatafutie ajira kwenye nchi kama kule China na maeneo mengine?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii itasaidia kuimarisha diplomasia yetu kwa sababu pia diplomasia imetajwa kwenye hotuba hii. Kama hilo linawezekana, itakuwa nzuri sana, lakini kama haiwezekani, tujiulize kinachoendelea pale Kariakoo ni kitu gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tunaheshimu diplomasia, na ni kweli kwamba vipo viwanda vinajengwa na hawa wenzetu, lakini jamani ndiyo kwenda kuuza hadi madafu! Ndiyo kwenda kuuza hadi herein! Kwa hiyo, wafanyabiashara wetu pale Kariakoo na maeneo mengine, hawa wafanyabiashara walioko maeneo ya Kariakoo kutoka nchi za ugenini wanaofanya biashara ndogo ndogo, naomba sana Serikali iwatazame.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikimbie haraka kwenye eneo hili hili kwa ajili ya kuimarisha ajira. Sisi tuna maeneo ambayo tukiyagusa kule Hai mtatusaidia sana kuongeza ajira, na Mheshimiwa Bashe anisikilize.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kijiji cha Ngusero tumetenga eka 100. Pamoja na uhaba tulionao ndani ya Jimbo la Hai, tumetenga eka 100 kwa ajili ya kuanzisha bwawa ambalo Kijiji cha Ngusero pamoja na Kata za Weruweru na Rundugai zitahudimiwa na bwawa hili. Namwomba sana atenge fedha ili bwawa hili likajengwe. Amefanya kazi kubwa mno, tunajua ametuletea pale zaidi ya shilingi bilioni 19 kwa ajili ya Skimu ya Mtambo, lakini shilingi bilioni nne hapo hapo, na maeneo mengine anafanya. Najua kwamba *feasibility study* inaendelea, lakini hiki ni chanzo kipya cha kwenda kutupatia fedha nyingi kwenye kilimo biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hapo, tuna eneo la Mkalama. Nao wametenga *acre* 100 *plus*. Tazama wale watu walivyo na uchungu na uzalishaji. Ufinyu wa ardhi tulionao, Mkalama wanazo *acre* 100. Tuna chanzo kipya cha Mto Mbuguni pale. Wakichukua maji ya Mto Mbuguni wakaleta hapa, wale watu watalima kilimo ambacho kitaongeza pato lao, lakini pato la Taifa ni sambamba na ile miradi yote ya umwagiliaji mliyotuahidi ifanyiwe kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni kuhusu Kiwanda cha *Kilimanjaro Machine Tools*. Nimeshasema hapa na Serikali ilikubali, hebu tukiangalie kiwanda hiki kiweze kuzalisha. Tunaenda kwenye makaa ya mawe ya Liganga na Mchuchuma, najua wanaendelea na utaratibu wa fidia. Tuanze kukipanua kiwanda hiki ili kiweze kuzalisha chuma pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko jambo la pembejeo kwenye mikutano yangu yote niliyokwenda. Naomba pia Waziri wa Kilimo anisikilize hapa. Pembejeo wakati mwingine inachelewa, na wakati mwingine inatoka nje ya maeneo yetu. Mwananchi anayeishi kule Soni analazimika kutembea, kupanda gari, tena kipindi cha mvua, kuja kuchukua pembejeo Boma la Ng'ombe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana, tafuteni mawakala kwenye maeneo yetu ili kuruhusu wananchi wapate huduma hii kwa wakati. Pembejeo hii ya mbolea na vingine, vije kwa wakati kulingana na msimu. Tumekuwa tukisema hili mara kwa mara. Maeneo mengine wanavuna, sisi kule kwetu Hai sasa hivi ndiyo tunakwenda kuweka mbolea. Kwa hiyo, ni lazima mfanye *study,* mjue mahitaji ya pembejeo, na zije kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina jambo ambalo ni ombi kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Nafahamu kwamba uwanja wa *KIA* kulikuwa na mgogoro kati ya wananchi wa *KIA,* Rundugai, na maeneo mengine. Sasa hivi mgogoro umekwisha na watu wamelipwa fidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo maeneo ambayo ndiyo yaliyokuwa yanategemewa kwa ajili ya uchumi wa Jimbo la Hai.

Wananchi wa Rundugai, wananchi wa *KIA* na maeneo mengine yanayozunguka hapo; leo wananchi wale wameondolewa, hawaruhusiwi kulima kwenye yale maeneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaelewa kwamba ni kweli ni maeneo ya uwanja wa ndege, lakini tunaomba turuhusiwe tulime kwa msimu, hata kwa kupewa mkataba kama ambavyo tunatumia mashamba yale ya *Kilimanjaro Machine Tools*, ya *NDC;* wananchi huwa wanapewa mkataba wanalima na awamu ikiisha wanapewa tena, tukiwa tunajua kwamba ni mashamba ya *NDC*. Ifanyike hivyo kwenye mashamba haya ya Kilimanjaro, Kiwanja cha Ndege cha *KIA*, ili wananchi waweze kupata. Kwa sababu eneo la Rundugai sasa hivi msimu huu, wananchi hawajalima. Kwa hiyo, Mheshimiwa Bashe ajiandae kutuletea chakula cha msaada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale *KIA* hawajalima. Mbaya zaidi, hata mifugo inapoingia kule inazuiliwa. Tunafahamu kwamba tunahitaji uwanja wa ndege na tunaheshimu sana, lakini turuhusiwe mifugo iweze kupata chakula. Maeneo yale yako pembezoni sana, hekta zaidi ya 11,000, na wala huwezi kuona hata uwanja wa ndege uko wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yale maeneo ya pembezoni turuhusiwe watu walime kwa utaratibu maalumu kama ambavyo tulishirikiana wakati wa mchakato wa fidia, nami kama Mbunge nitasimama kuongeza jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni kuhusu pensheni ya watumishi. Watumishi wanaomaliza vyuo vikuu kwa kweli walilipwa awamu ya nyuma kabla ya *formula* ya kikokotoo kipya. Wapo Maprofesa wamestaafu leo wanalipwa shilingi 80,000/= na shilingi 100,000/=; wale watumishi ambao walilitumikia Taifa hili na ambao pensheni yao bado iko chini, nawaomba sana, wangeneze *data base* ya wazee hawa. Wengi wako huko *frustrated* kwa sababu ya mazingira na pensheni na *formular* ambazo ziliwaumiza. Angalieni namna ya kuhuisha hili jambo ili liweze kufanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana watumishi wakiongozwa na Mkuu wangu wa Wilaya, Mkuu wa Wilaya mahiri kabisa, Mheshimiwa Hassan Bomboko na watumishi wote Wilaya ya Hai, namna ambavyo wakipokea fedha zinazopelekwa na Bunge wanafanya kazi zao kwa uaminifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naendelea kuomba, tazameni maslahi ya Watendaji wa Vijiji, na Wenyeviti wa Vijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Saashisha Mafuwe. Nilimtaja Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza kabisa, namshukuru Mwenyezi Mungu, Mwenye wingi wa Rehema kwa kunijaalia afya na kunipa kibali cha kusimama ndani ya Bunge lako Tukufu. Ninaanza kabisa kwa kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niungane na wenzangu kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri. Nampongeza Mheshimiwa Lukuvi na Naibu wake Mheshimiwa Ummy Nderiananga kwa kazi nzuri wanayoifanya. Pia nampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu, Mawaziri pamoja na Naibu Mawaziri, kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuitekeleza Ilani ya CCM. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kwa moyo wa dhati kabisa kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanya ya kuwatumikia Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, pongezi nyingine ziende kwa Makamu wake wa Rais, Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango kwa kazi kubwa anayoifanya kwa kushirikiana na Mheshimiwa Rais, kwa kuwatumikia Watanzania. Nawapongeza sana na Mwenyezi

Mungu aendelee kuwajaalia afya ili waendelee kuwatumikia Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imefanya kazi kubwa katika nchi yetu. Imefanya kazi kwenye ujenzi wa barabara nchi nzima. Naomba niseme mafanikio yaliyopatikana ndani ya Mkoa wa Kigoma. Serikali imetujengea barabara ya kutoka Kabingo – Kibondo – Kasulu – Buhigwe, kilometa 260, na barabara hii inaelekea kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, kuna barabara ya kutoka Kazilambwa – Chagu – Uvinza. Barabara hiyo nayo iko katika hatua za mwisho, inakaribia kukamilika. Kwa kweli ni jambo la kumshukuru Mwenyezi Mungu. Sisi watu wa Kigoma tulikuwa na shida ya Barabara, lakini muda siyo mrefu kilio hicho cha barabara kitasahaulika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndani ya Mkoa wa Kigoma, tumeweza kupata umeme wa gridi ya Taifa. Tayari tumeshapata umeme kutoka Nyakanazi, na Kituo cha Kupoozea Umeme cha Kidahwe kilizinduliwa mwaka 2024 na Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango, Makamu wa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea kuishukuru Serikali kuhusu suala la maji. Maeneo mengi kilio hicho cha maji kinaendelea kupungua. Suala la maji halijakamilika kabisa katika maeneo mengi, lakini kwa kiasi kikubwa Serikali imejitahidi, maeneo mengi wananchi wanapata maji. Ninaamini itaendelea kufanya kazi ili ieweze kukamilisha miradi yote ya maji, kusudi wananchi waondokane na tatizo la maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Serikali, kwani Mkoa wa Kigoma tumepata Chuo Kikuu cha Afya ya Sayansi kwa ajili ya madaktari na wauguzi. Chuo hicho kinaendelea kujengwa. Pia, Uwanja wa Ndege wa Kigoma unaendelea kujengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Kigoma ni lango kuu la biashara. Tunaamini Uwanja wa Ndege wa Kigoma utakapokamilika, ndege zitaweza kutua usiku na mchana

kwenda maeneo mbalimbali. Kwa hiyo, wafanyabiashara kutoka maeneo mbalimbali wataingia Kigoma na wataweza kufanya biashara, kwa sababu utakuwepo usafiri wa kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Awamu ya Sita imesaini mkataba wa kujenga *SGR* kutoka Uvinza kwenda Msongati – Burundi. Reli hiyo ikikamilika, tunaamini kilio cha ubebaji wa mizigo kutoka Dar es Salaam kwenda Kigoma na kuvusha nchi ya Kongo kitakuwa kimekwisha. Ni mambo mengi yamefanywa ndani ya Mkoa wa Kigoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumejengewa hospitali za wilaya. Hospitali ya Kakonko, Hospitali ya *Kasulu DC,* na Buhigwe zimekamilika. Vituo vingi vya afya vimejengwa na vingine vimekarabatiwa sambamba na zahanati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli tuna kila sababu ya kumshukuru Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa aliyoifanya ndani ya Mkoa wa Kigoma. Mwenyezi Mungu amjaalie, nasi tunaahidi itakapofika Oktoba, tutamlipa yaliyo mema kwa kumpigia kura nyingi. Kura za Kigoma hazina wasiwasi, tutampigia kura nyingi kwa sababu ameufungua Mkoa wetu wa Kigoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee kuzungumzia kuhusu kilimo. Nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, amefanya kazi kubwa ya kuhamasisha kilimo cha mchikichi Mkoani Kigoma. Naomba sasa, Serikali iweze kujenga viwanda vya kuchakata zao la mchikichi ili tuweze kupata mafuta yaliyo bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kilimo, hapa pia naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Bashe. Mheshimiwa Bashe tunamshukuru, kwani tangu ameingia Wizara ya Kilimo suala la mbolea ni historia. Tunamshukuru sana na Mwenyezi Mungu amjaalie. Kwa kweli tangu mwaka 2024 kilio cha mbolea kwa wananchi hakipo. Tunaishukuru Serikali kwa kuwapatia ruzuku kwa ajili ya mbolea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi watu wa Kigoma tunalima zao la muhogo, mahindi, na maharagwe. Naiomba sana Serikali iweze kutusaidia, wananchi wameitikia wito wa kulima kilimo cha muhogo, lakini hawana soko kwa sababu soko la muhogo limeanguka. Kwa sasa kilo moja ni shilingi 300 kutoka shilingi 1,000. Tunaomba Mheshimiwa Bashe atusaidie sana kututafutia namna ya kupata ufumbuzi wa soko kwa ajili ya zao la muhogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie kuhusu migogoro ya ardhi. Maeneo mengi kuna migogoro ya ardhi baina ya watu wa hifadhi na wananchi. Naomba Serikali inapokuwa inakwenda kupima mipaka iwashirikishe wananchi. Ikiwashirikisha wananchi kupitia viongozi wao wa vijiji, migogoro hii itapungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi kuna sintofahamu kati ya watu wa hifadhi na wakulima kwa sababu mipaka haionyeshi ni wapi inaishia? Kwa hiyo, naiomba Serikali iendelee na upimaji wa ardhi na kuweka *beacon* ili wananchi wajue wanaishia wapi na hifadhi nao wajue wanaishia wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee tu kuwaomba watu wa hifadhi kwamba wasitumie nguvu, wawaelimishe wananchi. Wananchi ni waelewa, ukiwaelemisha taratibu, wanaelewa kuliko kugombana, na wakati mwingine haileti afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule kwetu Kasulu eneo la Makere Kusini kuna mgogoro mkubwa baina ya wananchi na watu wa hifadhi. Naiomba Serikali iendelee na upimaji wa ardhi. Vipo vijiji vya Kabulanzwili ambako kuna tatizo kubwa la mwekezaji pamoja na wananchi. Naomba Serikali iendelee na upimaji wa ardhi ili wananchi waweze kuwa huru wanapokuwa wanaenda kulima mashamba yao. Siyo wanaanza kulima, halafu wanafukuzwa kwamba eneo hili siyo la kwao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, kilio hicho kipo katika Kata ya Kigembe na Kata ya Lusesa katika Vijiji vya Kacheli na Lugufu pamoja na Kigembe. Kwa hiyo, naiomba Serikali ipime ardhi kwa kuwashirikisha wananchi ili kuondoa sintofahamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, naomba kuzungumzia kuhusu UKIMWI. UKIMWI upo, wananchi waendelee kupima na wakigundulika kwamba wana UKIMWI waweze kutumia dawa za kufubaza UKIMWI ili waendelee na maisha yao ya kawaida ya uzalishaji mali na kuendelea kutunza familia zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema maneno hayo, nakushukuru, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Josephine Genzabuke. Huyu ni mchangiaji wetu wa mwisho kwa mchana huu. Nitawataja wale wachangiaji ambao wataanza kuchangia jioni ya leo.

Tutaanza na Mheshimiwa Zuena Athumani Bushiri, Mheshimiwa Sebastian Simon Kapufi, Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay, Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga, Mheshimiwa Mary Francis Masanja, Mheshimiwa Livingston Lusinde, na wengine wataendelea baadaye.

Baada ya kusema hayo, nawatakia mchana mwema, na ninasitisha shughuli za Bunge hadi saa kumi na moja kamili jioni.

*(Saa 6.57 Mchana Bunge liliahirishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)*

*Mwenyekiti (Mhe. Deodatus P. Mwanyika) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. AZIZA MAKWAI – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Namwita sasa Sebastian Simon Kapufi, atafuatiwa na Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay, Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga, ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Awali ya yote, naomba nianze kwa kuunga mkono hoja na niipongeze Ofisi ya Waziri Mkuu kwa ujumla wake, nimeipitia bajeti yote na nimeona imesheheni maeneo tofauti tofauti ambayo yanaeleza utekelezaji wa ilani ya chama chetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze na suala linalogusa idadi ya watu. Kwa idadi ya Watanzania ambao ni takribani milioni 60, 60% ni vijana ambao wapo chini ya umri wa miaka 25 na karibia 32% ni vijana wa kati ya miaka 10 na 24. Kuwa na idadi kubwa ya watu inaweza ikawa ni faida au ikawa ni balaa, itategemea. Unapokuwa na timu kubwa ya watu ambao ni tegemezi na wachache ndio wanaoshiriki kujenga uchumi wa nchi, taabu ndiyo inaanzia hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinyume chake, ukiwa na idadi kubwa na hasa vijana ambao ni nguvu kazi, wakitumika vizuri ni msaada kwa Taifa, lakini wakikutana na changamoto nao wakawa ni tegemezi, wakahitaji mahitaji makubwa ikiwa ni pamoja na ajira, hilo linakuwa ni bomu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nikiyasema hayo natamani kuendelea kusema kama nchi, na hapa bahati nzuri nina mkakati wa utekelezaji wa Sera ya Taifa Maendeleo ya Vijana ya mwaka 2007, lakini pia ninayo Sera ya Taifa ya

Maendeleo ya Vijana ya mwaka 2007. Hizi zote zimesheheni namna ya kuwafanya vijana wasiwe tegemezi, namna ya kuwasaidia vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba katika hilo, Ofisi ya Waziri Mkuu ina nafasi kubwa ya kuwasaidia vijana, ikiwa ni pamoja na madirisha mbalimbali, iwe ni mikopo, achilia mikopo ile ya 10% kwa maana ya *four, four, two* lakini pia na zile fursa nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzangu wazungumzaji wa mwanzo waliendelea kuishauri Serikali, yawezekana fursa hizi wengi wasizifahamu, kwa hiyo, wakati umefika sasa watu hawa waendelee kupewa nafasi ya kuyafahamu madirisha hayo ya kuzifukuzia hizo fursa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwapongeze wadau mbalimbali wanaosaidiana na Serikali katika kuwanusuru vijana. Nimebahatika kushiriki semina mbalimbali zilizokuwa zikiendeshwa na *NGO's* na watu wengine wa namna hiyo. Rai yangu kama ambavyo huko nyuma Serikali imewahi kushauri, hatukatai ushiriki wao, lakini ni pamoja na kuendelea kuwasisitiza waheshimu taratibu, kanuni na sheria, lakini ni wadau muhimu sana katika suala zima la maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimezungumzia Sera ya Taifa ya Vijana na fursa nzima ya mikopo. Nimelisema hilo kwa sababu gani? Ukizungumzia vijana ambao nimekwambia 60% wapo chini ya miaka 25, imenifanya niende kwenye sekta muhimu ya madini. Bahati nzuri nami ninajihusisha na shughuli ya madini na ninapata faida huko, ninalo la kusema katika hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa siku za hivi karibuni, hatukatai tumeendelea kupata wadau mbalimbali ambao wamejielekeza katika suala la uchimbaji wa madini, lakini tatizo ninaloliona kama Serikali, haitaingilia kati kuona namna nzuri kwa sababu taratibu zipo na bahati nzuri hapa nazungumza kwa Ofisi ya Waziri Mkuu, taratibu zipo, lakini sasa hivi kinachojitokeza, vijana hawa ambao nimesema, wasiposhikiliwa vizuri ni bomu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapokuta wengi wamejiajiri katika eneo la uchimbaji kama wachimbaji wadogo, lakini maeneo ambapo wamekuwa wakifanya shughuli zao za kila siku, sasa hivi maeneo hayo kwa namna moja au nyingine ni kama yamevamiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatukatai mtu mmoja mmoja anaweza akauza, lakini namna ya uuzaji ndiyo hapo ambapo nashauri Serikali itusaidie kwa sababu ni maeneo ambayo unaweza ukakuta yamekuwa yakishughulikia vijana wengi, lakini anatokea labda mwekezaji mmoja, na ukumbuke ni maeneo tumesema ya wachimbaji wadogo wadogo. Kwa namna nyingine yoyote ile anaingia mlango wa nyuma, anafanya ubia na baadhi ya wachimbaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa utakuta maeneo ambayo yalikuwa ya wasaidie wachimbaji wadogo wadogo ambao ni vijana hawa ambao nisema kwamba wasipopewa shughuli ya kufanya itakuwa ni tatizo, sasa hata kama ni maeneo ambayo yamekuwa yakiajiri vijana wengi yameanza kupotea. Hapo ndipo ninapoona ni tatizo kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikitoka hapo, naipongeza Serikali, mara ya mwisho mimi kwa kupitia Kamati yangu ya TAMISEMI tulipita tukaona suala la shule za wasichana, na kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, amesema shule za wasichana 26 za Sayansi zimejengwa. Rai yangu, shule hizo ni nzuri, lakini kwa maana tunazungumzia sayansi kama maabara hazitofanya kazi kama hawatoshiriki kwa vitendo, tafsiri nzima ya kuwa na shule za sayansi inapoteza maana. Kwa hiyo, naomba hilo lizingatiwe pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye huduma ya makundi maalumu nashukuru. Dira ya maendeleo niendelee kuishukuru. Nizungumzie habari ya urejeshaji wa miundombinu iliyoharibika kwa maana ya miradi ya dharura. Bahati nzuri hili limegusiwa na hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, nchi hii yote kwa ujumla wake eneo hili mimi ninaweza nikakwambia kwa mfano kule

kwangu yapo maeneo yana miradi mikubwa, mradi wa umwagiliaji wa takribani shilingi bilioni 31.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo hayo kama miundombinu imeharibika, yasipoweza kufikiwa, hata tafsiri ya ule mradi mkubwa inapoteza maana. Kwa hiyo, nilikuwa naomba sana, miradi ni mikubwa, miradi ni mingi, imetapakaa kila sehemu na ndiyo maana tulikuwa tunasema hata kama ni wenzetu wa *TARURA* waendelee kuangaliwa kwa maana ya fedha ili kunusuru maeneo haya ambayo yanaenda moja kwa moja kushiriki suala la maendeleo yetu na uchumi wetu kwa ujumla wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiyasema hayo, najua suala zima la madaktari bingwa na huduma hizo za kibingwa, mimi naipongeza Serikali, lakini kwenye hili naomba twende mbali zaidi. Wakati huduma hiyo ikiendelea kuimarishwa kwa sura hiyo, basi tuione ije katika sura ya utalii wa kimatibabu (utalii wa tiba), kwa maana ya hospitali mbalimbali ikiwa ni pamoja na hospitali yetu ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tu-*take advantage* ya hilo kwamba wakati Serikali imefanya vizuri kuhakikisha huduma hizi zimeboreshwa kwa kiwango chake, kama ambavyo sisi Watanzania tumekuwa tukisafiri hapa kwenda China, India, au *South Africa* tutumie nafasi hiyo hiyo ya kuhakikisha kwamba hilo linakuwa ni fursa au ni dirisha la kufanya utalii huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hiyo haitoshi, kwa nchi yetu hii njema wakati tunaendelea kuhubiri kuboresha utalii, yupo mtalii anayeweza akashindwa kufika nchini akiwa hana uhakika wa matibabu, sasa wakati sehemu hiyo ya tiba imeendelea kuimarika kwa kiasi hicho, mimi niseme inakuwa ni nafasi pia ya kuchochea hizo fursa nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami katika eneo hilo nisisite kuishukuru Serikali kwa…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa muda, na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Sebastian Kapufi. Kabla hujasimama Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay, namwomba Mheshimiwa Zuena Bushiri achangie, ana *special case*. Mheshimiwa Zuena, endelea.

**MHE. ZUENA A. BUSHIRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi nami nichangie bajeti hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya kwa kuifungua nchi yetu kwa miradi mingi sana nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma. Tumezunguka kukagua miradi mingi sana, miradi ya kimkakati kama Mradi wa *CAG*, Daraja la Busisi, Bwawa la Mwalimu Nyerere pamoja na miradi mingine mingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Mawaziri wenzake wote kwa kazi nzuri wanazozifanya katika kuhakikisha kwamba wanamsaidia Mheshimiwa Rais katika utekelezaji wake wa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, nampongeza Mheshimiwa Spika wetu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Naibu Spika na wenyeviti wote kwa jinsi mnavyoliongoza Bunge vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaongelea Mkoa wangu wa Kilimanjaro. Mkoa wetu wa Kilimanjaro sisi tumepata fedha shilingi trilioni 1.2. Fedha hizi zinatekeleza miradi 2,345 ikiwemo miradi ya maji, miradi ya miundombinu na miradi mingine mingi. Haijawahi kutokea katika Mkoa wa Kilimanjaro kupata fedha nyingi sana za miradi ya maendeleo kama kipindi hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi hii imegusa katika maeneo mengi kuanzia ngazi ya matawi, kata, wilaya, na mkoa. Kwa kweli tunamwambia Mama, tunashukuru sana, Kilimanjaro tupo pamoja naye na atatuona kwa kuwa sisi tumemshukuru kiasi kikubwa, tutamlipa deni lake ifikapo Oktoba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaanza na mradi wa maji wa Same - Mwanga na Korogwe. Ni hivi juzi tu ambapo Mheshimiwa Rais alikuja kuzindua mradi ule. Huu ni mradi ambao umewakwamua wananchi wa Same na Mwanga kwa tatizo la maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika kwamba mradi huu ulikuwa unasuasua siku nyingi sana, lakini mama kwa jinsi anavyomjali mwanamke, ameupigania mpaka leo mradi huu umefunguka na tumeanza kupata maji. Pongezi sana kwa Mheshimiwa Rais. Niseme neno moja tu, chanzo cha maji haya ya mradi huu kinatoka kwenye Ziwa Jipe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ziwa Jipe lina changamoto ya magugu, nilishaliongelea tena katika Bunge lako hili. Kutokana na changamoto hiyo ya magugu yanavyoendelea kuwa mengi, inaonekana, baada ya muda, maji yatakuwa kidogo. Naiomba Serikali ya Chama cha Mapinduzi kupitia Mheshimiwa Rais ihakikishe inatoa magugu yale ili zoezi la mradi huu liwe endelevu bila kukwama mahali popote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee kuhusu mikopo ya wanawake. Kwanza nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuruhusu mikopo ya 10% (4:4:2). Mikopo hii inakwamua wananchi kiuchumi hasa akina mama wahangaikaji. Katika Manispaa yetu ya Moshi tumepata vikundi 32 ambavyo tayari vimeshakopeshwa, imetoka shilingi bilioni 1.171. Tunampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kuwa sasa hivi wananwake wa Kilimanjaro, wafanyabiashara wakubwa, nadhani mnatuona pale tumebeba ndoo za maparachichi, vitunguu maji, tumebeba kila kitu sisi tunauza, tunachotaka ni pesa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wanawake kwa kupata mitaji hii, wanajikwamua kiuchumi. Naomba sasa Maafisa Maendeleo ya Jamii wawasaidie wale akina mama wa chini ambao hawawezi kujaza vizuri ule mfumo, inawachukua muda mrefu sana ili kukamilisha utaratibu mzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhusu afya, na niongelee Hospitali ya Rufaa ya *KCMC*. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kujenga jengo la mionzi. Wagonjwa wetu wote wa Kanda ya Kaskazini na jirani wakipata matatizo ya mionzi ni lazima waende *Ocean Road,* lakini sasa hivi jengo hili limejengwa kwa shilingi bilioni 5.3 na limefikia 94.5%, kilichobakia pale ni vifaa ambavyo vinatakiwa viingie ili kazi ianze. Wananchi wa Kilimanjaro na wananchi wa mikoa jirani kwa maana ya Kanda ya Kaskazini pamoja na nchi jirani ya Kenya, nadhani watakuwa wametoka katika matatizo hayo ya kwenda *Ocean Road*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya afya, nitarudi tena katika Hospitali yetu ya Rufaa ya Mawenzi. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais, tena sana, kwani ametusaidia sisi akina mama kwa kuhakikisha amekamilisha kwa 88% jengo la mama na mtoto. Hapo zamani ulikuwa ukienda Mawenzi unakuta kitanda kimoja, wamelala wanawake watatu na watoto wao. Sasa hivi japo halijakamilika lote, lakini hali inaridhisha kwa akina mama kulazwa katika wodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jengo hili likikamilika kwa sababu sasa hivi sakafu ya chini inafanya kazi, ghorofa ya kwanza inafanya kazi, bado ghorofa ya pili na ghorofa ya tatu, ikikamilika wananchi watafurahia huduma hiyo ambayo itawasaidia sana na ninadhani kila mwanamke atataka kujifungua sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu, Kilimanjaro sisi Mama hatudai. Tuna deni la Mheshimiwa Rais, na deni letu tutalilipa ifikapo Oktoba katika sanduku la kura. Tunamwombea kwa Mungu, Mwenyezi Mungu ampe afya njema, ampe maisha marefu tukutane siku hiyo ndiyo atajua kwamba Kilimanjaro ametugusa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, niseme ahsante sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zuena kabla hujakaa, tuweke rekodi zetu vizuri. Hapa kuna mahali ulisema Mradi wa *CAG*, nadhani ulimaanisha Mradi wa *SGR*.

**MHE. ZUENA A. BUSHIRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa ni *SGR* nisamehe katika hilo. *(Kicheko/Makofi)*

**MWENYEKITI:** Haya ahsante. Nimwite sasa Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay, atafuatiwa na Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga, Mheshimiwa Livingstone Lusinde, ajiandae.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Kwanza nichukue nafasi hii kuungana na Wabunge wenzangu wote kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema aliyetujalia wakati huu muhimu na nafasi hii muhimu ya kipekee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee, pia naipongeza na kuishukuru sana Serikali yangu kwa kazi kubwa iliyofanyika kote nchi nzima na hasa Jimbo la Mbulu Mjini. Sisi Kamati ya TAMISEMI tumetembea karibu mikoa yote, na kazi kubwa imefanyika. Naipongeza pia Ofisi ya Waziri Mkuu na Wizara, Idara mbalimbali zilizopo chini yake pamoja na Baraza zima la Mawaziri kwa kazi kubwa iliyofanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nichukue nafasi hii kutoa mchango kwa baadhi ya maeneo. Kazi kubwa imefanyika. Eneo la kwanza ni eneo la pembejeo kwenye kilimo. Kuhusu pembejeo ya ruzuku, tunaiomba sana Serikali ije kwa wakati na kwa aina mbalimbali kwa kadiri ya mahitaji ya wananchi na wakulima kote nchini. Eneo hili tukiboresha, tutakuza uchumi wa wananchi, lakini pia kilimo chenye tija kwa kila mwananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kadiri tunavyofahamu, Watanzania walio wengi ni wakulima na eneo hili mara nyingi tumeboresha, na kazi kubwa imefanyika. Ushauri wangu ni

kwamba, pembejeo ziletwe kwa wakati, na pia vile vifungashio vya kilo 25 kwenye mbolea ni vya muhimu sana kwa ajili ya uwezo wa wananchi na wakulima wetu, lakini pia ngazi za kata kuwa na mawakala kwa ajili ya kurahisisha upatikanaji na ufikaji kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine kwenye kilimo ni Jenga Kesho iliyo Bora, *(BBT)*. Ni kwamba tumewekeza, na tunataka kuona matokeo na tulitarajia kwa sasa tunafika kwenye ngazi nyingine za halmashauri baada ya *center* kuboreka na vituo tulivyoanzisha. Eneo hili ni eneo lenye tija sana kwa sababu linagusa sekta hiyo ya kilimo. Kwa sasa tufanye tathmini ya Jenga Kesho iliyo Bora kwenye kilimo na namna gani tunaondoa vikwazo vilivyopo na namna ya maboresho zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na muda, eneo hili tukifanyia kazi, tukaleta matawi kwenye halmashauri zetu, na kwenye wilaya, itasaidia sana kwa sababu ya kupanua wigo, lakini kwa manufaa zaidi kwa Watanzania hasa kundi hili la vijana na wakulima wenye nia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni ujenzi wa Vyuo vya *VETA*. Tulijenga *VETA* kwenye halmashauri nyingi, tunaipongeza sana Serikali. Sisi ambao hatukupata fursa hii, tulipoambiwa *FDS* zetu kwa maana ya vyuo vya maendeleo ya wananchi, vitakuwa *VETA B,* bado tunahitaji maboresho kwa ajili ya kukamilisha kwanza ujenzi ule wa miundombinu, lakini kuboresha mitaala na mwisho wa yote kuleta tija ili mwanafunzi wa vyuo vya maendeleo ya wananchi awe ni sawa na yule wa *VETA* katika taaluma wanayoipokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni miradi ya Barabara. Eneo hili tumeumia sana. Naishukuru Serikali, japo tulipata wakati mgumu sana kule Mbulu Mjini na Mbulu Vijiji. Barabara ya Mbulu - Garbabi ambayo imekwama muda mrefu, walau Serikali imeanza kuchukua hatua za kutafuta fedha na kuweza kunusuru hiyo hali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani hao wakandarasi tunaowapa kazi, pia kama tatizo ni malipo ya awali, basi

tutazame eneo la kuboresha sheria zetu na malipo yale ya awali ili tukishawalipa wale kwa namna ya pekee, basi kazi ifanyike kwa wakati kuliko mradi mdogo wa kilometa 25 unakwama kwa miaka mitatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo hili nilifikiri ni Mbulu tu, kumbe nilipoenda Singida pia wamekwama kilometa 25. Kule Lindi wamekwama kilometa 25, maeneo kadhaa wamekwama kilometa 25, miradi imesimama muda mrefu. Ombi langu kwa Serikali ni kwamba itazame utaratibu wa namna ya kuingia mikataba na namna ya kulipa fedha za awali ili walau miradi inayoanza ipatikane kwa wakati na gharama za ucheleweshaji na gharama mbalimbali tuweze kuepuka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaipongeza Ofisi ya Waziri Mkuu pia kwa mikopo ya vijana. Huu mradi wa mikopo ya vijana kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu bado haujaeleweka vijijini. Vijana wengi hawapo kwenye mtandao, vijana wengi hawaelewi hii ni fursa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kama inawezekana, kuwe na *forum* kwa maafisa vijana katika halmashauri yetu, lakini na vipindi maalumu vya vyombo vya uhabarishaji kwa maana ya *media* mbalimbali ili vijana wetu wengi wafahamu suala hili la mikopo Ofisi ya Waziri Mkuu, na kwa sababu fedha zile ni nyingi na zinasaidia vijana ili waweze kunufaika kwa namna inayowezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha za *TARURA,* kuna mradi upo Jimboni Mbulu na maeneo mengine tumekuta tulipokwenda Shinyanga. Tunaiomba Serikali itazame utaratibu wa kuboresha fedha za *TARURA* namna ya kuongeza fungu kwa fedha za *TARURA*. Fedha za Mfuko wa Jimbo ni karibu miaka miwili zimeyumba. Tunaomba fedha za Mfuko wa Jimbo zitolewe, kuna mradi umekwama sana kule Mbulu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri Mchengerwa, walau yule mkandarasi wa Mbulu Mjini amepewa fedha juzi, lakini hatua hii imechelewa sana kwa zaidi ya mwaka,

na ni mita 600 tu pamoja na daraja hapo Katikati, lakini wananchi wamepata adha kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, japokuwa Serikali tayari imechukua hatua, tunaipongeza Serikali, lakini tutazame maboresho zaidi ili kuokoa hali hii inapotokea wakati fulani fulani. Fedha hizi za tozo na Mfuko wa Jimbo ndiyo fedha zinazotusaidia sana sisi Wabunge wa Majimbo kwa sababu tunapotembea walau wananchi wanatuomba ahadi mbalimbali, lakini kwa namna ya pekee zinatutatulia kero kwa wananchi wetu. Tumeongeza barabara nyingi sana kupitia *TARURA* fedha za *TARURA* kwa sasa hazitoshi. Tunaiomba sana Serikali itazame upya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni mafao ya wastaafu. Tunaipongeza Serikali, kwa mafao ya wastaafu wale waliokuwa wanalalamikia kikokotoo, Serikali imesikia, tunampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kilio kile kusikika, lakini pia kuboresha. Eneo hili la wastaafu wale wa zamani wanalipwa shilingi laki moja na kitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hali ya kawaida, shilingi laki moja na kitu au shilingi laki moja, haimsaidii yule mstaafu. Kwa hiyo basi, tulikuwa tunaomba kama inawezekana, Serikali itusaidie. Hawa ni wastaafu wazee waliotumikia Taifa hili, na bado wanaiomba Serikali yao iwaone kwa jicho la pekee ili mafao yao ya yaweze kuangaliwa na yaboreshwe kulingana na hali ya sasa, kwani nao wanakabiliwa na changamoto lukuki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni malipo ya viongozi wa Serikali za Mitaa. Wenyeviti wa Mitaa na Wenyeviti wa Vijiji tumewatumia muda mrefu. Hawa viongozi wameomba sana, wameikumbusha sana Serikali, tumezungumza kwenye vikao, Waheshimiwa Madiwani wote hao ni nguzo muhimu katika Serikali yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka huu wa fedha kupitia bajeti zetu hizi, tuendelee kuona eneo hili ni la umuhimu mkubwa wa kuweza kuongeza fedha na walau wapewe hata kama ni kidogo ili wajisikie nao ni sehemu ya viongozi wa

kuchaguliwa. Vilevile, kila kinachofanyika, humkosi Mwenyekiti wa Mtaa, humkosi Diwani, na wote hawa wanaunga mkono juhudi za Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ajira na usaili kwa vijana, sisi tunaokaa na wananchi wachaguliwa, tunasikia mambo mengi sana. Eneo hili la usaili limelalamikiwa sana na vijana nchini. Eneo hili litazamwe upya, kwani eneo hili linaliliwa, eneo hili limeumiza, familia wamekata tamaa kusomesha vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee, tunaomba Serikali itazame utaratibu mzuri ambao hauleti manung'uniko lakini pia kwa kuwa wao walishasoma wakapewa vyeti, eneo hili lisiwe kigezo kikubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha mwalimu mwanafunzi anafundisha shule jirani, anakaa miaka mitatu kwenye kufundisha anafaulisha vizuri, lakini kwenye usaili hajafanikiwa. Yule aliyepo kijiweni yawezekana Mungu amemsaidia, amefaulu, lakini kwa namna ya pekee unakuta yule kijana aliyeajiriwa hakuwa ametoa hata uzalendo wa kusaidia kizazi cha hao vijana waliopo shuleni, na kwa namna ya pekee tunakatisha tamaa hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu tutazame vijana hawa wengi waliopo kwenye kujitolea. Je, leo wakiondoka kwenye nafasi za kujitolea, kwa nafasi hizo tutakuwa tumepata pengo kiasi gani? Kwa namna ya pekee, ili walau tuongeze jitihada za uzalendo wa watu kutumikia bila kujali anapewa nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, nashukuru. Kutokana na mambo mengi niliyonayo, nitachangia kwa maandishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana kwa nafasi hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Issaay. Nilimwita Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga, atafutiwa na

Mheshimiwa Livingstone Joseph Lusinde na Mheshimiwa Mary Francis Masanja, ajiandae.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi. Maana ni bahati iliyo njema kupata nafasi jioni hii kuchangia katika hotuba ya bajeti ya Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, na wenzangu wengi hapa wameshachangia mambo mengi makubwa kudhihirisha kwamba Serikali ya Chama cha Mapunduzi ipo kazini na inaendelea kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huko nje naona kuna baadhi ya watu wachache wanafikiri Wabunge wa CCM kazi yao ni kusifia, lakini tunasifia kutokana na yaliyotokea na kutendeka. Wabunge tuna akili timamu, na kama sisi ni waongo, ina maana wananchi wetu watatukuhumu. Mimi nasifia hapa kwamba Serikali imefanya mambo makubwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amefanya mambo makubwa, na nitayataja. Kama nasema uongo, wananchi kule watanijua kwamba huyu Mbunge amesema jambo hili lipo hapa, wakati halipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunataka kuwapa moyo wananchi waendelee kutuelewa ambavyo tunavyopongeza Serikali yetu kwa sababu ni Serikali ya Chama cha Mapinduzi, ipo madarakani chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na Mawaziri wote, Waziri Mkuu na Mawaziri wote wanaomsaidia, Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa na Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tulivyoomba 2020 kuchaguliwa kuwa Wabunge, zipo ajenda zilikuwa zinagusa Jimbo letu la Kilombero na yalikuwa mambo makubwa yanayotugusa wananchi wote. Tunavyosema leo, yamekamilika na kwamba changamoto lazima ziendelee tu mpaka mwisho wa dunia siyo lakini yale makubwa yamekamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikisema barabara ya lami Kidatu mpaka Ifakara imekamilika, wananchi Jimboni wanajua Mbunge anasema kweli au anasema uongo. Nikisema tumeshasaini

mkataba wa kujenga barabara ya Ifakara kwenda Ulanga, wameona kwenye vyombo vya habari tumesaini mkataba. Tukisema mkandarasi wa barabara ya Ifakara ya lami kutoka Ifakara kwenda Mlimba, wanajua mkandarasi yupo *site.* *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikisema leo tangu Wilaya ya Kilombero iumbwe safari hii ya Mama Mheshimiwa Dkt. Samia awamu hii ndiyo tumejenga Hospitali ya Wilaya, wanaiona Hospitali ya Wilaya. Nikisema vituo vya afya viwili; tulikuwa na kituo cha afya kimoja, miaka yote tumejenga viwili wakati wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, wanajua *Kituo cha Afya cha Msola Station* na *Kituo cha Afya cha Mbasa*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukisema umeme ulikuwa na changamoto za kukatika, Waziri wa Nishati amekuja, tumepewa karibu shilingi bilioni 25, tumejenga *substation,* umeme zaidi ya mwaka haukatiki, wanayo *substation* ipo Ifakara na umeme haukatiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi Mbunge siwezi kusema kwamba umeme haukatiki, halafu umeme unakatika na mwaka huu ni mwaka wa hukumu. Kwa hiyo, Mbunge unavyozungumza hapa, unazungumza jambo la ukweli. Tangu dunia iumbwe katika kipindi hiki cha miaka mitano tumejenga sekondari za *O' Level* 12. Yaani nimemzidi mpaka Mheshimiwa Waziri Aweso kwa Shule za Sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona Mheshimiwa Waziri Aweso anamwomba Mheshimiwa Rais, Kata zake nyingine hazina sekondari. Mimi nilishamaliza Kata 19 sekondari za O' *Level* na ninajenga nyingine za kurudia. Tunajenga Sekondari za *advance* tano, tumejenga shule ya ufundi hizi za amali imekamilika na wanafunzi wameanza kusoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna mradi wa maji wa Kiburubutu shilingi bilioni 41 unajengwa Ifakara Mjini, Kata tisa kuongoza kutatua changamoto ya maji. Wilaya tangu imeumbwa ilikuwa haina Kituo cha Polisi cha Wilaya, tumeshakijenga mpaka viyoyozi *(AC)* Mheshimiwa Rais kanunua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna Mahakama ya Wilaya ya ghorofa. Kwa mara ya kwanza gari la zimamoto wananchi wameliona, kwa mara ya kwanza magari ya Polisi *Ambulance* na kadhalika. Kwa hiyo, nataka kutia msisitizo, hapa tunasema changamoto haziwezi kwisha, maendeleo ni hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule Ifakara kwangu kuna maeneo wanapima viwanja, wananchi wanaanza kujenga. Wakijenga, wanataka Barabara, wanataka umeme, wanataka maji. Hiyo ni kazi yetu viongozi kufanya. Tunajua changamoto yao kubwa ni kazi yetu kama Bunge kusimamia na kuishauri Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya wananchi wachache wanafikiri kwamba ukiwa Serikalini, basi ni kuiba, ni wizi. Wanatushauri sana Wabunge tuwaambie Serikali, anapotokea mwizi, mbadhirifu, akamatwe, achukuliwe hatua. Hii ni kazi ambayo sisi sote tunaweza kuifanya. Kwa hiyo, hilo la kwanza nataka kusisitiza kwamba mambo makubwa yamefanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili ni changamoto na matarajio. Katika bajeti ya Serikali ya Waziri Mkuu, nimesoma karibu kurasa zote. Nimeona kuna changamoto na tunasema hapa ili Serikali izichukue, iziandike ikazifanyie kazi, na kuna fedha nyingi ya mwakani itakuja itayabeba mengine katika Uchaguzi Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, nataka kuzungumza hapa kuhusu sekta ya kilimo. Nimeona Mheshimiwa Waziri Mkuu amezungumzia hapa. Sisi tuliomba kiwanda kipya cha sukari karibu shilingi bilioni 700 tumejengewa kiwanda kipya cha sukari, lakini tunaiomba Serikali, na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo namwona hapa. Nimekutana na wakulima, na juzi wakulima walikuja Dodoma hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna changamoto ya ulipaji bei, kuna siasa inataka kuchezwa katika kilimo cha muwa. Tunaomba Serikali imulike, nimemwambia Waziri wa Kilimo, nimemwambia

Naibu Waziri na ninawaambia viongozi wote wa Serikali watazame.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watu tulivyobadilisha sheria ya kuruhusu kuingiza sukari kwa ajili ya kuwa-*favor* wananchi wasinunue sukari kwa bei mbaya, wanatumia *gap* hiyo kufanya siasa na siasa hizo zinahusisha wakulima wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina asilimia karibu 60 ya wananchi wangu ambao ni wakulima wa miwa. Sasa wamejenga kiwanda kipya cha sukari shilingi bilioni 700. Mkulima alikuwa anauza muwa tani shilingi 110,000 kwa shilingi 103,000, leo wanaambiwa shilingi 87,000. Mkulima akishauza muwa, anasubiri sukari iuzwe, sukari ikishauzwa analetewa fedha zaidi iliyobaki. Sasa hivi anaambiwa hakuna makato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkulima huyo huyo alikuwa anauza kwa *sucrose* ya kumi ya muwa anapata shilingi milioni karibu tatu kwa gari, sasa hivi anaambiwa karibu shilingi 600,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wazee wa Kilombero pale wameniita wakaniambia, Mbunge hiki kiwanda kipya kinaweza kisifanye kazi, watu watakosa moyo wa kulima muwa endapo Serikali haijachukua hatua za kutosha. Nimeshukuru sana Bodi ya Sukari, niliambiwa ilienda kufanya mkutano kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami ninasisitiza hapa tumejenga kiwanda kipya cha shilingi bilioni 700. Jambo kubwa ilikuwa ahadi yetu, sasa lazima tukawasikilize wakulima hawa na Mheshimiwa Waziri ameniambia au Naibu Waziri, tutaenda kukaa nao, tutawasikiliza ili kiwanda kile kiweze kulipa kama ilivyokuwa inalipa mwanzo shilingi 110,000 kwa tani na wananchi wapate fedha zao kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine tuna changamoto na *TARURA*. *TARURA* hawajapata fedha wakandarasi wengi kila Mbunge hapa anazungumza. Mimi nina imani sana na Waziri wa TAMISEMI, najua akija hapa atakuja na *solution* ya vituo vya afya

vya kimkakati ambako sisi tunajenga kule Michenga na Lumemo kituo kimoja cha afya, lakini Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI atakuja na majibu kuhusu *TARURA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa Jimboni jana, nimepita Ifakara Mjini sehemu inaitwa Mbasa Mjini, Ifakara ambako Mbasa Kwa Mfuga Punda Soko la Kariakoo, wanapita wananchi pale kama maji kwenye bomba, mkandarasi amejenga karavati ameondoka ameacha bila kufunika. Nimeongea na viongozi wa *TARURA,* mkandarasi yule hajalipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepita Katindiuka Ofisi ya Kata pale kuna Barabara, kuna makaravati. Mji wangu ule wa Ifakara upo mbondeni kidogo, barabara ili ipitike miaka yote lazima uichonge uweke changarawe uweka na makaravati. Sasa hali ile kwa Kata zote 19 kwa kweli ni mbaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba viongozi wangu wa *TARURA* tuweke angalua bajeti ya kueleweka na mpango maalumu wa kilometa kumi kumi katika Kata tupate kilometa 190. Itasaidia Jimbo letu na kuliondoa na barabara za *TARURA*. Hii ni changamoto kubwa sana. Pale pale Ifakara Mjini ukitoka Lumemo ukivuka tu daraja la Lumemo pale barabara ya *TANROAD* unaenda Mlimba ina mashimo manne makubwa na jana nimemtumia *Chief of TANROADS* barabara hiyo na ameiona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa nishati, ninafurahi ninamshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, kwani mara zote amekuja Jimboni kutufanyia siasa nzuri. Katuondolea tatizo la kukatika kwa umeme, vijiji vyote tumeshafikisha umeme. Namwomba katika vile vitongoji 15 najua wakandarasi wapo kule, wanaendelea, a-*push* kidogo nipate vitongoji vyangu 15, mkandarasi a-*supply* umeme katika vitongoji na juzi nilikuwa katika Kitongoji cha Upendo na Tupendane Michenga, hali bado ni ngumu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi ni miongoni mwa watu waliopata Mradi wa *TACTIC*. Mji wa Ifakara unakua, Mji wa Ifakara

benki hazifungwi Jumamosi na Jumapili kwa sababu tu ni wakulima wazuri na ni wafugaji wazuri. Tumepata soko jipya, Waziri wa Viwanda na Biashara amekuja pale, Mheshimiwa Jafo amezungumza pale na amevaa suti imempendekeza kabisa, na akatuambia Asenga linakuja hili soko Ifakara Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Serikali ituletee lile soko haraka kabisa, kwa sababu pale wafanyabiashara wa Soko la Ifakara Mjini wameshapisha ujenzi, wameenda kusogeza fremu zao mbali, wameacha lile eneo. Tumeambiwa soko zuri la ghorofa katika Mradi wa *TACTIC* linakuja. Tunaomba kazi hiyo ianze haraka iwezekanavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mji wetu wa Ifakara umesongamana, na barabara ya Mjini pale haina uwezo tena. Tunaomba sana Serikali itusaidie Mradi wa *TACTIC* wa stendi mpya kama ambavyo ilivyopanga. Mheshimiwa *DC* pale naona anasimamia vizuri, anafuatilia sana jambo hilo. Mradi huu wa *TACTIC* utaambatana na barabara za lami. Tunaomba nao uanze kwa wakati, kwa sababu kwa kweli ni changamoto kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huku nikimalizia, nataka kuzungumzia suala la maafa. Tunamshukuru Mwenyezi Mungu, mpaka sasa Halmashauri ya Ifakara na Jimbo la Kilombero hatujapata maafa kwa kiasi kikubwa, lakini mvua zimeanza. Naendelea kuwaomba na nilimwomba Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu anisaidie, *TANESCO* walijenga tuta upande mmoja wa mto, wajenge na upande wa pili. Nimepeleka barua Ofisini kwake, wanisaidie ili tuweze kupunguza hilo suala la tuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuzungumza kwenye suala la ardhi. Naishukuru sana Wizara ya Ardhi, kwa kweli kwa kiasi kikubwa imepunguza sana changamoto za migorogoro ya ardhi, na tangu wakati ule, tangu Mheshimiwa Lukuvi akiwa Waziri, tulianza kupata hati za kimila. Wananchi wakaona ardhi yao imepanda thamani, na kasi kubwa, wanauza. Tunawasihi kila siku wasiuze ardhi yao, lakini sasa kuna changamoto moja ya Baba

Askofu pale Kanisani, nilizungumza Mheshimiwa Rais alivyokuja tarehe 4 Agosti, mwaka 2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali isikilize jambo hili ili iweze kutusaidia. Kwa heshima kubwa, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Asenga. Nilimwita Mheshimiwa Livingstone Joseph Lusinde, atafuatiwa na Mheshimiwa Mary Francis Masanja, Mheshimiwa Juma Usonge Hamad, ajiandae.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kunipa nafasi hii. Namshukuru Mungu sana kwa kunipa mimi, na Waheshimiwa Wabunge wewe afya njema pamoja kwa ajili ya kujadili bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na bajeti nzima ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi nyingi sana zimetolewa kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, nasi pia kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mvumi tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa sababu, kama kulikuwa kuna kimeo cha muda mrefu na kichomi ilikuwa ni barabara yetu ya Ntyuka *Junction* - Mvumi *Mission* - Kikombo kwenda kutokea Handali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo furaha kwamba Mheshimiwa Rais ametupatia pesa na sasa hivi mkandarasi yupo *site* anafanya *mobilization* vifaa vyake ili aweze kuanza ujenzi mara moja. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuliona hilo. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge mkija kutibiwa tena pale hamtakutana na vumbi, mtakutana na mkeka tu kutoka hapa mpaka Mvumi unaunganisha Kikombo Makao Makuu ya Jeshi unakuja kutokea Chamwino Ikulu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu na Baraza zima la Mawaziri, wamefanya kazi kubwa kumsaidia Mheshimiwa Rais kutafsiri maono yake pamoja na ndoto zake, lakini nataka niseme mambo machache hapa.

Jambo la kwanza, nchi ikitaka kubadili hali ya uchumi wa nchi kwa haraka na uchumi wenyewe siyo ule unaoonekana kwenye karatasi, bali ule unaohusianisha watu na unaozingatia kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo pekee yake ndiyo kinaweza kikabadilisha maisha ya watu wengi kwa haraka, na ni maono ya Mheshimiwa Rais akaona kwamba ni vyema kuwekeza nguvu kubwa kwenye kilimo, Mheshimiwa Rais akanunua magari kwa Maafisa Ugani wa mikoa yote, akanunua pikipiki kwa Maafisa Ugani wa kata zote, akanunua mashine za kupimia udongo kujua afya ya udongo, karibu kata zote zimegawiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais hakuishia hapo, akanunua *photocopy machine,* kwamba ukipima udongo unaweka kwenye *photocopy machine* inatoa majibu kwamba shamba hili linahitaji uweke mbolea gani? Linahitaji ulime zao gani ili mkulima aweze kupata tija? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado hatuoni hizo mashine na hizo pikipiki zikifanya kazi ambayo Mheshimiwa Rais ameikusudia. Leo hii tukitaka tutembee kwenye kata za Waheshimiwa Wabunge, ni kata ngapi ambazo tutakuta Afisa Ugani amebandika pale wakulima aliowatembelea, vipimo vilivyopimwa na tija waliyopata? Ni tofauti kabisa na mawazo ya Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaitaka Serikali kusimamia haya maono yatokee kwa vitendo ili yaweze kusaidia wananchi kusonga mbele. Kama huwezi kuuza nje mazao makubwa kama mkonge, kahawa, korosho, na zabibu kwa maana ya mvinyo, unainuaje uchumi wa hilo Taifa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni maono ya Mheshimiwa Rais kwamba Maafisa Ugani watembee kwa wakulima. Leo tukifanya sensa, hatuwezi kukuta Afisa Ugani, siyo tu kwa wakulima, hajatembea shamba la Diwani; hajatembea shamba la Mbunge; hajatembea shamba lake yeye mwenyewe. Sasa hii siyo sawa. Hatumtendei haki Mheshimiwa Rais, na hatutendei haki maono ya Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi Mheshimiwa Rais amekaa hapa na Maafisa Ugani akaagiza, anzisheni Wakala wa Ugani kwa maana ya namna ya kufanya kazi, itakuwa rahisi. Tuwe na wakala kama ilivyo *TANROADS* na *TARURA*. Tuwe na wakala wa namna hiyo kwa Maafisa Ugani ili kuweza kuwa na *speed* ya kuwakagua. Mpaka leo nataka kujua, imefikia wapi? Maana tunaona mpaka tunamaliza mpo kimya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuzungumza hapa hapa kwenye kilimo. Mheshimiwa Rais ametupatia shamba kubwa sana lipo Mlazo pale. Ukienda utaona matokeo, vijana wa *BBT* wameripoti, wamelima alizeti, zimekubali, lakini tuna tatizo. Tatizo letu kubwa ni kwamba wataalamu wetu hawapiti kushauri. Kazi yao kubwa ni kupanga tu mwaka huu ushuru gunia moja shilingi 5,000/=. Shilingi elfu tano, umelima wewe! Elfu tano, umemsaidia nini huyu mkulima?

Mheshimiwa Mwenyekiti, huyu mkulima hujamsaidia kumshauri, hujamsaidia mbegu, hujamsaidia mbolea, hujampimia ardhi yake, wewe unapanga tu kwamba mwaka huu tunataka ushuru wa gunia uwe shilingi 5,000. Hivi hii ndiyo elimu mliyopewa jamani! Elimu gani hii ambayo mmepewa ya kupanga tu bei bila kusaidia watu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, angalia kero anazopata mkulima. Mkulima analima kwa tabu, hakuna mtu anamshauri, akishapata mazao yake akiyaleta sokoni, anakutana na *barrier* pale Mkonze, anakamatwa, anaambiwa gunia limezidi kilo 20, unalipa shilingi 500,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukubaliane leo kwenye Bunge na Mheshimiwa Waziri akisimama atusaidie hapa, kwani gunia Serikali inavyolitambua ni kipimo au ni kifungashio? Kama gunia ni kipimo, kwa nini watu wa *TBS* wanaruhusu gunia linalozidi kilo mia kuwa sokoni? Kwani anayelileta gunia ni mkulima? Wanaolileta gunia ni watu wengine, limegongwa muhuri wa *TBS*, mkulima ananunua, akilijaza linaingia kilo zaidi ya mia moja, anakuja anakamatwa anaambiwa faini shilingi 500,000, vinginevyo mazao

tunayataifisha. Sasa mnataka kutuambia kila mkulima pamoja na shida na tabu za kulima, kila mkulima awe na mizani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kila mkulima anunue mizani aweke shamba? Huu utaratibu wa wapi? Hii siyo sawa. Haya mambo ndiyo Mheshimiwa Rais anayakataa kila siku. Katika Serikali kuna baadhi ya watumishi wetu huku chini wanaonea watu. Haiwezekani, kwa sababu gunia hakutengeneza mkulima. Kwa nini tusimshtaki yule anayetengeneza gunia kwamba umetengeneza gunia ambalo linachukua zaidi ya kilo 100?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kweli tunataka kutenda haki, kwa nini Maafisa wetu wa Vipimo hawakai kwenye mizani anapokuja kuuzia? Akifika pale anaambiwa bwana utalipa ushuru kulingana na kilo utakazopima, limeisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini twende tuwadhulumu watu mazao yao? Inakuwa tabu kwenye kulima, na tabu kwenye kuuza na tukumbuke kwamba mkulima wa kawaida siyo mfanyabiashara wa mazao. Yeye anakuja kulima na kuuza mwaka mmoja mara moja, anataka zile pesa zisaidie familia yake. Kwa hiyo, hili jambo mimi nimeona limekuwa likileta uchungu sana na malalamiko makubwa sana kwa wananchi. Ni lazima tusimamie haki za wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ninalotaka kulizungumza hapa, ni kuhusu mfumo wa kupambana na majanga kwenye kilimo. Hii ni tofauti na mifumo mingine yote ya taasisi. Leo hii ukitokea moto, utaona zimamoto wanaenda kwa haraka sana. Ikitokea nguzo zimeanguka, *TANESCO* wataenda kwa haraka sana, lakini ikitokea janga kwenye kilimo, ndugu zangu ni matatizo makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kikianguka viwavijeshi, anatakiwa Afisa Ugani wa Kijiji amwandikie Afisa Ugani wa Kata, Afisa Ugani wa Kata amwandikie Afisa Ugani wa Wilaya, Afisa Ugani wa Wilaya amwandikie *DAS*, *DAS* amwandikie *RAS, RAS* aandike Wizarani, hilo shamba utalikuta? Huwezi kulikuta. Yaani

huo mlolongo wa kuandikiana na kupeana taarifa utakuta shamba limeshakuwa jeupe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu bahati mbaya sana, fidia za Serikali ni za ajabu sana. Leo hii mtu akiua tembo analipa karibu shilingi milioni 15 au 30, lakini huyo huyo ndovu akiua mtu, kifuta machozi ni shilingi milioni moja. Leo hii mtu akifanya *abortion* anashtakiwa kwa mauaji kwamba ameua mtoto ambaye alikusudiwa kuzaliwa, lakini shamba la mtu likiliwa kabla halijaiva wakati wa kufanya uthamini yale mazao, wanasema asingepata gunia 40. Kwa nini asingepata gunia 40 wakati yeye ndio uwezo wake wa shamba lake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuthaminishe sawa sawa. Leo binadamu anauliwa, mnasema shilingi milioni moja kifuta machozi. Shamba zima ekari 20 zimeliwa, mnalipa gunia moja. Hivi gunia moja mtu anaweza akala mwaka mzima? Huu utaratibu wa wapi? Hiyo siyo sawa! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nashauri kwamba Serikali tusimamie haki za wakulima. Ikitokea matatizo, tuwe *serious* kama tunavyochukulia matatizo ya sehemu nyingine. Unavyopeleka mgonjwa kwa *speed* kuwahi matibabu, ndivyo upeleke ndege ya kuua ndege kwenye mashamba ya wakulima kwa sababu ukichelewa wakishamaliza mazao, huyu mkulima hana kitu. Halmashauri haina kodi na wala mwenyewe hawezi kutunza familia yake pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, tumezungumza sana kuhusu ajira na hili mimi nalirudia tena hapa. Nilishauri kama tunaona hatuwezi kuwaajiri Watanzania wote kupitia *Ajira Portal*, ajira hizi tuzigawe kwenye halmashauri. Kila halmashauri, wewe ajira zako 20, wewe ajira zako 10, wewe ajira zako 30. Wakikosa kupata mtu mwenye elimu hiyo ambayo inatakiwa kwenye hiyo ajira, watairudisha ile ajira kuipeleka mkoa mwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu utaratibu wa kuwaleta wote Pamoja, hivi, hivyo vyeti mlivyowapa mnavikagua unasema hiki cheti chako *original* kabisa, halafu baadaye unamwingiza

kwenye mtihani wa dakika moja ndiyo umkoseshe mtoto ajira! Haiwezekani. Tunawa-*stress* watoto wetu. Hii siyo sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe umekagua cheti chake; cheti cha Ualimu mtu amesoma zaidi ya miaka mitatu, yaani wewe unakuja kumpa mtihani wa dakika mbili, unafuta yote haya! Masomo yote aliyosoma miaka mitatu yanaonekana hayana maana kwa sababu ya mtihani wa dakika mbili! Hapana, hii siyo sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama uwezo wetu tunaajiri watu 15, tuseme ajira 15,000 tunazigawa katika halmashauri, nendeni muajiri bila kusumbua watu, mnawajaza hapa. Wanakuja wanalala nje, watoto wa watu wanakuja na nauli za kukopa, wakija hapa wanaishi maisha magumu sana. Hii siyo sawa. Sasa badala ya kuondoa kero, tunazalisha kero. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inakuwa siyo sawa, kwani ukisema kwamba tuna uwezo wa kuajiri watu 15,000, leteni vyeti, ukavikagua, ukawaajiri, si jambo limeisha? Sasa leo hii unakuja unanipa mtihani, mtihani wenyewe wa dakika moja, halafu huu huu mtihani wa dakika moja unaniondolea sifa yote niliyosoma, halafu huyo huyo aliyefeli mwaka huu, amekosa; mwakani anafaulu. Hiyo inakuwa siyo sawa. Kwa hiyo, ni lazima tuwatendee haki kabisa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, nimezungumza sana kuhusu lango la utalii. Kutoka hapa kwenda Iringa ukitumia barabara ya lami uje kuingia mpaka kwenye mbuga za Wanyama, mzunguko wake ni mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekit, tuna barabara ya mkato, tunaishauri Serikali kwamba ukitoka hapa mpaka Mpunguzi kwa Mheshimiwa Anthony Mavunde, ukitoka pale Mpunguzi nenda moja kwa moja, nyoosha moja kwa moja mpaka Huzi, ukitoka Huzi nenda moja kwa moja Manda, ukitoka Manda jenga pale daraja la kuingia kwenye mbuga. Hii inakuwa rahisi sana kwa watalii, na sisi huku tutaguswa na maendeleo kwa haraka kwa sababu na sisi mbunga yetu huku tunakutana na Mzee Lukuvi kule pamoja na

kwamba ananong'ona pale. Tunaomba watusaidie kurahisisha lango la utalii lipitie Ilangali badala ya kupitia sehemu nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsanteni sana kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Lusinde. Nilishamwita Mheshimiwa Mary Francis Masanja, Mheshimiwa Juma Usonge Hamad, atafuatia na Mheshimiwa Rehema Juma Migilla.

**MHE. MARY F. MASANJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia katika bajeti ya Waziri Mkuu. Awali ya yote, namshukuru sana Mwenyezi Mungu ambaye ametupatia afya njema na leo tumeweza kukutana hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kabisa, nichukue nafasi hii kumpongeza na kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa aliyoifanya ya utekelezaji wa Ilani ya uchaguzi ya mwaka 2020/2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitazama miradi mikubwa ya kimkakati iliyofanyika katika Mkoa wa Mwanza na Kanda ya Ziwa kwa ujumla, siwezi kuielezea hapa kwa siku moja. Miradi ni mikubwa na imetekelezwa kwa zaidi ya 98%. Nikienda kwa upande wa Kigongo - Busisi katika Sekta ya Ujenzi tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais. Daraja hili liliachwa likiwa 25% na mtangulizi wake, lakini hivi ninavyoongea, daraja hili sasa limefikia 98%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wanamwanza tunajiandaa kwenda kusheherekea ufunguzi wa daraja hili. Daraja hili lina ukubwa wa kilometa 3.2, Tanzania hapa halipo, Afrika Mashariki nadhani ndiyo tunaongoza, lakini ukiliangalia linatupa sifa nzuri ya nchi yetu na linatangaza utalii wa Kanda ya Ziwa hususan Mkoa wa Mwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, faida ya daraja hili itakuwa ni faida nyingi, lakini kikubwa daraja hili linakwenda kuokoa vifo vya mama na mtoto. Wakati ule tunatumia kivuko, akinamama walikuwa wanakaa zaidi ya masaa sita pale kwenye kivuko wanasubiri kivuko na wakati huo wanakimbizwa kwenda kujifungua. Leo hii pale tutatumia dakika chache tu na akinamama watawahishwa na usalama wa mama na mtoto utapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiacha hilo, kuna faida nyingine ya uchumi. Uchumi utakuwa mkubwa na utafungua mikoa ya jirani ikiwemo Mkoa wa Geita, Mkoa wa Kagera, Simiyu, na mikoa ya jirani inayozunguka daraja hilo kwa maana ya Mkoa wa Mwanza. Pia nchi jirani zitaweza kufaidika kwa sababu kutakuwa na urahisi sasa wa kuzunguka kwa maana ya kupitisha biashara mbalimbali kwenda ndani ya nchi na nje ya nchi. Ukiacha faida hizo, daraja hili linaenda kuokoa muda ambao ulikuwa unapotea kwa kusubiri kivuko kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie sasa kuhusu Sekta ya Nishati. Sisi akinamama tunamshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kututua kuni kichwani. Tangu mababu na mababu zetu wamekuwa wakitumia nishati chafu ya kupikia. Mama zetu hasa upande wa Kanda ya Ziwa wamekuwa wakisingiziwa wengine wana mambo ya kishirikina kwa ajili ya macho mekundu, lakini moshi huu huu unaenda kuathiri mapafu. Mapafu haya yanapata athari kubwa na madhara mengine makubwa ya kiafya na matokeo yake wananchi wetu wanatumia gharama kubwa kwenda kujitibia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tunamshukuru Mheshimiwa Rais kwa sababu ameibeba kama ajenda ya kitaifa, na hii ajenda ni ya kidunia, lakini mama ameibeba kama ajenda ya kitaifa. Leo hii hakuna mama asiyejua matumizi bora ya nishati safi ya kupikia. Tunamshukuru sana, lakini naiomba Wizara ya Nishati itusaidie akinamama kwa sababu sasa kuna mwamko mkubwa wa kutumia nishati safi ya kupikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, changamoto iliyopo ni kwamba bei ya ku-*refill* au kuongeza ile gesi ni kubwa sana, ukizingatia uchumi wa akinamama upo chini sana. Tunaiomba Serikali iendelee kuongeza ruzuku ili hawa akinamama wasiishie kukaa na mitungi ikiwa mitupu. Waendelee kurudi kwenye hali ile ya zamani ambayo kwa sasa hivi ninavyoongea tayari tunaenda kuokoa ukataji wa miti ovyo, na mazingira ambayo yalikuwa tayari yanaendelea kuharibika, sasa hivi yanaenda kuimarika vizuri. Naiomba Serikali yangu Tukufu ilione hili ili iendelee kutoa ruzuku katika eneo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nizungumzie suala zima la Sekta ya Uchukuzi. Sekta ya Uchukuzi kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2022, Mkoa wa Mwanza ni mkoa wa pili Kitaifa kwa kuwa na idadi ya watu wengi. Ukiacha hilo, Mkoa wa Mwanza ni wa pili kwa kuchangia pato la Taifa. Pia, Mwanza imepakana na mikoa zaidi ya mitano ambayo huwa inatumia suala zima la matumizi ya uwanja wa ndege wa Mwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachosikitisha ni kwamba, hakuna *route* ya kutoka Mwanza kuja Dodoma na kurudi Mwanza. Wasafiri wanaotoka Mara, Simiyu, Shinyanga, Kagera, na Geita inatulazimu kufunga safari zaidi ya masaa 10 kutoka Mwanza kuja Dodoma kufuata huduma za Kiserikali kwa maana ya wananchi, lakini hata sisi wenyewe Waheshimiwa Wabunge tunapokuja Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kama Mkoa huu tu pekee ni wa pili kwa kuchangia, inachangia 7.2%, kwa nini kusiwepo na *route* inayotoka Mwanza kuja hapa Dodoma na kurudi? Ni nini kinachokwamisha? Pia, naiomba Wizara ya Uchukuzi, pale Mwanza kuna upanuzi wa jengo la abiria. Upanuzi wa jengo hili utasaidia Uwanja huu upate sifa ya kuitwa Uwanja wa Kimataifa wa Mwanza. Tunakwama na tunakwamisha uchumi mkubwa katika Mkoa wa Mwanza kwa sababu Mwanza ni lango zuri kwa suala la utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watalii wanazunguka, wanapita Arusha, wakitoka Arusha wanaenda kilometa zaidi ya 500 kwenda

kuiona Serengeti, lakini ukiwa Mwanza kwenda Serengeti ni kama kilometa 134, umefika lango la Serengeti. Hata hivyo, kwa sababu uwanja huu siyo wa Kimataifa, ndege kubwa haziwezi kushuka pale kwa sababu tu ya jengo la abiria ambalo mpaka sasa limekwama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali yangu, kupitia Wizara ya Uchukuzi iweze kulitilia maanani suala hili ili tufungue uchumi wa Mwanza na usafiri wa anga uweze kuimarika katika Mkoa wa Mwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa namna ambavyo aliweza kuzindua huduma ya usafiri wa reli. Usafiri huu ni wa raha, ni usafiri ambao hakuna Mtanzania ambaye hajaufurahia. Sote tumeufurahia na wote tumeonja raha ya usafiri wa reli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa sababu ametupa heshima kubwa Kitaifa na Kimataifa. Sasa hivi usafiri wa reli hakuna mtu asiyeupenda, na nimeiona bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ya kwamba vipande vilivyobaki ni vipande vya Mwanza – Isaka, kuna Makutupora – Tabora, Tabora – Isaka na Tabora – Kigoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatamani sana reli hii tuonje utamu wanaoupata wengine kwenye upande wa pili. Nasema hivyo kwa sababu tukiweza kuunganisha reli hii ikakamilika, kwanza tutaokoa muda, na uchumi utakuwa pamoja na kurahisisha muda wa wananchi kusafiri kutoka sehemu moja kwenda nyingine kwa wakati. Pia tutapunguza ajali…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. MARY F. MASANJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mary Masanja. Nilimwita Mheshimiwa Juma Usonge Hamad na sasa simwoni. Tuendelee na Mheshimiwa Rehema Juma Migilla, atafuatiwa na Mheshimiwa Benaya Liuka Kapinga.

**MHE. REHEMA J. MIGILLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi nami jioni hii niweze kuchangia Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai na afya ambayo inanifanya niweze kusimama katika Bunge lako Tukufu kwa jioni hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa moyo wa dhati na kipekee kabisa, napenda kumshukuru Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa maono yake na mapenzi yake mema kwa Watanzania hususan wananchi wangu wa Ulyankulu. Ameweza kutufanyia mambo makubwa sana tangu alipoingia madarakani, nami kama Mbunge wa Jimbo la Ulyankulu, tangu niingie madarakani kuna mabadiliko makubwa sana na maendeleo makubwa sana ambayo yamepatikana katika Jimbo langu la Ulyankulu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ulyankulu ya mwaka 2020 siyo Ulyankulu ya mwaka 2025. Kiufupi niseme, naishukuru sana Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na wasaidizi wake wote ambao wanamsaidia katika kuhakikisha wananchi wa Tanzania na wa Jimbo la Ulyankulu tunapata maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, napenda kumshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu na timu yako, kwa kweli wanafanya kazi nzuri ya kuhakikisha huduma zinawafikia wananchi kwa ukaribu na kwa raha zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kuchangia mchango wangu wa leo kwa kuanza na sekta ya kilimo. Jimbo la Ulyankulu kwa kiasi kikubwa asilimia kubwa ya wananchi wake kama siyo yote, wanashiriki kwenye shughuli ya kilimo kama ndiyo shughuli yao mama ya kuwaingizia kipato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapenda kuishukuru Serikali yetu kwa mambo makubwa sana ambayo imeweza kuyafanya kwenye sekta ya kilimo, kwani tunaona sasa hivi tayari kuna mbolea ya ruzuku ambayo imetolewa kutoka shilingi 150,000 mpaka 60,000. Hayo ni mabadiliko makubwa na ni faida kubwa sana kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, tunaona pembejeo zinatolewa na zinakuja kwa wakati katika Jimbo langu, na bado wananchi wanapata katika maeneo yao yaliyo karibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, kwenye zao hili la tumbaku tunaona bei elekezi imetolewa na wananchi wetu wanauza tumbaku yao kwa bei ambayo ina manufaa kwa maendeleo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikisalia hapo hapo kwenye tumbaku, pamoja na haya mazuri yote ambayo yamefanyika kwenye hili zao letu la tumbaku, bado zao hili linaonekana kama halina tija kwa mkulima wetu. Kwa mfano, mwaka jana 2024 ilinyesha mvua kubwa sana. Mwenyezi Mungu alitupatia baraka ya mvua, lakini baraka hii ilikuwa ni kilio kwa wananchi wangu wa Ulyankulu ambao wamelima tumbaku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mashamba mengi yalilowa na bani zao nyingi zilianguka, hivyo wakawa kwenye madeni na kwenye sonona kubwa sana, lakini kupitia Mama Samia, akatuletea ruzuku ya tumbaku kufidia yale madhila ambayo wananchi wameweza kuyapata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi tunavyoongea, tulimsikia Mheshimiwa Bashe hapa amesema zimetengwa shilingi bilioni 13 kwa ajili ya kuwalipa fidia ya ruzuku wakulima wote wa tumbaku hapa Tanzania, lakini cha ajabu mpaka hivi leo tunavyoongea wakulima wangu wa tumbaku hawajalipwa hii ruzuku na hatufahamu ni kwa nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbaya zaidi wananchi na wakulima hawa wamesainishwa saini hewa bila kujua amesaini

shilingi ngapi ambazo atakwenda kulipwa. Sasa Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Waziri wa Kilimo tunataka tufahamu, hivi kuna usiri gani kwenye hii fedha? Kama mlisema hawa wakulima watalipwa kulingana na idadi ya mifuko ya mbolea waliyotumia, leo mnakwenda kuwasainisha wakulima wetu saini hewa, kuna usiri gani hapo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo mtu anasaini hajui anaenda kusaini shilingi ngapi na kwa nini mfanye hivyo? Mnafanya makusudi au vipi? Leo mtu anasaini lakini hajui analipwa shilingi ngapi? Je, ukienda mkulipa fedha ambazo ni tofauti na idadi ya mifuko ambayo ametumia, ataenda kudai wapi wakati tayari ameshaweka saini yake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Waziri wa Kilimo mtueleze hili suala na wananchi wetu wajue, kuna watu wamesaini miezi miwili iliyopita na mwezi mmoja uliopita lakini mpaka leo wanaendelea kuhangaika hawajui fedha zao watalipwa lini? Naomba hili suala lichukuliwe kwa umuhimu mkubwa na wananchi wetu wajulishwe kwa nini mpaka leo hawajalipwa hizi fedha? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo hapo kuna kampuni ya wazawa ya *Voedsel* inayonunua tumbaku. Mpaka hivi tunavyoongea, wakulima waliolima tumbaku msimu wa mwaka jana 2024, hawajalipwa fedha zao na Kampuni ya *Voedsel* mpaka leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina wakulima wangu 86 kutoka Kijiji cha Usonga hawajalipwa hata shilingi moja na tayari tuna msimu mwingine na hivi tunavyoongea, soko linaenda kuanza tarehe 28, lakini hawajalipwa. Naomba hawa wananchi wangu waweze kulipwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala lingine la barabara. Naendelea kuipongeza Serikali kwa kuweza kutuongezea bajeti kwenye Halmashauri yetu ya Wilaya ya Kaliua. Mwaka 2020 bajeti yetu ya barabara ilikuwa ni shilingi milioni 985, lakini leo tunavyoongea, tayari bajeti ya barabara imefika shilingi

4,300,000,000. Kwa kweli haya ni mafanikio makubwa. Tunachoiomba sasa Serikali yetu, iweze kuzitumia hizi fedha vizuri na hizi fedha ziweze kufika huko chini kwa sababu barabara nyingi zimeharibika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mvua ya mwaka 2024 imetuharibia barabara karibia zote, lakini mpaka hivi leo tunavyoongea, kuna baadhi ya wakandarasi hawajalipwa na wamekimbia kwenye maeneo. Vifusi vingi viko kule na havijasambazwa, barabara hazijatengenezwa na wakandarasi wamekimbia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inasababisha kuwaongezea wananchi wetu mzigo wa maisha, wanasafiri kwa tabu sana kwa sababu inawalazimu waweze kutembea kwenye njia ambazo ni ndefu sana kwa sababu zile njia ambazo zina vifusi hazipitiki. Hivyo, naiomba Serikali kusimamia na kuiongezea *TARURA* bajeti ili iweze kuzihudumia barabara zetu kwa umakini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, naipongeza Serikali, imeweza kuanzisha hii *Samia Bond* ambayo inawawezesha wakandarasi wa ndani kupata fedha kuanzia 30% mpaka 70%. Hali hii itawezesha barabara zetu kutengenezwa kwa umakini, lakini pia na hawa wakandarasi wawepo *site* na wawe na uhakika wa kuweza kutengeneza hizi barabara zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, naishukuru Serikali, lakini pia naomba Serikali isilegelege, ihakikishe inaweza kufunga mkanda kuhakikisha hizi fedha zinatoka na wakandarasi wanapata ili waweze kwenda *site*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la maji. Ni nia ya dhati kabisa ya Mheshimiwa Rais kuhakikisha anatutua kina mama ndoo kichwani, lakini suala hili kwa watu wa vijijini bado kabisa. Mimi nikirejea kwenye Jimbo langu la Ulyankulu, lina Kata 15 lakini katika hizi Kata 15 tumepata mradi wa maji wa bwawa la Ichemba ambao unagharimu shilingi bilioni 3.98, lakini mpaka hivi tunavyoongea mradi huu umeingiziwa fedha shilingi 598,000,000, fedha ambayo ni ndogo kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tujue kwamba Jimbo la Ulyankulu, maji kutoka chini ya ardhi yako chini sana, mbadala wake ni maji kutoka Ziwa Victoria. Mheshimiwa Waziri Mkuu, maji kutoka Ziwa Victoria yameshafika kwenye Jimbo la Kaliua lakini sasa ninachoshangaa, umbali wa kutoka Kaliua mpaka Ulyankulu ni kilometa kama 98, imewezekana kuyafikisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa nini haya maji yasifike kwenye Jimbo langu ilhali kuna mradi mfano kwenye Jimbo la Nanyumbu pale wametengewa shilingi bilioni 38 ili kupata maji kutoka kwenye Mto Ruvuma ambao ni kilometa 100? Wakati huo huo, inawezekana kabisa kuyatoa maji katika Mji wa Kahama ambapo kutoka kwangu kwenye Jimbo la Ulyankulu mpaka Kahama ni kilometa 42, kwa nini inashindikana? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba kabisa Wizara ya Maji na Mheshimiwa Waziri Aweso ananisikia, haya maji yaweze kufika na Ulyankulu ili na wananchi wetu wafungue maji kutoka bombani. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. REHEMA J. MIGILLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilimwita Mheshimiwa Mheshimiwa Benaya Liuka Kapinga, atafuatiwa na Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo na Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo ajiandae.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia. Ninaanza kwa kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu na Waheshimiwa Mawaziri waliopo katika ofisi hii; Mheshimiwa Lukuvi na Mheshimiwa Ridhiwani

Kikwete kwa kufanya kazi nzuri sana pamoja na Waheshimiwa Naibu Mawaziri pamoja na wataalam wote katika Wizara hii ya Ofisi ya Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu mwenyewe kwa namna anavyofanya kazi vizuri. Hongera sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. Wamesema wenzangu hapa, umelitendea haki sana Taifa hili, na ni kweli kabisa. Sisi wananchi wa Mbinga tunakupongeza mno. Mara kadhaa wewe mwenyewe umekuwa shahidi, unafanya ziara pale Jimboni, Wanambinga wamekupokea kwa bashasha, na ile bashasha siyo ya bure, ila ni kwa sababu ya mambo mazuri unayolifanyia Taifa hili ikiwemo Mbinga Vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Mbinga tunayo kawaida, tunapofarijika na kazi nzuri, huwa tunagalauka ama kukwara. Sasa wananchi wa Mbinga mara kadhaa wamekuwa wakifanya hivyo, wakigalauka na kukwara kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa kipekee nawaomba Wataalamu wa BAKITA wayaweke maneno haya mawili kwenye msamiati sahihi wa Kiswahili. Kwa nini ninasema hivi? Mwaka 2024 Mheshimiwa Rais alifanya ziara Mkoani kwetu. Dada yangu Mheshimiwa Jenista aliongoza wananchi kugaragara. Nikisema kugaragara, ninapunguza ubora wa tendo lenyewe hili, ni kugalauka na ndiyo maana nawaomba sasa wataalam wa Kiswahili waliweke hili neno kama lilivyo, kugalauka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisema kugaragara inakuwa ni kitu fulani kinachoshusha hadhi yake, lakini kugalauka ni kuonesha kuridhika na mambo mazuri ya yule mtu unayemgalaukia pale mbele. Kwa hiyo, nawaomba wataalam wa Kiswahili waliweke neno hili au maneno haya kwenye Kiswahili ili yasilete usumbufu kama yalivyoleta mwaka 2024. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake alipokuja Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Jenista kuonesha kuridhika na utendaji mzuri wa Mheshimiwa Rais, akawaongoza akina mama wale wa Mkoa wa

Ruvuma kugalauka na kukwagha. Khaa! Ilileta shida kweli kweli! Watu wakasema hee, heee! Kumbe ni jambo la kawaida kabisa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Benaya, hilo jina kugalauka ni la Kiswahili?

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kugalauka siyo neno la Kiswahili, ni maneno yanayoingiliana na ya Kiswahili. Kingoni na Kimatengo humo humo ndani yake, ndiyo maana sasa nikawaomba hawa wataalam wetu wa Kiswahili waliingize kwenye kamusi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua mambo mazuri kama haya ni lazima tuyaweke ili watu waendelee kujifunza, tusiyaache tu hivi hivi halafu yanaenda kuleta shida, watu wanaona kwamba siyo kawaida, kumbe sisi kule kwetu mtu akifanya hivyo maana yake anaonesha kuridhika na heshima kubwa juu ya mtu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili linafanyika hata kwenye *level* ya familia. Mtu anafanya siyo ili uonekane au kujipendekeza. Ah ah, Hili ni jambo la kawaida ku-*appreciate* kile kitu kizuri alichofanya huyu. Kwa hiyo, natumia nafasi hii kuwaomba wataalam wetu wa Kiswahili wayaweke maneno haya ya kukwagha na kugalauka kwenye kamusi ili Watanzania wote wajifunze utaratibu huu mzuri unaofanyika Mkoani Ruvuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, naishukuru sana Serikali hii ya Awamu ya Sita, imefanya mambo mengi mazuri. Hata tukianza kuyataja hapa hatutamaliza leo. Nasema tu, naishukuru sana Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu mpenzi na Mama yetu, amefanya mambo mengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa niseme tu kuhusiana na suala la migogoro. Mheshimiwa Rais mara kadhaa amekuwa anatoa maelekezo ya namna gani Serikali hii anayoisimamia iweze kuwahurumia Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale kwangu nilikuwa na mgogoro mmoja wa muda mrefu, wa Ndika. Naishukuru sana Serikali hii ya Awamu ya Sita, kwanza kwa kutuletea viongozi wazuri. Mkuu wa Mkoa, Kanali Abbas, Mkuu wa Wilaya, Mheshimiwa Makori, Mkuu wa Wilaya ya Nyasa na Mkurugenzi wa Halmashauri yetu, wamefanya hii kazi ikawa nyepesi mno. Mgogoro wa miaka saba hadi nane ulitatuliwa kwa muda mfupi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii wananchi wa Maeneo yale ya Ndika wana amani, hawana tena vita na hamna tena kupigana risasi. Naipongeza na kuishukuru sana Serikali hii ya Awamu ya Sita. Baada ya kumaliza huu mgogoro, kulikuwa na maelekezo ya kuyafanyia kazi. Wenzetu wa *TFS* walipewa wajibu na Wakurugenzi kwa nafasi yao, Mkurugenzi wa Nyasa na Mkurugenzi wa Mbinga *DC* naye alikuwa na maeneo yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa sababu miezi sita ndiyo imekamilika hivi karibuni, imekamilika tarehe 12 juzi, wale wananchi ilikuwa walipwe fidia. Wananchi wale wamekuwa watulivu, wameendelea kusubiri na bado wanaendelea kusubiri. Naomba sana wahusika sasa walimalize hili jambo moja kwa moja ili wananchi wale waendelee kunufaika na utendaji mzuri wa Serikali hii ya Awamu ya Sita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tulipofikia, naishukuru sana sana Serikali hii kwa utendaji huu mzuri na leo hii ile vita na mgogoro vimetulia kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine naipongeza sana Serikali hii ya Awamu ya Sita. Mwaka jana 2024 Mheshimiwa Rais alipofika tulimwomba kuhusiana na suala la barabara. Tulikuwa na ujenzi wa Barabara ya Amani Makolo – Ruanda hadi Lituhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais alivyo msikivu, pale pale aliachia fedha ambazo zimeanza kufanya kazi. Tayari kilometa tano zimeshakamilika, lakini ile barabara ina kilometa 35, pia awamu ya pili ina kilometa karibu 50. Naiomba sana Serikali sikivu ya Awamu ya Sita, kwa vile mkandarasi yupo *site,* basi

iharakishe kutoa zile fedha ili kile kipande kilichoanza cha kilometa 35 kiweze kukamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wamenituma, nishukuru kwa hizo kilometa za awali ambazo tayari lami inaonekana, lakini naendelea kuiomba Serikali, zile kilometa zilizobaki sasa watoe fedha kwa sababu mkandarasi bado yuko *site* ili ikamilike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, tunaishukuru Serikali kwa upande wa pili kutoka Ruanda hadi Lituhi na Lituhi hadi Ndumbi, tayari mkandarasi amepatikana, kilichobaki ni mkandarasi kupewa *advance* ili aanze kazi. Tunaishukuru sana Serikali hii ya Awamu ya Sita kwa sababu inaona, inasikiliza na inatekeleza. Tunaishukuru sana Serikali hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, nashukuru mwaka ule wa 2020, Mheshimiwa Rais, huyu huyu Mama Samia alikuja pale akaiona barabara nzuri ya kutoka Kigonsera – Matiri hadi Mbaha yenye kuleta maendeleo, akatamka, "nitaijenga barabara hii kwa lami." Nafurahi kusikia kwamba tayari mkandarasi wa upembuzi yakinifu wa barabara hii, tayari yuko *site* anafanya kazi. Kilichobaki sasa, ni muda mfupi tu, natambua Serikali hii itaweka fedha na hii barabara nayo itapata lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vivyo hivyo kwa barabara inayotoka Mbinga kwenda hadi Litembo, na barabara hii nayo inaenda mpaka Nkiri – Nyasa kwa dada yangu Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya, zote hizi tayari wakandarasi wako *site* na wanaendelea kufanya kazi ya upembuzi yakinifu, ninawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, niongelee suala la barabara ya Nyoni kwenda hadi Maguu. Barabara hii nayo inakwenda Kipapa inamalizikia hadi Ziwani Nyasa. Barabara hii ni ya kimkakati, Mheshimiwa Rais alipofika nilimwomba apeleke fedha kwa sababu tayari upembuzi yakinifu umefanyika na ipo kwenye Ilani, tayari kazi imeanza kufanyika. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais ili sasa ikikamilika ombi letu la yeye kuja

kuifungua barabara hii, liweze kukamilika miaka mitano inayofuata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nashukuru sana.

Waheshimiwa Wabunge, tuna mgeni mmoja ndani ya *gallery* ambaye ni mgeni wa Mheshimiwa Nicodemas Henry Maganga, mpiga kura wake kutoka Mbogwe Mkoani Songwe, yuko pale, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na uchangiaji. Namwita sasa Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo, atafuatiwa na Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo. Mheshimiwa Charles Muguta Kajege, ajiandae. Nimemwona Mheshimiwa Nollo pale muda siyo mrefu. Mheshimiwa Suma, unaweza kuendelea?

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nami nafasi ya kuweza kuchangia kwenye bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye amenipa uzima na afya njema nami nimeweza kusimama mbele ya hili Bunge Tukufu kutoa mchango wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, nampongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan na Amiri Jeshi Mkuu kwa kazi kubwa ambazo amezifanya kwenye Taifa hili la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na miradi mkubwa sana ambayo Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan amekwenda kuikamilisha, sasa hivi kwenye Mradi wa *SGR* ni mteremko, ni mtelezo na Watanzania tunafaidika. Tunaenda Dar es Salaam kwa haraka na tunakuja Dodoma kwa haraka. Pongezi kubwa sana kwa Mheshimiwa Rais. Pia, mradi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere ni mradi mkubwa sana ambao Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ameukamilisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na miradi hiyo mikubwa, kuna miradi ya maji, miradi ya barabara, miradi ya shule na miradi ya vituo vya afya na zahanati, Mheshimiwa Rais amegusa kila mahali na kila mahali ujenzi umeendelea na umekamilika, kwa hiyo, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan anastahili sifa na pongezi kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hizo pongezi za Mheshimiwa Rais, nampongeza kwa sababu, pamoja na kazi kubwa anazozifanya, bado ndani ya Taifa letu la Tanzania amekwenda kuibua Rais wa Mabunge Duniani, Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson. Haijawahi kutokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii imekuwa ni heshima kubwa sana kwetu Wananchi wa Tanzania. Tunasikia sifa na fahari kubwa sana. Hivyo, Mheshimiwa Rais siyo tu ameibua hawa watu ambao wameibuka kwenye Mataifa mbalimbali, ni wengi; siyo tu Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, yeye pamoja na Mawaziri; Mheshimiwa Lukuvi, Mheshimiwa Ridhiwani pamoja na Manaibu Waziri kwa kazi kubwa anayoifanya ambayo inafanya kwa weledi mkubwa sana kwenye kazi inayoendelea kwenye hili Taifa la Tanzania. Mheshimiwa Waziri Mkuu aliwasilisha hapa vizuri sana bajeti yake ambayo imesheheni kila sehemu, ambayo inatakiwa kukamilishwa kwa majukumu yaliyobaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Naibu Waziri Mkuu, Mheshimiwa Dkt. Doto Biteko. Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu huyu amekuwa ni kiongozi ambaye ana hofu kubwa ya Mungu. Mara nyingi kila akisimama kuongea Watanzania wanamwelewa, kwa sababu hapendi mambo ya kujikweza. Amekuwa akiongea kwamba, ukiwa na cheo hupaswi kupandisha mabega, unatakiwa uwe mnyenyekevu, unatakiwa uwe msikivu, kwa maana cheo ni dhamana, leo kipo, kesho hakipo. Mheshimiwa Dotto Biteko, Mwenyezi Mungu akubariki sana kwa namna ambavyo unaeleweka vizuri sana kila unavyosimama kuongea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana Wizara ya Maji. Mheshimiwa Waziri Jumaa Aweso ni msikivu sana, amekuwa akisikiliza ukienda kumwambia juu ya shida ya maji. Naishukuru Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Dkt. Samia Suluhu Hassan. Pale Tukuyu Mjini kulikuwa na tenki ambalo lilitakiwa lijengwe, mara nyingi nilikuwa nikiuliza hapa, lakini bado nilikuwa nikimfuatilia Mheshimiwa Waziri, ili kuuliza hilo tenki linakamilika lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tenki hilo sasa hivi limekamilika. Natoa shukurani sana kwa niaba ya wananchi wa Tukuyu ambapo maji sasa hivi yatakuwapo. Ni maji ambayo lengo kubwa la Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa wanawake wengi ni kumtua ndoo mama kichwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado Serikali ilitoa fedha kiasi cha shilingi 4,700,000,000 ambapo chanzo kilikwenda kutolewa Busokelo, kwa ajili ya maji ya wananchi wa Wilaya ya Kyela. Wilaya ya Kyela wanakwenda kunufaika na mradi mkubwa wa maji haya. Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu namna ambavyo tunamwombea kwa Mwenyezi Mungu, tunaamini anampa macho ya rohoni, Mawaziri wake hawa wanafanya kazi kubwa nzuri na njema sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Hussein Bashe, anafanya kazi nzuri sana. Kazi ya Mheshimiwa Hussein Bashe inaeleweka mpaka kwa macho. Yaani kwenye jambo la kilimo, Mheshimiwa Hussein Bashe anatosha na chenji inabaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sijawahi kuona hata mara moja namna ambavyo hiki kipindi cha Nane Nane ya mwaka 2024, Mheshimiwa Bashe alileta mambo makubwa sana, ukizingatia ma-*power tiller,* kwa ajili ya wakulima, alitoa kwa wananchi *power tiller* 800 kwenye hiyo Wizara, trekta 500 na pikipiki 6,444 kwa wafanyakazi wa huko vijijini na mambo mengine mengi. Hivyo, Mheshimiwa Bashe anatosha na chenji inabaki, anafanya kazi njema sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho naishukuru sana Serikali kwa kuleta fedha kwenye Barabara ya Mbeya Mjini ambayo inaanzia Uyole mpaka Ifisi. Barabara ile inaeendelea kujengwa, lakini pia, ninaomba niishauri Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya kuanzia Igawa – Tunduma, kwanza ni nyembamba, lakini imechakaa kiasi kwamba inasababisha ajali nyingi sana, na kwenye ajali vifo vingi sana vinatokea kwa sababu ya barabara ambayo imechakaa. Naiomba Serikali iitizame barabara hiyo kwa jicho kubwa, kwa jicho pana, kwa jicho la uhuruma na upendo, ili wananchi ambao wanatumia barabara hiyo waweze kupona, ukizingatia hiyo barabara kwa sehemu ni ya Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye barabara hiyo, hata magari ya nje ya nchi mengi sana, yanapita kwenda Congo, Zambia, Burundi, Zimbabwe na Malawi. Kwa hiyo, naiomba sana Serikali muichukulie kwa uzito sana ile barabara, imekuwa nyembamba zaidi, lakini pia imechakaa vibaya sana, inagharimu maisha ya watu, wengi wamebaki vilema na wengine wamepoteza maisha. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naona kengele inanikatisha hapa. Naishukuru Serikali ya Awamu ya Sita ya Dkt. Samia Suluhu Hassan namna ambavyo inafanya vizuri sana. Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan mwezi wa Kumi utusubiri, wewe kaa tu, sisi kwako ni kukupitisha moja kwa moja, kwa sababu, umepita, na kazi yako ambayo unaifanya vizuri sana ni njema, tunajisikia kunenepa tu kila mahali kwa jinsi unavyofanya vizuri, tunajidai popote tunapopita. Hongera sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo, ahsante sana. Sasa namwita Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo, atafuatiwa

na Mheshimiwa Charles Muguta Kajege na mchangiaji wetu wa mwisho atakuwa ni Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq.

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuwa mchangiaji. Kwa dhati kabisa nachukua nafasi hii kuipongeza Serikali kwa kazi kubwa ambayo imefanya katika sekta mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa umadhubuti wa kuliongoza hili Taifa na namna ambavyo shughuli za Serikali, kama nilivyosema, hasa katika miradi ya maendeleo, imeweza kufanyika katika maeneo mengi na kwa upana zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilitaka nijikite zaidi katika ufanisi wa Serikali. Pamoja na mambo yote ya mafanikio makubwa ya miradi, bado tunahitaji ufanisi zaidi wa Serikali katika kuwapa wananchi huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nina mambo mawili ambayo, kama nchi, ni lazima tuangalie ni namna gani tunaweza tukaliweka suala hili. Tumekuwa na sikukuu mbalimbali, zile *public holidays*, lakini kutokana na hilo jambo ukienda kwenye hospitali nako kunakuwa na sikukuu. Kwa hiyo, tunapoteza maisha ya wananchi wengi wa Taifa letu kwa sababu tu kunakuwa na sikukuu, basi na huduma nazo zinaenda sikukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iangalie ufanisi wa jambo hili. Wapo watumishi ambao mtawapanga kipindi cha sikukuu wafanye kazi kama kawaida, lakini sikukuu imeingia Alhamisi, hospitali hakuna huduma mpaka Jumatatu. Tunapoteza maisha ya wananchi wetu. Jambo hili ninaishauri sana Serikali, tutoke kwenye huu utamaduni kwamba, ikiwa sikukuu wote tunaenda sikukuu. Zipo sekta ambazo hazitakiwi kwenda sikukuu. Naomba hili suala tuliangalie sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, sisi Wabunge ni mashahidi, kumekuwa na malalamiko kuwa mgonjwa akifariki inatakiwa gharama zile alizokuwa anatibiwa zilipwe. Serikali

imetoa tamko kwamba, hakuna jambo kama hilo, lakini hili jambo linaendelea. Mtu ameshafariki, unataka faida gani tena na huyo alikuwa ni mlipakodi wako, kama Serikali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni kuachilia kwamba, ameshafariki. Jambo hili limejirudia mara nyingi sana na Serikali imekuwa inatoa majibu kwamba, hakuna maiti inayozuiwa, lakini ukweli ni kwamba, maiti zinazuiliwa baada ya mgonjwa kufariki. Sasa ifike mahali Serikali iseme kabisa jambo hili na zile hospitali waambiwe kwa maana wanasema hayo ni matamko ya wanasiasa tu, lakini ni wanasiasa gani? Ni suala la Serikali. Kwa hiyo, naomba jambo hili nalo liweze kuangaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine, mwaka huu sisi Mkoa wa Dodoma tumepata mvua kidogo na ukweli ni kwamba, hatujapata kabisa mazao. Sasa njaa imeanza. Kwa mfano kilo 20, sisi tunaita debe, kwa sasa linauzwa mpaka 22,000. Ina maana kufika mpaka Novemba, bei inaweza ikaongezeka zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ni kwamba, nilitaka niseme, kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu, tathmini ifanyike katika maeneo yetu, kwanza tujue upungufu wa chakula mapema ili kama ambavyo *NFRA* huwa inaleta chakula cha bei nafuu, jambo hili lifanyike mapema zaidi, ikiwezekana ndani ya Mwezi wa Sita wananchi wetu wauziwe chakula cha bei nafuu. Kwa kufanya hivyo, wataweza kuwahi kuliko bei kupanda, ili kila watakachonunua waweze kukihifadhi walau kiwafikishe katika miezi mingine ambayo inafuata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla katika Jimbo langu la Bahi, naishukuru sana Serikali na kama kupendelewa na Mheshimiwa Rais, mimi Bahi nimependelewa sana. Nimefanyiwa mambo makubwa. Suala zima la afya, hospitali yetu ile ya wilaya imeboreshwa kwa kiasi kikubwa. Ongezeko la majengo ikiwepo *emergency* na wodi mbalimbali za wanaume nazo zimeongezeka. Pia tumepata kituo cha afya, na juzi tumeahidiwa hapa na fedha ninasikia zimeanza kuingia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutapata kituo kingine cha afya na kile kituo mimi niliwahi kuki-*propose,* kitaenda katika Kata ya Mtitaa ambacho kitahudumia Tarafa nzima ya Mwitikila.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumejenga zahanati 17. Vijiji 19 havikuwa na zahanati, kwa hiyo, tumejenga zahanati 17 tumebakisha vijiji viwili tu ambavyo havina zahanati; Kijiji cha Mchito na Kijiji cha Ngome. Ni matumaini yangu kwamba, hivi navyo tutavimalizia ili kwamba, huduma ianze kupatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa umeme, tumepewa vitongoji 15 na kazi kubwa inafanyika. Naipongeza Idara ya *TANESCO*, Wilaya ya Bahi wanafanya kazi kubwa na tunaiomba Serikali iongeze zaidi kama ambavyo tuliahidiwa vitongoji 90 mpaka 70, basi hili jambo liweze kuja haraka, wananchi wetu wana shauku ya kupata umeme katika maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la maji, kwanza naishukuru sana Serikali kwa namna ambavyo mmeweza kusambaza na kuleta miradi mingi. Kipekee nawashukuru Shirika la *Water Mission* kwa Bahi, wamefanya kazi kubwa. Tumepata miradi nane ambayo imeleta manufaa makubwa kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la Barabara, madaraja mengi yamejengwa. Kwa Bahi tulikuwa na shida kubwa ya makorongo, lakini kwa sasa tumebakiza madaraja machache. Daraja la Mayamaya – Mkondai ninaambiwa fedha ziko tayari na mkandarasi amepatikana. Tuna daraja la Chifutuka lililojengwa na mkoloni, hilo nalo linatakiwa liwekwe jipya. Kwa hiyo, naishukuru Serikali kwenye suala la Barabara, tumeweza kufungua barabara kubwa za kimkakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la elimu. Nimepata shule nne mpya za sekondari na shule za msingi 14. Naomba Serikali iendelee kuboresha suala zima la elimu kwa maana, sisi Wilaya ya Bahi tunafanya vizuri Kitaifa, tumekuwa wa pili mwaka huu katika shule za msingi. Kwa hiyo, Serikali ina sababu maalumu, kwa sababu tunafanya vizuri, iendelee kutupatia shule za kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la ufugaji. Naishukuru Serikali, nilipata madume 20 ya mbegu bora. Madume yale yanafanya kazi kubwa na tunafanya utaratibu, linatoka hapa wiki moja, linakaa wiki nyingi linaenda kwenye maboma mengine. Kwa hiyo, tuongezewe ili tuweze kupata madume ya kutosha na wakulima wetu waweze kupata ufugaji mzuri wa kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu na Ofisi yake kwa namna uratibu wa Serikali unavyoenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kikubwa zaidi, naunga mkono hoja, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kenneth Nollo, ahsante sana. Sasa nimwite Mheshimiwa Charles Muguta Kajege.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia katika hoja hii ya Hotuba ya Waziri Mkuu. Kwanza nichukue fursa hii kumpongeza Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini vilevile nataka niwapongeze Waziri Mkuu Kassim Majaliwa na Naibu Waziri Mkuu, Mheshimiwa Dkt. Doto Biteko kwa kazi nzuri ambayo wameifanya. Hawa wamekuwa ni kiunganishi kizuri sana kati yetu na Serikali na hakika hakuna hata siku moja ambayo nimekwenda kuwaona, na wakashindwa kunisaidia katika kutatua changamoto yangu. Nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali yetu imefanya kazi kubwa sana katika kipindi cha hii miaka minne. Miradi mingi imetekelezwa. Sasa nitaigawa katika maeneo mawili, kwanza Kitaifa na lingine katika jimbo langu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa kwanza ni wa Bandari ya Dar es Salaam. Baada ya *DP* kupewa hii Bandari ya Dar es Salaam imekuwa na mafanikio makubwa. Katika kipindi cha kuanzia Julai mwaka 2024 mpaka Machi mwaka huu, jumla ya makasha 686,515 yameingia, ukilinganisha na makasha 670,724 katika kipindi hicho hicho katika mwaka uliopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile mapato yameongezeka kutoka shilingi bilioni 850 hadi kufikia shilingi trilioni moja. Vilevile muda wa meli kutia nanga kusubiri kuingia bandarini umepungua kutoka siku 30 hadi kufikia siku tatu. Hii ni *improvement* kubwa sana katika upande wa bandari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi mwingine ni Mradi wa Umeme wa Julius Nyerere ambao thamani yake ni shilingi trilioni 6.6. Mpaka kufikia Machi mwaka huu, jumla ya megawati 2,115 zimeingia katika Gridi ya Taifa na huu umeme umeweza kuingia katika vijiji vyote 12,318, lakini vilevile na vitongoji 33,657 ikiwa ni asilimia 52.3 ya vitongoji vyote nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika miradi jimboni kwangu nataka nikiri kwamba, kama kuna jimbo ambalo limepata miradi mingi, ni pamoja na Jimbo langu la Mwibara. Kwa upande wa elimu katika kipindi cha miaka minne, tumeweza kujenga shule nane mpya za sekondari ikiwa ni pamoja na shule moja ya wasichana ya *special, Mara Girls,* ambayo thamani yake ni shilingi bilioni 4.4.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tumepata *VETA* ambayo thamani yake ni shilingi bilioni 3.3. Pamoja na hiyo, tumeweza kupata madarasa mengine mapya 315, ambayo kama ingekuwa ni shule za msingi, ukigawa katika madarasa ambayo hayana mkondo, maana yake ni kwamba, tumepata shule nyingine mpya za msingi 45 na matundu 260 ya vyoo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa afya. Jimbo langu limeweza kupata vituo vingine viwili vipya vya afya; Kituo cha Isanju na Kituo cha Kisolya. Pamoja na hivyo, huduma zime-*improve* ikiwa ni pamoja na kupata *x-ray* na *ultrasound.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuna zahanati mpya zimejengwa, ambazo ni Zahanati ya Mranda, Nambaza, Lagata, Mwiseni na Sozia, lakini kuna zahanati nyingine ambazo zitakamilika hivi karibuni. Kwa hiyo, naishukuru sana Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa barabara. Mwaka 2021 wakati tunaingia madarakani, Jimbo la Mwibara lilikuwa halipitiki kabisa, barabara zote zilikuwa kama zimekufa, madaraja yalikuwa yamepasuka hayapitiki na baadhi yalikuwa yanabeba wanafunzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtangulizi wangu aliyekuwa ametangulia, aliwahi kusema kwenye mkutano wa hadhara kwamba, hizi barabara au haya madaraja hayataweza kujengwa labda mpaka Yesu atakapokuja, lakini kupitia Serikali ya Dkt. Mama Samia haya madaraja na barabara zimeweza kujengwa katika mwaka mmoja. Nampongeza sana mama Samia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia barabara tumeweza kujenga tena barabara nyingine kuunganisha maeneo mengine. Kwa mfano, barabara ya kutoka Bugala – Sikilo, Barabara ya kutoka Nambaza – Igundu na barabara nyingine ambayo itajengwa kutoka Kalukekere – Musoma Vijijini. Hizi ni jitihada za Mheshimiwa Rais kuhakikisha kwamba, maeneo yote yanafikika kwa uhakika, lakini vilevile barabara nyingine zote sasa hivi zinapitika kwa urahisi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jimbo langu hakuna sehemu ambayo barabara haipitiki, sasa hivi unaweza ukaenda hata na *IST* wakati kufikia mwaka 2020 ulikuwa hauwezi kwenda hata na *Land Cruser*. Kwa hiyo, hali ya barabara jimboni kwangu imekuwa nzuri sana na huduma zimekuwa nzuri zaidi. Naishukuru sana Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Mama Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa maji, vilevile tumepata miradi mikubwa ya maji ikiwa ni pamoja na mradi wa kutoka Buzimbwe – Lagata na Kabainja. Mradi huu unategemewa kukamilika hivi karibuni. Vilevile kuna mradi wa Isanju – Nyalugoma ambao umeshakamilika na vilevile kuna mradi mkubwa ambao umemaliziwa kusanifiwa, mradi ambao utapitia katika vijiji 33 ambao vilevile ukiwa katika kata sita ambazo ni Kata Kisolya, Nampindi, Igundu, Nansimo, Chitengule na Kibara. Mradi huu utakapokamilika utakuwa ni *game changer*

kwa ajili ya kutatua changamoto ya maji katika Jimbo la Mwibara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio hayo, bado jimbo langu lina changamoto. Changamoto ya kwanza ni maji. Kama nilivyozungumza, kuna mradi wa maji ambao umekamilika kusanifiwa, lakini bado haujakamilika. Kwa hiyo, maeneo yote ambayo bado mradi haujaanza, maana yake ni kwamba yana matatizo ya maji. Naiomba sana Serikali ifanye kila iwezalo ili mradi huu uweze kujengwa na kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto nyingine ni kwenye kilimo. Kilimo ni sekta muhimu sana katika jimbo langu ambayo inasaidia wananchi wengi katika kupata kipato chao. Pamoja na kwamba jimbo langu kila kata imegusa kwenye maji, lakini bado tuna tatizo la maji sehemu nyingine nyingi. Hivyo, naomba Serikali itusaidie kujenga *scheme* za maji; na hii nimeshaongea na Mheshimiwa Waziri Bashe, tupate *scheme* za maji katika maeneo ya Kisorya, Mwitende, Kigaga, kuna Bulamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukishapata hizi *schemes* nina imani kwamba hatutakuwa na haja tena ya kuomba vyakula Serikalini. Kwa hiyo, naomba Serikali itusaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kuhusu umeme. Ni kweli kwamba vijiji vyote 12 vimepata umeme, lakini bado kuna vitongoji havijapata umeme. Kama ujuavyo umeme ni kila kitu sasa hivi katika maisha, tunaomba Serikali itusaidie umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile katika umeme, nataka nimkumbushe Mheshimiwa Waziri Mkuu, na hii ni Wizara yake. Aliahidi mwaka 2020 wakati akiwa anafanya ziara jimboni kwangu kwamba ataipatia Nafuba umeme wa sola. Kwa hiyo, kwa sababu Mheshimiwa Waziri Mkuu naye yupo hapa, nafikiri atasikia na nina imani kwamba tutapata umeme hivi karibuni katika hilo eneo la Nafuba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni mawasiliano. Jimbo langu vile vile lina visiwa vingi ikiwa ni pamoja na Nafuba, Buguma,

Sozya na sehemu nyingine. Kutoka kwenye hivi visiwa kuja nchi kavu, kuna tatizo kubwa la usafiri. Serikali imeniahidi mara kadhaa kuhusu kunipatia vivuko. Naomba sasa Serikali itekeleze ahadi zake ili tupate vivuko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja tena katika upande wa elimu. Pamoja na kwamba tumepata shule mpya nyingine nane, lakini bado tunahitaji. Upande wa elimu, bado haijakaa vizuri. Kuna shule kongwe ambazo madarasa yake yamechakaa sana, naomba Serikali ianze kutusaidia kurekebisha madarasa hayo katika shule za Chitengule, Nansimo, Namibo A, Kinkombyo, Namhula Stoo, Kabainja, Ragata na Buzimbwe. Ukienda katika shule hizi, hali yake siyo nzuri, madarasa kabisa ni kama hayatakiwi...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Muda wako umeisha, malizia.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali itusaidie katika kuboresha haya madarasa kwenye hizi shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile tunahitaji minara ya simu. Bado mawasiliano siyo mazuri katika jimbo langu. Kwa hiyo, tunahitaji minara mingine mingi ya simu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa afya, bado tuna upungufu wa madaktari, wauguzi na vifaatiba. Tunahitaji tena bado tupewe vituo vingine vya afya. Kuna ahadi za Serikali mwaka 2024 wakati wa ziara ya Mheshimiwa Waziri Mkuu katika jimbo langu...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kajege...

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie dakika moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2024 wakati wa ziara ya Mheshimiwa Waziri Mkuu jimboni kwangu aliahidi kwamba kutajengwa kituo cha afya katika sehemu za Bulamba. Kituo hicho bado hakijajengwa. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu atekeleze ahadi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, na hivyo naunga mkono hii hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Charles Muguta Kajege. Namwita sasa Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana nami kwa kunipa fursa ya kuchangia hoja iliyopo mbele yetu. Niendelee kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, Mwingi wa Ukarimu kwa kunipa fursa na afya njema kuweza kuongea katika hili Bunge Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu katika kuendelea kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi nzuri anayoifanya kwa ajili ya maendeleo endelevu ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee, naomba pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Niabu Waziri Mkuu, pamoja na Waheshimiwa Mawaziri wote kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu; Mheshimiwa Lukuvi, Mheshimiwa Ridhiwani, Waheshimiwa Manaibu Mawaziri, Makatibu Wakuu pamoja na Watendaji wote wa Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba nzuri ambayo wameiandaa ambayo imesheheni taarifa nzuri, dhima kuu ikiwa ni kuleta maendeleo endelevu kwa ajili ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halikadhalika, naomba niwapongeze pia Watendaji Wakuu wa taasisi ambazo zipo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu ambao nao wamekuwa wakifanya kazi nzuri sana kwa ajili ya kuleta maendeleo ya Watanzania. Naomba niwataje kwa majina; Ndugu Masha Mshomba, Mtendaji Mkuu wa

*NSSSF;* Ndugu Bandru, Mtendaji Mkuu wa *PSSSF*; Bi. Khadija Mwenda Mtendaji Mkuu wa OSHA; na Dkt. John Mduma, Mtendaji Mkuu *WCF*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watendaji hawa kwa kweli ni wazalendo na tumeona kabisa kazi ambazo wanazisimamia, wamezifanya kwa weledi mkubwa sana. Kwa hiyo naomba pia niwapongeze sana kwa sababu taasisi ambazo wamekuwa wakiziongoza zimekuwa zina matokeo chanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukurasa wa 14 wa hotuba hii Serikali imezungumzia kuhusu mazingira wezeshi ya kupanua wigo wa ajira kwa kipindi cha mwaka 2020 hadi Februari, 2025, kwamba, jumla ya ajira milioni 8,640,204 zilikuwa zimezalishwa. Naipongeza sana Serikali kwa kazi hii kubwa ambayo imefanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizo, nina ushauri kwamba, kwa kuwa vyuo vikuu, vyuo vya kati, na taasisi mbalimbali zimekuwa zikizalisha wahitimu wengi, bado uhitaji wa ajira ni mkubwa sana. Tunatambua kabisa kwamba pamoja na juhudi kubwa ya Serikali ambayo imeandaa mazingira wezeshi kwa ajili ya vijana kujiajiri au kuajiriwa, bado kuna ombwe kubwa sana la vijana hawa katika kuajiriwa. Kwa hiyo, niendeee kuipongeza kwamba kumekuwa kuna programu mbalimbali za kuhakikisha kwamba vijana wanaajiriwa, ikiwemo miradi ya *BBT* na mingineyo na mazingira wezeshi na mikopo na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo kubwa ambalo nilikuwa nataka, na ninatamani kuishauri Serikali ni kwamba katika Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu kuna ule Mfuko wa Maendeleo ya Vijana. Mfuko huu umekuwa ukitengewa bajeti, lakini bajeti yake ilikuwa haitoshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba niishauri Serikali, ili kusudi vijana wengi waweze kujiajiri, waweze kukopesheka na pia kuajiri wenzao, ni budi Serikali ikaangalia upya kuuongezea mfuko huu fedha ya kutosha ili kusudi kundi kubwa la vijana waweze kupata mikopo hii na hatimaye waweze kujiajiri na kuajiri vijana wenzao wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, nilikuwa natamani kuendelea kuishauri Serikali. Natambua kabisa kwamba ajira zilizopo ni haba, lakini pia kuna nchi za wenzetu huko ughaibuni ambazo wamekuwa wakihitaji vijana wa fani mbalimbali kwenda kufanya kazi huko, yaani *diaspora.* Kwa hiyo, bado naona kwamba kasi ya kuwaunganisha vijana na zile nchi ambazo zinahitaji wataalamu au vijana mbalimbali kwenda kufanya kazi kule, bado ni ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa naomba niishauri Serikali kuweka mkakati maalum wa namna ya kuandaa dirisha maalumu la kuhakikisha kwamba vijana wengi zaidi wanaunganishwa na hizi ajira za nje ili kusudi waweze kwenda kufanya kazi kule ughaibuni. Wakifanya kazi kule ughaibuni maana yake ni kwamba yale mapato ambayo yatatokana na zile kazi wanazozifanya kule ughaibuni yatasaidia nchi yetu kupata kipato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa uchache tu ni kwamba, wenzetu Nigeria wamefanikiwa, kwamba walau wanapata dola bilioni 25. Pia wenzetu Kenya mwaka 2023 ilipokea dola bilioni 4.2 kutoka *diaspora;* na sisi Tanzania tunaweza na tunaweza tukapata zaidi tukitafuta zile fursa kwa ajili ya vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nilitamani kulizungumzia, lipo kwenye ukurasa wa 23 wa taarifa hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ambayo imezungumzia kuhusiana na suala zima la upatikanaji wa maji. Naipongeza sana Serikali, nampongeza sana Rais wangu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuhakikisha kwamba anamtua ndoo mwanamke kichwani kwa kuhakikisha kuwa anapata maji kutoka katika maeneo ya karibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija katika Mkoa wetu wa Dodoma, bado suala la upatikanaji wa maji limekuwa ni tatizo kidogo katika baadhi ya maeneo na hasa katika Jiji la Dodoma. Natambua kwamba uhamiaji wa Makao Makuu umesababisha pia uhaba huo. Hata hivyo, kwa kuwa Serikali ilikuwa imebaini

kwamba watajenga lile Bwawa la Farqwa, basi nilikuwa naomba niishauri Serikali ifanye haraka kujenga lile bwawa ili kupunguza hili ombwe la upungufu wa maji katika maeneo mbalimbali ya Mkoa wa Dodoma, Jiji la Dodoma viunga vyake na hasa eneo la Nkuhungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, wananchi wamekuwa hawana taarifa yoyote kuhusiana na maendeleo ya Bwawa hili la Farqwa. Ni vizuri Serikali iwe inatoa taarifa za mara kwa mara ili wananchi nao wajue ni nini kinaendelea ili waache kulalamika. Nadhani wakipata taarifa na maarifa, itawasadia kujua kwamba Serikali yao Tukufu ipo mbioni katika kutafuta pesa na miundombinu mbalimbali ili kuhakikisha kwamba bwawa hili linafanya nini? Linajengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa uchache niliona niseme hayo. Baada ya kusema hayo, nakushukuru sana kwa kunipa fursa, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, wachangiaji wa jioni ya leo wamekwisha na kwa hiyo tumefikia mwisho. Nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango yenu ambayo mmeitoa hapa. Nawashukuru sana upande wa Serikali wapo kikamilifu kabisa, Mheshimiwa Waziri Mkuu tunamwona yupo hapa. Pamoja na kuzunguka, tumemwona anafanya kazi nyingine, lakini amekuja Bungeni na mpaka muda huu tunaye. Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu naye tunaye hapa. Kwa hiyo, tunawashukuru sana kwa namna mnavyoichukulia kazi hii ya Waheshimiwa Wabunge na kuchukua mawazo yao.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, naahirisha Bunge mpaka kesho Jumanne, tarehe 15 Aprili, saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 12.50 Jioni Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumanne, Tarehe 15 Aprili, 2025 Saa Tatu Asubuhi)*